



ادارة اوقاف

صالح عبدالعزيز

**MAHARAMISHO YALIYODHARAULIWA NA
WAISLAMU WENGI**

AMBAYO NI WAJIBU KUJIHADHARI NAYO

**MTUNZI
SHEIKH MUHAMMAD BIN SALEH
AL MUNAJJID**

**KIMETAFSIRIWA NA
ALI MUHAMMAD BIN SALMIN.**

مطبعة دار حلبيه - الرياض - ت: ٤٢٨٤٨٤٠

GIFT NOT FOR SALE

**MAHARAMISHO YALIYODHARAULIWA NA
WAISLAMU WENGI**

AMBAYO NI WAJIBU KUJIHADHARI NAYO

**MTUNZI
SHEIKH MUHAMMAD BIN SALEH
AL MUNAJJID**

**KIMETAFSIRIWA NA
ALI MUHAMMAD BIN SALMIN.**

**MAHARAMISHO
YALIYODHARAULIWA NA WAISLAMU
WENGI AMBAYO NI WAJIBU
KUJIHADHARI NAYO**

**MTUNZI:
SHEIKH MUHAMMAD BIN SALEH
AL-MUNAJJID**

**KIMETAFSIRIWA NA
ALI MUHAMMAD BIN SALMIN.**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu na rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya mjambe wake Muhammad na juu ya aali zake na maswahaba wake watukufu na wale wenyewe kufuata uongofu wao. Ama baad;

Nimekipitia kitabu hiki alichokiandika fadhilat Sheikh Muhammad bin Saalih Al-Munajjid Mwenyezi Mungu amuafikishe, chenye anuani isemayo:

“MAHARAMISHO

**YALIYODHARAULIWA NA WAISLAMU
WENGI, AMBAYO NI WAJIBU
KUJIHADHARI NAYO”**, na nikakikuta kuwa ni kitabu kizuri chenye faida nydingi ,

na mwandishi wake amefanikiwa vizuri sana na kunufaisha . Mwenyezi Mungu amlipe kila la kheri na amzidishie elimu zaidi na amali njema, na wanufaike waislamu na kitabu chake hiki,na vitabu vyake vingine, hakika Mwenyezi Mungu ni mwingi wa upaji na ukarimu.

Na rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Mtume Muhammad ﷺ pamoja na aali zake na maswahaba wake.

Imeandikwa tarehe 11/9/1414H

Na Sheikh Abdul Azizi Bin Baaz

**Mufti mkuu wa Saudi Arabia na raisi wa
Baraza kuu la maulamaa la utafiti wa
kielimu na
utoaji wa fatwa na kulingania na kuongoza.**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, ambae ndie tunaemtukuza na kumtaka msaada, na kumuomba msamaha wa dhambi zetu, na tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na shari za nafsi zetu, na uovu wa matendo yetu. Mwenye kuongozwa na Mwenyezi Mungu huwa hana wa kumpotosha na mwenye kupotoshwa na Mwenyezi Mungu huwa hana wa kumuongoza, na ninashuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake asiyekuwa na mshirika wake, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni mjambe wake. Ama Baad; Kwa hakika Mwenyezi Mungu mtukufu ameamuru baadhi ya mambo kuwa ni faradhi na wajibu ambayo hayafai kuachwa au kupotezwa na akaweka mipaka kwenye

baadhi ya mambo ambayo haifai kuvukwa. Na akaharamisha baadhi ya vitu ambavyo havifai kukiukwa.

Kwa sababu hii basi ndio maana Mtume ~~nasema~~ anasema :

ما أحل الله في كتابه فهو حلال، وما حرم فهو حرام وما سكت عنه فهو عافية فاقبلوا من الله العافية، فإن الله لم يكن نسيأ ثم تلا هذه الآية (وما كان ربك نسيأ) ﴿

(Halali ni ile aliyoihalalisha Mwenyezi Mungu kwenye kitabu chake na Haramu ni ile aliyoiharamisha Mwenyezi Mungu. Na yale aliyooyanyamazia ni msamaha (kwenu) basi ukubalini msamaha wa Mwenyezi Mungu, kwa hakika Mwenyezi Mungu hakuwa ni mwenye kusahau (kwa kuyanyamazia mambo hayo) kisha akasoma Mtume ~~nasema~~ aya hii; “Na Mola wako si mwenye kusahau.” Al Haakim 2/375 Ghaayatul maraami - Al Baaniy uk 14.

Kwa hiyo basi mipaka ya Mwenyezi Mungu ni yale mambo aliyooyaharamisha na kuyakataza. Anasema Mwenyezi Mungu:

﴿ تَلَكَ حَدُودُ اللَّهِ فَلَا تَقْرِبُوهَا ﴾ [سورة البقرة الآية: ١٨٧]

“Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu basi msiikaribie.” Al Baqarah : 187.

Na Mwenyezi Mungu amewakemea vikali wale wenyewe kuvuka mipaka yake na kufanya mambo maovu aliyoyaharamisha kwa kuwaambia kuwa watakuwa na adhabu kali siku ya kiyama. Anasema Mwenyezi Mungu :

﴿ وَمَنْ يَعْصِي اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدُ حَدَّوْدَهِ يَدْخُلُهُ نَارًا ﴾

﴿ خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ مُهِينٌ ﴾ [النساء الآية: ١٤]

“Na anaemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuiruka mipaka yake (Mwenyezi Mungu) atamwingiza motoni humo atakaa milele na atapata adhabu ifedheheshayo.” Annisaa : 14

Kwa hiyo kujiепusha na kujiweka mbali na mambo aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu na kutoyakaribia maovu ni wajibu kwa kila mtu kwa ushahidi wa maneno ya Mtume ﴿:

"**وَمَا نَهِيْتُكُمْ عَنِ الْفَاجِتَبَوْهِ وَمَا أَمْرَتُكُمْ بِهِ فَافْعُلُوْا مِنْهُ
مَا أَسْتَطِعْتُمْ**"

(Yale niliyokukatazeni kufanya jiepusheni nayo, na yale niliyokuamrisheni kuyafanya basi yafanyeni kwa kiasi mnachoweza). Muslim No. 130.

Lakini mambo tunayoshuhudia hivi sasa kutoka kwa baadhi ya watu wenyewe kufuata matamanio ya nafsi zao, wenyewe nafsi dhaifu na wachache wa elimu wanaposikia mambo yaliyoharamishwa yakinajwa mbele yao moja baada ya moja utawaona wakighadhibika na kulalamika huku wakisema, 'hivi kila kitu ni haramu tu! Hamjaacha kitu chochote isipokuwa mmekitia uharamu, mmeharibu maisha yetu na kutuchokesha na kuzidhikisha nafsi zetu, basi nyie hamna jambo lolote isipokuwa ni haramu na kuhamramisha tu, dini ni nyepesi na mambo ni mengi na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa msamaha na rehema!!

Watu kama hawa tunaweza kuzijadili hoja zao na kuzijibu kama ifuatavyo:-

Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye sifa zote za utukufu huhukumu vile apendavyo na wala hakuna mtu wa kupinga hukumu zake. Yeye ni mwingi wa hekima na mjuzi wa kila jambo, yeye huhalalisha mambo ayatakayo na kuharamisha mambo ayatakayo. Na katika misingi ya kumuabudu kwetu ni kuridhika na kufuata vile alivyohukumu na kunyenyeka hukumu zake kwa ukamilifu.

Na hukumu zake Mwenyezi Mungu hutoka

kwenye ilimu yake na hekima zake na uadilifu wake mtukufu, na wala huwa hazitoki kwa upuuzi na mchezo mchezo tu kama anavyosema kwenye Qurani:

﴿وَتَمَتْ كَلْمَةُ رَبِّكَ صَدِقًا وَعَدْلًا لَا مُبْدِلٌ لِكَلْمَاتِهِ وَهُوَ السَّمِيعُ﴾

العلیم ﴿١١٥﴾ [سورة الانعام]

“Na yametimia maneno ya Mola wako kwa kweli na uadilifu, hakuna awezae

kuyabadilisha maneno yake, na yeye ndie asikiae na ajuwae.” Al An’am : 115.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ametubainishia kipimo ambacho ni marejeo makubwa katika kuharamisha na kuhalalisha kitu pale aliposema:

﴿... وَيَحْلِلُ لَهُمُ الطَّيِّبَاتُ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبَائِثُ...﴾

[سورة الأعراف الآية: ١٥٧]

“Na huwahalalishia vizuri na kuwaharamisha vibaya.” Al Aa’raf : 157
 kwa hivyo kitu kizuri chenye manufaa hicho huwa ni halali na kitu kibaya chenye madhara hicho huwa ni haramu. Na hakuna mwenye haki ya kuhalalisha au kuharamisha kitu isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake, na mwenye kudai kwenye nafsi yake kuwa ana uwezo wa kuhalalisha au kuharamisha kitu kinyume na Mwenyezi Mungu au akakiri kuwa fulani ana uwezo wa kufanya hivyo kinyume na Mwenyezi Mungu, basi mtu huyo huwa amekufuru, tena kufuru kubwa

yenye kumtoa kwenye uislamu. **Mwenyezi Mungu** anasema:

﴿إِنَّ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَّ عَوْالَهُمْ مَنْ الَّذِينَ مَا لَمْ يَأْذَنْ لِهِمْ﴾ [٢١] [سورة الشورى الآية: ٢١]

“Oh! Wana washirika (wa Mwenyezi Mungu) waliowawekea dini asiyoitolea Mwenyezi Mungu ruhusa (yake)?” Ash-shuura : 21

Kisha haifai kwa yoyote kuhalalisha au kuharamisha kitu isipokuwa kwa wale wanazuoni walio wajuzi wa kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna za Mtume wake peke yao, kwa sababu Mwenyezi Mungu amemkemea vikali na kumkataza yule mtu anaejaribu kuthubutu kuhalalisha jambo au kuharamisha bila ya kuwa na ujuzi wowote kielimu, kwa kusema:

﴿وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِيفُ الْسِّنَّتُكُمُ الْكَذِبَ هَذَا حَلَانٌ وَهَذَا حَرَامٌ لِتُقْرُوا عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ...﴾ [١١٦] [سورة النحل: ١١٦]

“Wala msiseme kwa sababu ya uongo usemao ndimi zenu, hii ni halali na hii ni

haramu, msije mkamzulia uwongo **Mwenyezi Mungu.**” An-Nahl : 116

Na mambo ya haramu yaliokatiwa hukumu kuwa ni haramu yametajwa kwenye Qurani tukufu na sunna sahihi kama vile kauli ya **Mwenyezi Mungu** isemayo:

﴿ قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ أَلَا تَشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدِينَ إِحْسَانًا وَلَا تَقْتُلُوا أُولَادَكُمْ مِنْ إِمْلَاقٍ... ﴾ [سورة الأنعام: ١٥١]

“Sema; (uwaambie) Njooni nikusomeeni aliyokuharamishieni Mola wenu (na aliyokuamrishi; si yale ya uwongo mnayojidai nyinyi kuwa **Mwenyezi Mungu** amekuamrishi) ya kwamba msimshirikishe na chochote na wafanyieni wema wazazi wenu, na wala msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini.”

An-Am : 151

Na kwenye sunna vile vile yametajwa mambo mengi yenyeye kuharamishwa kama vile kauli ya **Mtume** isemayo”

”إِنَّ اللَّهَ حَرَمَ بَيْعَ الْخَمْرِ وَالْمَيْتَةِ وَالْخَنَزِيرِ وَالْأَصْنَامِ“

(Hakika Mwenyezi Mungu ameharamisha kuuza pombe na nyamafu na nguruwe na masanamu.” Abu Daud 3486.

Na kauli ya Mtume ﷺ:

”إِنَّ اللَّهَ إِذَا حَرَمَ شَيْئًا حَرَمَ ثُمَّنَهُ“

(Hakika Mwenyezi Mungu anapoharamisha kitu chochote basi huharamisha pia kula thamani yake.” Darkutniy 3/7.

Wakati mwingine huja baadhi ya aya na hadithi zenyeye kutaja vitu vilivyo haramishwa kulingana na aina fulani ya kitu. Kama vile alivyotaja Mwenyezi Mungu baadhi ya vitu vilivyo haramishwa

kutoka kwenye aina ya vyakula akasema:

﴿حَرَمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالدَّمْ وَلِحْمَ الْخَنْزِيرِ وَمَا أَهْلَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمَنْخَنَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ وَالْمُتَرْدِيَّةُ وَالنَّطِيْحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبْعُ إِلَّا مَا ذَكَرْتُمْ وَمَا ذَبَحْتُ عَلَى النَّصْبِ وَأَنْ تَقْسِمُوا بِالْأَزْلَامِ...﴾ [سورة المائدة: ٣]

Mmeharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe na kinyama kilichochinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kilichokufa kwa kusongeka koo

na kilichokufa kwa kupigwa, na kilichokufa kwa kuanguka , na kilichokufa kwa kupigwa pembe (na mwengine), na alichokila mnyama (kikafa) ila mkiwahi kukichinja (kabla hakijafa) na kilichochinjwa panapofanyiwa ibada isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu. Na ni (haramu kwenu) kutaka kujua siri kwa kuagua kwa mabao (na yaliyo kama hayo)."

Al-maida : 3

Kisha akataja Mwenyezi Mungu watu walioharamishwa kwenye ndoa, ambapo mtu hawezi kuwaoa. Akasema:

﴿حَرَّمْتُ عَلَيْكُمْ أَمْهَاتِكُمْ وَبَنَاتِكُمْ وَأَخْوَاتِكُمْ وَعَمَاتِكُمْ وَخَالَاتِكُمْ وَبَنَاتِ الْأَخْ وَبَنَاتِ الْإِخْتِ وَأَمْهَاتِكُمُ الَّتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخْوَاتِكُمْ مِنَ الرَّضَاعَةِ وَأَمْهَاتِ نِسَائِكُمْ ...﴾

[سورة النساء: ٢٣]

“Mmeharamishiwa (kuoa) mama zenu, na watoto wenu na dada zenu na shangazi zenu, na ndugu wa mama zenu, na watoto wa ndugu zenu, na watoto wa dada zenu, na mama zenu waliokunyonyesheni

na dada zenu, wa kunyonya, na mama wa wake zenu na watoto wa kambo walio katika ulinzi wenu.” Annisaa : 23.

Na akataja vile vile mambo yalioharamishwa katika njia za kutafuta riziki akasema:

﴿وَأَحَلَ اللَّهُ الْبَيْنَ وَحَرَمَ الرِّبُوا...﴾ [٢٥٧] سورة البقرة: ٢٥٧

“Na hali Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na kuiharamisha riba.”

Al Baqara : 275

Kisha Mwenyezi Mungu aliye mwangi wa rehema kwa waja wake ametuhalalishia mambo mengi mazuri yasiohesabika kwa wingi wake, kwa sababu hii basi ndio maana tunakuta mambo mengi ya halali hakuyafafanua kwa undani na kuyaorodhesha, kwa kuwa ni mengi mno yasioweza kudhibitika kwa urahisi. Lakini hapo hapo tunakuta kuwa mambo ya haramu ameyafafanua kwa undani zaidi na kuyaorodhesha. Hii ni kwa kuwa mambo yenyewe ni machache na yanaweza kudhibitika kwa urahisi na hivyo kuwa

wepesi kwetu kuyajua na kuyafahamu vilivyo hatimae kujiепusha na kujiweka nayo mbali , Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿وَقَدْ فَصَلَ لَكُمْ مَا حَرَمَ عَلَيْكُمْ إِلَّا مَا اضْطَرَرْتُمْ إِلَيْهِ﴾

“Na amekubainishieni wazi wazi alivyokuharamishieni isipokuwa vile mnavyolazimika (kuvitumia kwa ajili ya njaa na mengineyo). Al An aam : 119
Ama vitu vya halali Mwenyezi Mungu ameviharamisha kwa ujumla bila kubainisha wazi wazi maadam kuwa ni vizuri akasema:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ كُلُوا مِمَّا فِي الْأَرْضِ حَلَالًا طَيِّبًا﴾

“Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi halali na vizuri.” Al Baqara : 168.

Na miongoni mwa rehema zake kubwa Mwenyezi Mungu kwa waja wake ni kuwa amejaalia asili kwenye vitu vyote kuwa ni ruhusa kutumiwa mpaka pale itakapokuja dalili ya kuharamisha. Na hizi ni katika karama zake Mwenyezi Mungu na

ukunjufu wake kwa waja wake, kwa hiyo wajibu wetu kutii, kunyenyeka na kushukuru.

Baadhi ya watu wanapoona vitu vyaharamu vikiorodheshwa na kufafanuliwa kwao hudhikika na nafsi zao kukosa raha na uvumilivu, na hii ni kutokana na ule udhaifu wa imani zao na uchache wa ilimu zao kwenye sheria za **Mwenyezi Mungu**.

Kitu cha kushangaza kwa watu hawa, hivi sijui wanataka wahesabiwe aina ya vitu vyahalali alivyovihalalisha **Mwenyezi Mungu** kimoja kimoja ndipo waweze kukinaika na kukubali kuwa dini hii ni nyepesi? au sijui wanataka waorodheshewe aina ya vitu vizuri vilivyohalalishwa na dini hii ndipo watulize nafsi zao na kujua kuwa sheria za dini hii haziwachafulli maisha yao au vipi? Hivi wanataka waambiwe kuwa nyama ya ngamia, ng'ombe, mbuzi, kondoo, sungura, paa, mbuzi mwitu, kuku, njiwa, bata, bata maji, na mbuni waliochinjwa kihalali kutokana na sheria za **Mwenyezi Mungu**

kuwa ni halali kuliwa ndipo waridhike? Na kuwa maiti za nzige na samaki ni halali kuliwa? Na kuwa mboga za majani, matunda na baadhi ya nafaka na matunda yenyе faida ni halali kuliwa na binaadamu? Maji, maziwa, asali, mafuta na siki ni halali?

Na kuwa kutumia mbao, chuma, kokoto, mchanga, plastiki, vioo na mpira ni halali?

Na kuwa wanyama kama farasi, punda, ngamia, nyumbu, au magari, treni, majahazi na ndege ni halali kupandwa na binadamu?

Au wanataka waambiwe kuwa kutumia vipoza hewa (air condition), majokofu, mashine za kusagia nafaka, mashine za kukandia unga, mashine za kuokea mikate, mashine za kukamulia matunda, na vitendea kazi mbali mbali kama vile vya utabibu, uhandisi na mahesabu, utabiri wa hali ya hewa na anga, majengo, mashine za kuchimbia petroli na kuvuta maji, madini ,

Na kuva a nguo za pamba, katani, sufi, manyoya na ngozi zilizoruhusiwa, nylon na polyester pia wanataka waambiwe kuwa ni halali kuvaliwa?!

Na kuwa asili kwenye ndoa, biashara, udhamini na hawala,(Bill of Exchange) uajiri na kazi za ufundi kama vile useremala na uhunzi na utengenezaji wa ala mbalimbali (repairing) na kazi za uchungaji kama vile uchungaji wa kondoo, ng'ombe, mibuzi na ngamia ni halali?

Je huoni kuwa haiwezekani kuorodhesha na kuhesabu mambo yote ya halali aliyotuhalalishia Mwenyezi Mungu? Na kama tutajaribu kufanya hivyo mlolongo wake utakuwa mrefu usiokwisha? Hivi wana nini watu hawa kiasi kwamba hawataki kufahamu ukweli ulio wazi?

Ama kuhusu hoja yao kuwa dini ni nyepesi, huu ni ukweli usiopingika na mtu yoyote, lakini lazima ifahamike kuwa hii ni kauli ya haki yenye kukusudiwa baatili ndani yake, kwa sababu uwepesi unaofahamika kwenye

dini hii si huo wanaokusudia wao, kwa sababu wepesi wake hauendi kulingana na matamanio au matakwa ya watu fulani na rai zao, isipokuwa wepesi wake unakwenda kama vile ulivyokuja kwenye sheria za Mwenyezi Mungu.

Kuna tofauti kubwa sana baina ya kukiuka maharamisho ya Mwenyezi Mungu kwa kigezo cha baatili kuwa dini ni nyepesi ambapo huo ni ukweli usiopingika bila shaka na baina ya kuchukua ruhusa za kisheria kama vile kukusanya sala na kupunguza rakaa na kufungua wakati wa safari, na kupaka kwa maji kwenye khofu mbili kwa msafiri siku tatu usiku na mchana. Na kutayamamu badala ya kutawadha kwa maji kama kutakuwa na madhara pindi utakapotumia maji. Na kukusanya sala mbili kwa pamoja kwa mgonjwa na wakati wa kunyesha mvua, na ruhusa ya kumuangalia mwanamke wa kando kwa yule mwenye kutaka kuoa, na kuchagua kwenye kafara ya kiapo baina ya

kumpa mtumwa uungwana, kulisha au kuvisha. Na kujuzu kula nyamafu kwa mwenye kulazimika kufanya hivyo kutokana na njaa na mengineyo. Haya na mambo mengine yasiokuwa haya ni mionganoni mwa ruhusa na takhfisu za kisheria.

Mbali na hayo yaliyotangulia pia ni wajibu kwa kila muislamu kujua kwamba katika kuharamisha mambo ya haramu kuna hekima kubwa ndani yake, mionganoni mwa hekima hizo ni kuwa:

Mwenyezi Mungu huwatia mtihani waja wake kwenye mambo haya ili apate kuona jinsi gani watakavyofanya na jinsi gani watakavyofuata amri zake, na jinsi gani watakavyojiepusha na makatazo yake. Na mionganoni mwa njia za kupambanua watu wa motoni na watu wa peponi ni kuwa watu wa motoni walizamia na kubobe kwenye matamanio ambayo ndio yaliozungushiwa moto, na watu wa peponi wao walisubiri kwenye mambo yalioharamishwa ambayo

moto, na watu wa peponi wao walisubiri kwenye mambo yalioharamishwa ambayo ndio yaliozungushiwa pepo. Na lau kama si mtihani huu basi asingejulikana mtu mbaya aliye muovu, na mtu mwema aliye mtiifu. Na kwa maana hii basi ndio maana wale watu wenyе imani zilizokuwa barabara huchukulia uzito wa taklifa kwa mtizamo wa subira na uvumilivu na kutarajia malipo kwa Mola wao, hivyo huwa watiifu na wanyenyekevu kwenye amri za Mwenyezi Mungu ili wapate ridhaa zake, kwa hiyo uzito wa taklifa hiso hupungua kwa upande wao.

Ama wale watu wanaafiki wao huzitazama taklifa hiso kwa jicho la uchungu na ghadhabu na kuona kuwa wamenyimwa raha, kwa hiyo mzigo wa taklifa huwa ni mzito kupita kiasi kwa upande wao, Na hatimae kukosekana kabisa utiifu na unyenyekevu kutoka kwao.

Mtu mtiifu, kwa kule kuacha mambo yalioharamishwa huhisi ladha na raha ndani ya nafsi yake.

"من ترك شيئاً لله عوضه الله خيراً منه، ويجد لذة الإيمان في قلبه"

"Mwenye kuacha kitu kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humbadilishia kitu bora zaidi kuliko kile alichokiacha, na hupata ladha ya imani ndani ya moyo wake."

Ndugu yangu msomaji mtukufu! Kwenye kijitabu hiki kidogo utapata kujua mambo mengi tofauti yaliyoharamishwa kwenye dini pamoja na kukuwekea wazi dalili za kuhamramishwa kwake kutoka kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna

Sahihi za Mtume wake [﴿]¹. Na mambo haya

¹ Baadhi ya wanazuoni watukufu wameshatunga vitabu vyenye kuonyesha mambo yalioharamishwa au kuonyesha baadhi ya aina ya mamba yalioharamishwa, kama vile madhambi Makubwa AL KABAIR. Na mionganini mwa vitabu vizuri vyenye kuzungumzia mas

waislamu, nami nimeona niyataje ndani ya kijitabu hiki kwa lengo la kuyaweka wazi na kutoa nasaha, na nina muomba Mwenyezi Mungu anipe uongofu na taufiki na kusimama kwenye mipaka yake mimi pamoja na ndugu zangu wote wa kiislamu.

Na atuepushe sote na mambo ya haramu na kutulinda na uovu, na Mwenyezi Mungu ni mbora wa kuhifadhi na mwingi wa rehema.¹

¹ Kitabu hiki kimerejewa na kupitiwa na maulama watukufu mbali mbali Mwenyezi Mungu awape kheri, mionganini mwao akiwa Mtukufu Sheikh Abdul Aziz Bin Abdallah bin Baaz, Mufti mkuu wa Saudi A.

1. KUMSHIRIKISHA MWENYEZI MUNGU

Ni haramu kubwa kabisa kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu chochote, kwa ushahidi wa hadithi ya Abu Bakrah kuwa Mtume ﷺ amesema:

”أَلَا أَنْبَئُكُمْ بِأَكْبَرِ الْكَبَائرِ (ثَلَاثَةِ) قَالُوا: قُلْنَا بَلَىٰ يَا رَسُولَ اللَّهِ، قَالَ: إِلَشْرَاكُ بِاللَّهِ“

“Je nikwambieni madhambi makubwa kupita yote?” (akarejelea mara tatu kauli hii) wakasema maswahaba, tukasema tuelezee Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akasema Mtume ﷺ “Kumshirikisha Mwenyezi Mungu.” Bukhari No. 2511. Madhambi yote huenda Mwenyezi Mungu akayasamehe isipokuwa shiriki, mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu hana budi kuleta toba haraka sana kabla hajafa.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرِكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يُشَاءُ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kushirikishwa na husamehe yasiokuwa haya kwa amtakae, na anaemshirikisha Mwenyezi Mungu bila shaka amebuni dhambi kubwa.” An-nisaa : 48

Kuna shiriki za aina tofauti, nyingine huwa ni kubwa ambazo humtoa mfanyaji wake kwenye dini ya kiislamu na kuingizwa motoni na kubaki humo milele ikiwa atakufa kwenye hali ya shiriki hiyo bila kurejea kwa Mola wake na kutubu. Na miongoni mwa shiriki zilizoenea kwenye miji tofauti ya waislamu ni kama vile:-

KUABUDU MAKABURI;

Nayo ni kuamini kuwa mawalii na watu waliokufa zamani wana uwezo wa kuondosha matatizo na kutuliza au kupunguza huzuni pindi unapowataka au kuwaomba msaada pale unapopatwa na matatizo. Na Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ﴾ ...

“Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila yeye tu.” Israa : 23
 Vile vile kuomba shufaa au kutaka kuondoshewa matatizo kutoka kwa watu waliokufa zamani sawa watu hao iwe ni manabii walio wema au watu wengine wasiokuwa wao. Na Mwenyezi Mungu anasema:

Je yuko Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? An-Naml : 62

Baadhi ya watu hufanya kutaja jina la Sheikh wake au walii fulani kuwa ndio ada na ibada yake pindi anapotaka kukaa, kusimama au anapojikwaa, na kila inapotokea kufikwa na maafa, matatizo, misiba au huzuni utaona huyu akisema ‘Ewe Muhammad, na huyu akisema, Ewe Aliy, na huyu akisema Ewe Hussein, na huyu akisema Ewe Badawiy, na huyu akisema Ewe Jailaaniy na huyu akisema Ewe Shaadhily na huyu akisema Ewe Rifaa na mwingine akimuomba Idarous, na huyu akimuomba Saidat Zainab na huyu akimuomba bin Ulwani n.k. Na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anasema:

﴿إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ عِبَادٌ أُمَّالُكُمْ﴾

Hakika wale mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni waja (watumwa) kama nyinyi.” Al Aaraf : 194

Baadhi ya wale wenye kuabudu makaburi hufanya tawafu kwenye makaburi hayo na

kugusa nguzo zake na kujipangusa nazo mwilini, na kubusu vizingiti vyake na kuchukua udongo wa makaburi na kujipaka nao usoni, na wengine huanguka kuyasujudia pindi wanapoyaona na kusimama mbele yake kwa heshima na utulivu, hali ya kuwa niwenye kunyenyekea na kudhalilika na kuomba dua mbalimbali kama vile kuomba kuondoshewa maradhi au kupata watoto au kurahisishiwa matatizo. Na wakati mwengine huita mwenye kuabudu makaburi kwa kusema Ewe sayidi yangu mimi nimekuja kutoka nchi ya mbali, basi usinirejeshe mikono mitupu kwenye dua yangu.

Na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَمَنْ أَفْلَى مَنْ يَدْعُو مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُ
إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنْ دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ﴾

“Na wapotofu (wapotevu) wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ambao hawatawajibu

mpaka siku ya kiama na hawatambui dua zao?" Al Ahqaaf : 5.

Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasema:

"من مات وهو يدعون دون الله ندا دخل النار"

Mwenye kufa hali ya kuwa anaomba kwa yule asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi ataaingia motoni." Bukhariy Fat-hul Baary.

8/176.

Baadhi ya hawa wenye kuabudu makaburi utawaona wakinyoa vichwa vyao mbele ya haya makaburi, na wengine utawaona wakiwa na vitabu vyenye anuani kama - manaa sikal-hajjil mashaahid (yaani utaratibu wa kuzuru mashaahidi). Mashaahid yanayokusudiwa hapa ni makaburi na maziara ya mawalii.

Na baadhi ya watu hawa wanaamini kuwa mawalii wanamamlaka na uwezo wa kumdhuru mtu au kumnufaisha kwa lolote, na hali Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَإِنْ يَمْسِكَ اللَّهُ بِضَرٍ فَلَا كَاشِفٌ لَهُ إِلَّا هُوَ وَإِنْ يَرْدِكْ
بِخَيْرٍ فَلَا رَأْدٌ لِفَضْلِهِ يُصِيبُ بِهِ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَهُوَ
الْغَفُورُ الرَّحِيمُ﴾

“Na kama Mwenyezi Mungu akikugusisha dhara basi hakuna yoyote awezae kuiondoa isipokuwa yeye (mwenyewe) na kama akikutakia kheri basi hakuna awezae kurudisha fadhila zake (Mwenyezi Mungu) Huzifikisha (fadhila hizo) kwa amtakae katika waja wake (maadamu anajinyenyeka kwake) nae ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. (Yunus : 107).

Na ni katika shiriki vilevile kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu kama wanavyofanya wale wenye kuweka nadhiri kuwa wataweka mishumaa na taa kwa watu wa makaburi. Na mionganini mwa sura za shiriki kubwa ni kuchinja kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anasema:

﴿فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحِر﴾

“Basi sali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako) na kila utakalolifanya basi lifanye kwa ajili ya Mola wako sio mizimu wala mapango wala makaburi.” Al Kauthar : 2

Na maana ya wanhar ni kuwa chinja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa jina la Mwenyezi Mungu. Anasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

”لَعْنَ اللَّهِ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللَّهِ“

“Amelaaniwa na Mwenyezi Mungu yule mwenye kuchinja kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu.” Muslim No. 1978.

Kwenye kuchinja kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu kunapatikana haramu za aina mbili kwa kile kinachochinjwa, kwanza kabisa ni kule kuchinjwa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na pili ni kule kuchinjwa kwa jina lisilokuwa la Mwenyezi Mungu, na mambo haya mawili kwa pamoja hukifanya kile kinachochinjwa kuwa ni haramu kabisa kuliwa na Muislamu.

Na mionganini mwa uchinjaji wa kijahilia (kipagani) ulioenea sana kwenye zama zetu hizi za leo ni kuwachinjia majini. Na kitendo hiki mara nyingi hufanywa na baadhi ya watu pale wanapokuwa wamechimba kisima, kwa hiyo huchinja mnyama mbele yake au juu ya kizingiti cha nyumba kwa kuchelea au kuhofia kuwa wasije wakaudhiwa na majini. (Rejea Taysiril Aziizil-hamiid uk:158).

Na mionganini mwa shiriki zilizoenea wakati huu ni kuharamisha mambo aliyooyahalalisha Mwenyezi Mungu au kuwa na imani kuwa kuna mtu yoyote kinyume na Mwenyezi Mungu mwenye haki na uwezo wa kuhalalisha jambo au kuharamisha, au kujihukumu kwenye mahakama zenye kutumia kanuni za kijahilia, hali ya kuwa uko radhi na kanuni hizi na tena kwa uchaguzi wa nafsi yako, Na pia ukawa ni mwenye kuzihalalisha kanuni hizi za kijahilia na kuitakidi kuwa zinatafaa kutumika badala ya sheria alizoteremsha

Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu amekitaja kitendo hiki kuwa ni kufuru kubwa kabisa kwenye kauli yake isemayo:-
 ﴿اتخذوا أَحْبَارَهُمْ وَرَهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أَمْرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سَبَّحَانَهُ عَمَّا يَشْرَكُونَ﴾

“Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Na wamemfanya Masihi mwana wa Mariamu (pia Mungu) hali hawakuamrishwa isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anaestahiki kuabudiwa ila Yeye, Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo.” Taubat : 31.

Adiy bin Haatim alipomsikia Mtume akisoma aya hii akasema; “Nikasema, “kwa hakika wao hawakuwa wakiwaabudu (hao wanavyuoni wao na watawa) akasema ‘Ndio lakini wanawahalalishia mambo aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu na wao wakayafanya kuwa ni halali na kuwaharamisha mambo aliyoyahalalisha

Mwenyezi Mungu na wao wakayafanya ni haramu na huko ndiko kuwaabudu kwenyewe!' Al Bayhakiy 10/116 ; Tirmidhiy no. 3095. Ghaayatul maraami-Al Baaniy: uk 19.

Na Mwenyezi Mungu amewaeleza washirikina kuwa wao:

﴿ ولا يحرمون ما حرم الله ورسوله ولا يدينون دين الحق﴾ ...
 “Wala hawaharamishi alivyoviharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wala hawashiki dini ya haki.” Taubat:29

Na akasema tena Mwenyezi Mungu:

﴿ قل أرأيتم ما أنزل الله لكم من رزق فجعلتم منه حراما
 وحللا قل والله أذن لكم أم على الله تفترون﴾

“Sema, Je! Mnaonaje zile riziki alizokuteremshieni Mwenyezi Mungu kisha mkafanya katika hizo (nyingine kuwa za) haramu na (nyingine kuwa za) halali, sema Je! Mwenyezi Mungu amekuruhusuni (kufanya hivyo au mnamzulia Mwenyezi Mungu uongo tu?” Yunus : 59

UCHAWI NA UTABIRI NA UPIGAJI RAMLI.

Ama uchawi ni kufuru, na ni moja katika yale madhambi saba makubwa yenyeye kuangamiza. Na uchawi huleta madhara na wala hauna faida yoyote kwa mtu. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu kujifundisha uchawi:

﴿وَيَتَعْلَمُونَ مَا يَضْرِهِمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ﴾

“Na wanajifunza ambayo yatawadhuru na wala hayatawafaa.” AlBaqara:102. Na akasema Mwenyezi Mungu:

﴿وَلَا يَفْلُحُ السَّاحِرُ حِيثُ أَتَى﴾

“Wala mchawi hafaulu (hafuzu) popote afikapo.” Taha : 69

Na mwenye kuchukua uchawi ni kafiri bila shaka. Amesema Mwenyezi Mungu:

﴿وَاتَّبَعُوا مَا تَنَاهَى الشَّيَاطِينُ عَنْ مِلَكِ سَلِيمَانَ وَمَا كَفَرَ سَلِيمَانَ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يَعْلَمُونَ النَّاسُ السُّحُورُ وَمَا أَنْزَلَ عَلَى الْمُلَكِينَ بِبَابِلِ هَارُوتَ وَمَارُوتَ وَمَا يَعْلَمَنَّ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولُوا إِنَّمَا نَحْنُ فَتَّةٌ فَلَا تَكْفُرُ﴾ ...

“Na Suleimani hakukufuru bali mashetani
ndio waliokufuru wakiwafundisha watu
uchawi (waliokuwa wakiujua wenyewe
zamani) na (uchawi) ulioteremshwa kwa
malaika wawili Haaruti na Maaruta katika
(mji) wa Babil wala (Malaika hao)
hawakumfundisha yoyote mpaka
wamwambie; ‘Hakika sisi ni mtihani
(wa kutazama kutii kwenu) basi usikufuru.’
Al Baqara : 102.

Na hukumu ya mchawi katika uislamu ni
kuuliwa na pato lake huwa ni haramu.
Baadhi ya wajinga na madhaalimu na
wadhaifu wa imani huwaendea wachawi
kwa ajili ya kutaka kufanyiwa uchawi ili
wapate kuwafanya uadui watu wengine au
kulipiza kisasi. Na baadhi ya watu wengine
huingia kwenye makosa kwa kule
kukimbilia kwa wachawi ili wakaaguliwe au
kuondoshwa uchawi baada ya kurogwa, na
wakati ilikuwa ni wajibu wao kukimbilia
kwa Mwenyezi Mungu na kujitibu kwa
maneno yake kama vile kusoma

muawadhaatani (Qul audhu birabbil Falaq, na Qul audhu birabbinaas) na nyinginezo.

Ama mtabiri na mpiga bao hao wote ni wenyewe kumkufuru **Mwenyezi Mungu Mtukufu** ikiwa watadai kujua elimu ya ghaibu, kwa sababu hakuna mtu yoyote anaejua mambo ya ghaibu isipokuwa **Mwenyezi Mungu Mtukufu** peke yake.

Wengi wa watabiri na wapiga bao huwapumbaza wajinga ili kuwalia mali zao kwa dhuluma, na hutumia njia nyingi tofauti tofauti kama vile kuchora mistari kwenye mchanga au kupiga simbi au kusoma viganja vya mkono au kutumia kikombe au mpira wa kioo, n.k. Na watabiri hawa kama watafanikiwa mara moja kusema kweli basi mara tisini na tisa watakuwa ni waongo. Lakini wale watu wajinga hawakumbuki isipokuwa ile mara moja waliosema kweli wazushi hawa!

Utawaona wajinga wakiwaendea watabiri na wapiga bao eti wanataka kujua mambo yatakayokuja au kutaka kujua kama

ndoa yake au biashara yake anayokusudia kuifanya ina kheri na furaha ndani yake au ina shari na nuksi, au kutafuta vitu vilivyopotea n.k.

Na mwenye kuwaendea watu hawa na kuyaamini kwa dhati yale wanayosema hukumu yake mtu kama huyu huwa ni kafiri, na mwenye kutoka kwenye uislamu, na dalili ya maneno haya ni kauli ya Mtume:

”من أتى كا هنا أو عر افا فصدقه بما يقول فقد كفر بما
أنزل على محمد ﷺ“

”Mwenye kumuendea kuhani au mpiga ramli (bao) kisha akayaamini yale anayoyasema huwa ameyakufuru aliyoteremshiwa Muhammad.” Ahmad : 2/329.

Ama ikiwa yule mwenye kuwaendea wapiga bao na watabiri bila kuamini kuwa wanajua mambo ya ghaibu lakini lengo lake ni kuwa anakwenda kuwapima na kuwajaribu na mfano wa haya; Mtu huyu hapewi hukumu ya ukafiri na kutoka

kwenye uislamu, isipokuwa sala yake huwa haikubaliwi na Mwenyezi Mungu kwa muda wa siku arobaini, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume:

”من أتى عرافا فسأله عن شيء لم تقبل له صلاة أربعين ليلة“

“Mwenye kumuendea mpiga bao akamuuliza kitu hatokubaliwa sala yake kwa muda wa siku arobaini.” Muslim 4/1751. Hii ni pamoja na kuwa sala itabakia kuwa ni wajibu kwake pamoja na kuleta toba kwa Mola wake.

**KUAMINI KUWA NYOTA ZINA
MAMLAKA KWENYE MATUKIO NA
MAISHA YA WATU.**

Imepokewa kutoka kwa Zaid bin Khaalid Al-Juhaniy akisema;

عن زيد بن خالد الجهنمي قال: "صلى لنا رسول الله صلاة الصبح بالحدبية - على أثر سماء كانت من الليلة - فلما انصرف أقبل على الناس فقال: ((هل تدرؤن ماذا قال ربكم؟)) قالوا: الله ورسوله أعلم، قال: ((أصبح من عبادي مؤمن بي وكافر، فاما من قال مطرنا بفضل الله ورحمته فذلك مؤمن بي وكافر بالكوكب، وأما من قال بنوء كذا وكذا فذلك كافر بي ومؤمن بالكوكب"))

‘Alitusalisha Mtume sala ya asubuhi tukiwa Al- hudaibiya mara tu baada ya mvua iliyonyesha usiku, alipomaliza (kusali) aliwaelekea watu (maswahaba) na kusema: “Je mnajua Mola wenu amesemaje? wakajibu maswahaba ‘Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wenyewe kujuza zaidi,’ akasema Mtume, “Wamepambazukiwa waja wangu (hali ya kuwa) mionganoni mwao

wakiwa ni wenyе kuniamini na wengine wakiwa ni wenyе kunikufuru. Ama yule mwenye kusema ‘Tumeletewa mvua kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema zake basi huyo ndio mwenye kuniamini mimi, ama yule mwenye kusema tumeletewa mvua kwa sababu kadhaa wa kadhaa huyo ndie yule mwenye kunikufuru mimi na ndie (huyo) mwenye kuamini nyota.’ Muslim : 4/1751.

Na mionganі mwa kufuru hiyo pia kukimbilia nyota za bahati kwenye magazeti; ikiwa mtu ataitakidi na kuamini kuwa mambo yalioandikwa kwenye magazeti hayo ni kweli yanatokana na mamlaka na athari za nyota na falaki, mtu huyo mwenye imani kama hii bila shaka atakuwa ni mshirikina. Na kama atasoma kwa ajili ya kupoteza muda tu na kujiliwaza huyo atakuwa ni muasi na mwenye dhambi, kwa sababu haifai kujiliwaza kwa kusoma mambo ya shiriki, na hasa ukiongezea kuwa shetani anaweza akamuingiza mtu huyo

kwenye itikadi hii ya kuamini nyota, na hivyo kuwa ni njia mionganini mwa njia za shiriki.

Na katika shiriki vile vile kuamini kuwa baadhi ya vitu vina manufaa na hali Mwenyezi Mungu hakuyaumba manufaa hayo kwenye vitu hivyo:-

Kama vile wanavyoamini baadhi ya watu kwenye azima na hirizi za kishiriki, au kwembe, simbi na vikuku vya madini na mambo mengineyo, kwa ushauri kutoka kwa waganga, au wachawi au kutokana na imani za kale za kurithi kutoka kwa mababu na hatimae kucaa hirizi au vikuku hivi shingoni au viunoni au kuwavisha watoto wao wadogo kwa lengo la kuzuia kudhurika na vijicho vya mahasidi, au kufunga hirizi na vikuku hivyo kwenye miili yao au kuning'iniza kwenye magari yao au majumbani mwao. Au kucaa pete yenyeye aina fulani ya kito wakiamini kuwa ndani yake kuna nguvu fulani fulani zenyeye kuondosha balaa au kuzuia.

Na imani hii bila shaka inakwenda kinyume na imani ya kumtegemea Mwenyezi Mungu peke yake, na wala haimzidishii binaadamu isipokuwa udhaifu na udhalilifu, kwa sababu huku ni kujitibu kwa njia ya haramu. Na hirizi nyingi kati ya hizi zinazovaliwa ndani yake huwa kunashiriki ya wazi, na kuwataka msaada baadhi ya majini na mashetani, au michoro migumu au maandishi yasiofahamika. Baadhi ya waganga wenye kufanya kiini macho huandika aya za Qur'ani na kuchanganya na mambo mengine ya shiriki, na baadhi yao hufikia hata kuziandika aya za Qurani kwa kutumia vitu vya najisi au kutumia damu ya hedhi, Subhaanallah!

Kwa hiyo basi kufunga na kucaa vitu hivyo vilivyotajwa hapo juu ni haramu kabisa, kwa ushahidi wa maneno ya Mtume

"من علق تميمة فقد أشرك" "Mwenye kuваа hirizi (tamaimu) basi atakuwa amemshirikisha Mwenyezi Mungu." Ahmad 4/156.

Na mwenye kuyafanya haya, ikiwa ataaミニ kuwa mambo haya yananufaisha au kudhuru kinyume cha Mwenyezi Mungu basi atakuwa amemshirikisha Mwenyezi Mungu tena shiriki kubwa. Na atakaeitakidi na kuamini kuwa hizi hirizi ni sababu tu ya kunufaisha au kudhuru na Mwenyezi Mungu wala hakuzijaalia uwezo huo. Mtu huyo atakuwa amefanya shiriki ndogo, na kitendo hiki kinaingia kwenye shiriki ya sababu.

KUFANYA IBADA KWA KUJIONYESHA (RIA)

Miongoni mwa masharti ya amali njema ni kuwa lazima ziwe zimetakasika na ria, halafu ziwe zimeshikamana na sunna sahihi. Na yule mwenye kufanya ibada kwa lengo la kujionyesha kwa watu huwa ni mshirikina wa shiriki ndogo na amali zake hupotea bure bila faida yoyote kama vile mwenye kusali kwa ajili ya kujionyesha kwa watu. Amesema Mwenyezi Mungu:

﴿إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يَخْادِعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَادِعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كَسَالَىٰ يَرَأُونَ النَّاسَ وَلَا يَذَكَّرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا﴾

“Hakika wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu, nae atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao (huko) na wanaposimama kusali husimama kwa uvivu, wanaonyesha watu (kuwa wanasali) wala hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo”. An-Nisaa : 142.

Na vile vile pindi anapofanya amali yoyote basi hutaka watu wajue na kusikia kuwa kafanya amali fulani ya kheri¹ ; basi huyu nae vile vile huingia kwenye shiriki. Na imepokewa onyo kali kwa mwenye kufanya hivi kama ilivyokuja kwenye hadithi ya Ibn Abbas Mwenyezi Mungu awe radhi nae pamoja na baba yake kutoka kwenye hadithi marfuu;

"من سمع سمع الله به ومن راعى راعى الله به"

'Mwenye kufanya amali yoyote kwa ajili ya kutaka kusikikana kwa watu,

¹ Yaani kama vile wanavyofanya baadhi ya matajiri wanapokuwa wanasaidia kitu fulani , hutaka watangazwe redioni, magazetini na kwenye matelevisheni, kuwa fulani labda katoa mablanketi kadhaa kusaidia watoto yatima, au hospitali au kadhaa na kadhaa. Na wengine wanapoombwa msaada fulani husema yuko tayari kufanya hivyo kwa sharti wawepo waandishi wa habari wanukuu habari hizi kwenye vyombo vyaa habari n.k. Na wajue watu hawa kuwa Mtume (S.A.W) amekikemea vikali kitendo hiki.

Mwenyezi Mungu humfanya akasikikana, na mwenye kufanya kwa ajili ya kutaka kujionyesha kwa watu, Mwenyezi Mungu humfanya akaonekana.” Muslim : 4/2289.

Na mwenye kufanya ibada akimkusudia ndani yake Mwenyezi Mungu na watu, basi amali yake hiyo hurudi patupu bila kupata thawabu yoyote kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kama ilivyokuja kwenye hadithi kudsiy Mwenyezi Mungu anasema:

”أَنَا أَغْنَى الشَّرْكَاءِ عَنِ الشَّرْكِ، مَنْ عَمِلَ عَمَلاً أَشْرَكَ فِيهِ مَعِي غَيْرِي تَرَكَهُ وَشَرَكَهُ“

“Mimi ni mwenye kujitosheleza zaidi na washirikina kutokana na shiriki yao, mwenye kufanya amali yoyote akanishirikisha ndani yake mimi pamoja na mtu mwingine basi mtu huyo nitamuacha na shiriki yake.” Muslim no. 2985.

Na mwenye kufanya amali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kisha ikaja kuzukiwa katikati yake na ria, kama ataichukia ria hiyo na kuitakasa upya amali yake basi amali hiyo husihi, lakini kama ataridhika

nayo na nafsi yake kutulia, hapa
wanachuoni wengi wanasema kuwa amali
yake itakuwa batili.

TIYARA(NUKSI) (Evil Omen) ¹

Maana yake ni tabia ya kutazamia misiba na matatizo (Pessimism) na Mwenyezi mungu anasema:

﴿فِإِذَا جَاءَنَّهُمُ الْحَسَنَةَ قَالُوا لَنَا هَذِهِ وَإِنْ تُصِيبُهُمْ سَيِّئَةٌ يَطْيِرُوا بِمُؤْسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ﴾....

“Unapowafikia wema husema ‘Huu ni kwa ajili yetu’ na ukiwafikia ubaya humnasibishia ukorefi huo mussa na walio pamoja nae.” Al Aaraaf : 131.

Zamani walikuwa waarabu kwenye zama za jahilia anapotaka mmoja wao kusafiri au

¹ Aina ya ubashiri, au kubashiri mambo yatakayokuja kutokea baadae kwa njia ya viumbe vya asili(Evil Omen), ndege mbaya, nuksi au kisirani, kama vile wanavyoamini baadhi ya watu kwamba bundi ni ndege mbaya mwenye nuksi, anapolia karibu na nyumba ni dalili ya kutokea maafa na misiba kwenye nyumba hiyo, au kama vile wanavyoamini baadhi ya watu kuwa kuna mlio fulani wa paka anapolia usiku inakuwa ni uchuro. Nk.

kufanya jambo humshika ndege na kumrusha angani, kama ndege yule ataruka kuelekea upande wa kulia hapo huamini kuwa safari yake au jambo lake alilokusudia kulifanya lina kheri ndani yake, la kama ataruka kuelekea upande wa kushoto hapo huona kuwa jambo lake au safari yake aliyokusudia kuifanya ina nuksi ndani yake au itakuwa na matatizo hivyo hurejea na kujiepusha nayo.

Na Mtume amebainisha hukumu ya kitendo hiki kwa kusema: "الطيرة شرك"

'Kurusha ndege ni shiriki.' Ahmad 1/389.

Na mionganini mwa mambo yanayoingia kwenye imani hii ya haramu yenyewe kwenda kinyume na tauhidi ni kuamini kwamba baadhi ya miezi ina nuksi kama vile kuacha kuoa kwenye mwezi wa mfungo tano, na kwenye masiku kama vile kuamini kuwa jumatano ya mwisho wa kila mwezi ni siku ya nuksi ya kudumu. Au namba kama vile 13 au majina au watu wenye vilema; kama vile mtu anapotaka kwenda kufungua duka

lake ikatokea kwa bahati mbaya akakutana na kilema njiani huamua kurejea nyumbani kwa kuamini kuwa kukutana na kilema ni nuksi na mambo mengineyo mengi yenyε kufanana na haya.

Mambo haya yote tulyoyataja hapa na mengineyo mfano wa haya ni haramu na ni katika shiriki, hivyo ni wajibu kwa kila muislamu kujiepusha nayo.

Na Mtume amewaepusha na kuwatakasa hawa wote au vitu hivyo na nuksi hizi za uzushi kwa kusema;

"ليس من تطير ولا ظير له ولا تكهن ولا تكهن له
(وأظنه قال:) أو سحر أو سحر له".

"Si katika sisi (Waislamu) yejote atakaevifanya(bashiri) vitu kuwa na nuksi, (kisirani) au atakaetaka kufanyiwa (kubashiriwa) au mwenye kutabiri au kutaka kutabiriwa (na ninadhani alisema vilevile) mwenye kufanya uchawi au kutaka kufanyiwa. Attabrianiy : 18/162.

Na mwenye kuingia kwenye kitu chochote katika hivi tulivyovitaja basi kafara yake ni

kama ile iliyopokewa kutoka kwenye hadithi ya Abdallah bin Amru Mwenyezi Mungu awe radhi nae kuwa amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake kuwa;

"من ردته الطيرة من حاجة فقد أشرك؟ قال يا رسول الله: ما كفارة ذلك؟ قال أن يقول أحدهم":

Yeyote atakaerejeshwakwenye haja yake kutokana na kuamini tiara(nuksi, kisirani) basi atakuwa amemshirikisha Mwenyezi Mungu, akasema ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni nini kafara ya kitendo hicho? Akasema na aseme mmoja wao:

"اللهم لا خير إلا خيرك ولا طير إلا طيرك ولا إله غيرك"

"Ewe Mwenyezi Mungu hakuna kheri isipokuwa ile itokayo kwako, na hakuna shari isipokuwa ile ulioikadiria kuwa ni shari, na hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe." Ahmad 2/220.

Kutazamia misiba au nuksi ni tabia ya kila nafsi, hupungua na kuongezeka, na jinsi ya kuitibu tabia hii ni kutegemea kwa

Mwenyezi Mungu kama ilivyokuja kwenye kauli ya Ibin Masoud,

‘Hakuna yoyote kati yetu isipokuwa huingia kwenye nafsi yake kitu kama hicho, na lakini Mwenyezi Mungu hukiondoa kwa kutegemea kwake.’ Abou Daud no. 3910.

KUAPA KWA ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU.

Mwenyezi Mungu huapa kwa anaetaka katika viumbe vyake. Ama viumbe haiwapasi wao kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kuapa ni aina moja wapo ya taadhima, hakuna anaestahiki taadhima hii isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake. Imepokewa kutoka kwa Ibin Omar kwenye hadithi marfuu akisema;

”أَلَا إِنَّ اللَّهَ يَنْهَاكُمْ أَنْ تَحْلِفُوا بِآبَانَكُمْ، مَنْ كَانَ حَالَفَ فَلْيَحْلِفْ بِاللَّهِ أَوْ لِيَصُمْتَ“

‘Eleweni! Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kuapa kwa mababu zenu,

**mwenye kuapa basi na aape kwa (jina la)
Mwenyezi Mungu au anyamaze. Bukhariy
Fat-hul-Baariy : 11/530.**

**Na imepokewa tena kutoka kwa Ibin Omar
kwenye hadithi marfuu kuwa;**

" من حلف بغير الله فقد أشرك "

**'Mwenye kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi
Mungu huwa amemshirikisha.' Imam
Ahmad : 2/125.**

Amesema Mtume;

" من حلف بالأمانة فليس منا "

**'mwenye kuapa kwa amana si katika
sisi.' Abou Daud 3253.**

**Haifai kuapa kwa Al Kaaba,wala kwa
amaana, wala kwa utukufu wala kwa
msaada, wala kwa baraka za fulani wala
kwa maisha ya fulani wala kwa jaha ya
mtume wala kwa jaha ya walii fulani, wala
kwa baba na mama wala kwa kichwa cha
mtoto, viapo hivi vyote ni haramu na
mwenye kuapa kwa kiapo chochote katika
hivi tulivyo vitaja kafara yake ni kusema**

الله لا إله إلا -Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah. Kama ilivyopokewa kwenye hadithi sahihi kwamba

"من حلف فقال في حلفه باللات و العزى فليقل لا إله إلا
الله"

Mwenye kuapa akasema kwaenye kiapo chake 'Naapa kwa Lata na Uzza basi na aseme لا إله إلا الله Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu. (Bukhariy 11/536).

Na mfano wa mlango huu vile vile yanaingia baadhi ya matamko ya kishirikina yenyeye kuharamishwa ambapo baadhi ya waislamu huyatamka mara kwa mara, kama vile kusema; 'Najilinda kwa Mwenyezi Mungu na kwako, mimi ninategemea kwa Mwenyezi Mungu na kwako, mimi sitegemei chochote isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu na kwako.'

Mwenyezi Mungu ni mtegemezi wangu mbinguni na wewe ni mtegemezi wangu ardhini lau kama si Mwenyezi

Mungu na fulani¹, mimi nimejivua (niko mbali) na uislamu. Vile vile kutumia ibara ambazo ndani yake kuna kuzitukana zama kama vile kusema zama hizi ni mbaya,

saa hizi ni za nuksi, na zama hizi ni hadaifu, na mfano wa hayo, sababu kutukana zama matusi yake yanarejea kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye ndie aliyeziumba zama. Na vile vile kujiita kwa majina yenyе kuabudiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu kama vile kujiita Abdul masiihi (mja wa masihi), na Abdul Nnabiy (mja wa Nabii), Abdul Rasuul (mja wa Mtume), Abdul Hussaini (mja wa Hussaini).

Na katika ibara za kileo zinazokwenda kinyume na tauhidi ambazo hutumika kwa wingi, ni kama vile kusema usoshalisti wa kiislamu, Demokrasia ya

¹ Usahihi ni kusema lau kama si Mwenyezi Mungu kisha fulani,

kiislamu, matakwa ya wananchi ndio matakwa ya Mwenyezi Mungu, Dini ni ya Mwenyezi Mungu na nchi ni ya wote, kwa jina la Uarabu, kwa jina la mapinduzi!

Na ni katika haramu vile vile kutumia matamshi kama mfalme wa wafalme, kadhi wa makadhi, kwa kiumbe, au kutumia tamko la sayid (bwana) kwa mtu mnaafiki, au kafiri, iwe kwa lugha ya kiarabu au lugha nyingine yoyote ile.

Kutumia herufi ya 'lau' ambayo hujulisha ghadhabu, majuto na masikitiko na ambayo hufungua amali ya shetani, au kusema Ewe Mola nisamehe kama 'unataka.' Kwa maelezo zaidi, soma kamusi ya matamko yaliokatazwa - ya Sheikh Bakri Abou Zaid.

**KUKAA NA WANAAFIKI AU WATU
WAOVU NA KUWAFANYA NDIO
MARAFIKI WA KUSHIRIKIANA NAO.**

Watu wengi hasa wale ambao imani zao hazijathibiti sawa sawa kwenye nyoyo zao hupenda kukaa na watu waovu na mafasiki, sio hilo tu bali hata wakati mwingine hukaa na wale watu wenyewe kuitukana dini na sheria za Mwenyezi Mungu na kuicheza shere dini yake na vipenzi vyake. Bila shaka kitendo hiki ni kitendo cha haramu na ni kuutukana uislamu. Mwenyezi Mungu anasema: ﴿وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي آيَاتِنَا فَأَغْرِضْ عَنْهُمْ حَتَّىٰ يَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ وَإِمَّا يُتَّسِّيَّنَكُ الشَّيْطَانُ فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ الذِّكْرِ مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ﴾

“Na (wewe muislamu kama kweli muislamu si munafiki) unapowaona wale wanaozungumza (kuzikadhibisha) aya zetu, basi jitenge nao (wende zako) mpaka wazungumze maneno mengine.

Na kama shetani akikusahaulisha (ukakaa nao, na hali wamo katika mazungumzo haya) basi baada ya kutanabahi usikae pamoja nao(hawa) watu madhalimu.” Al An-Aam : 68.

Haifai kabisa kukaa pamoja nao watu hawa wala kuingiliana nao wanapokuwa katika hali hii, hata kama watakuwa ni jamaa zako wa karibu kupita kiasi, au hata kama wataonyesha kukufanyia upole na kuwa tamu ndimi zao kwako, isipokuwa unaweza kuingiliana nao ikiwa tu unataka kuwalingania au kuzijibu batili zao au kupinga mambo yao, ama kuridhika na mambo yao na kuyanyamazia hii haifai kabisa. **Mwenyezi Mungu anasema:**

﴿فَإِنْ تَرْضَوْا عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَى عَنِ الْقَوْمِ﴾
الْفَاسِقِينَ

“Basi mkiwa radhi nao nyinyi (ndio nini maadamu Mwenyezi Mungu hakuwapa radhi?) basi Mwenyezi Mungu hawi radhi na watu wavunjao amri.” At-Tawba : 96

KUACHA UTULIVU KWENYE SALA.

Uovu mkubwa wa wizi ni kuiba sala. Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

”أَسْوَا النَّاسَ سَرْقَةً الَّذِي يَسْرُقُ مِنْ صَلَاتِهِ قَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ وَكَيْفَ يَسْرُقُ مِنْ صَلَاتِهِ قَالَ: لَا يَتَمَرَّدُ عَلَيْهَا وَلَا سُجُودُهَا“

“Muovu mkubwa wa watu kwa wizi ni yule mwenye kuiba kwenye sala yake, wakasema (maswahaba); ‘Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu vipi mtu ataiba kwenye sala yake? Akasema Mtume:

“Haikamilishi rukuu yake wala sijida yake.” Imamu Ahmad 5/310.

Hakika kuacha utulivu na kutokutulia mgongo kwenye rukuu na kusujudu na kutousimamisha sawa sawa baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu, na kutoutuliza sawa sawa kwenye kikao baina sijida mbili, hayo yote ni mashuhuri na mambo yenyewe kuonekana mara kwa mara kutoka kwa watu wengi wenye kusali, kiasi

kwamba inakaribia kutopatikana msikiti wowote ila ndani yake huwa kuna watu kama hawa wasiotulia kwenye sala zao. Elewa kuwa kupatikana utulivu kwenye sala ni nguzo mojawapo miongoni mwa nguzo za sala, na sala haikamiliki na kusihi bila kupatikana utulivu, na jambo hili ni la hatari mno! Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

" لا تجزئ صلاة الرجل حتى يقيم ظهره في الركوع
والسجود "

"Haijuzu sala ya mtu mpaka aunyooshe mgongo wake (sawa sawa) kwenye rukuu na sujudi." Abou Daud 1/533.

Bila shaka huu ni uovu na mwenye kufanya kitendo hiki anastahili kukemewa na kuonywa.

Imepokewa kutoka kwa Abi Abdullah Al-Ash-aariy akisema;

" صلى رسول الله ﷺ بأصحابه ثم جلس في طائفة منهم
فدخل رجل فقام يصلي، فجعل يركع وينقر في سجوده
فقال النبي ﷺ: أترؤن هذا؟ من مات على هذا مات على

غير ملة محمد ينقر صلاته كما ينقر الغراب الدم، إنما مثل الذي يركع وينقر في سجوده كالجائع لا يأكل إلا التمرة والتمرتين فماذا تغنيان عنه"

(Siku moja) Mtume aliwasalisha maswahaba wake, kisha (akageuka) na kukaa pamoja nao kwenye kundi, kisha akaingia mtu mmoja akasimama akasali ikawa anarukuu na kudonoa kwenye sijida yake, akasema Mtume;

"Mna muona mtu huyu? Atakae kufa katika hali hii hufa kwenye mila (dini) isiyokuwa mila ya Muhammad, anadonoa kwenye sala yake kama vile kunguru anavyodonoa kwenye damu, hakika mfano wa yule ambae hurukuu na kudonoa kwenye sijida yake ni kama vile mtu mwenye njaa ambae hali isipokuwa tende moja au tende mbili, vipi zitamtosheleza ?"

Ibin Khuzaima 1/332.

Na imepokewa kutoka kwa Zaid bin Wahabiy akisema; '(siku moja) Hudhaifa alimuona mtu mmoja akisali, ikawa hakamilishi rukuu yake, wala sijida yake),

akasema Hudhaifa (kumwambia yule mtu) bado hujasali, lau kama utakufa, basi utakufa kwenye fitra (dini) isiyokuwa fitra ile aliyomuumba nayo Mwenyezi Mungu Muhammad.' Yaani utakufa katika dini isiyokuwa dini ile aliyomtuma Mwenyezi Mungu Mtume wake Muhammad.

Bukhari 2/274.

Hivyo basi inatakiwa kwa yule mwenye kuacha utulivu kwenye sala atakapojua hukumu yake basi na airejee tena sala ya faradhi ya wakati ule alionao, na atubu kwa Mwenyezi Mungu kwa yale yaliyopita, na wala si lazima kwake kuzirejea sala zote zili~~zopita~~ ambazo alizisali kwa njia hii. Kama ilivyopokewa kwenye hadithi :

«ارجع فصلَ فإنكَ لم تصل»

“Rejea tena ukasali kwa sababu wewe bado hujasali.”

**KUFANYA MCHEZO NA HARAKATI
ZISIZOKUWA NA MAANA KWENYE
SALA.**

Haya ni maafa, na watu wengi wenye kusali hawasalimiki na maafa haya kwa kule kutokunyenyekea kwao kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

﴿وَقَوْمًا لِلَّهِ قَاتِلِينَ﴾..

“Na simameni kwa unyenyekevu katika kumuabudu Mwenyezi Mungu.” Al Baqarah : 238.

Na kauli ya Mwenyezi Mungu:

﴿قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ﴾

“Hakika wamefuzu waislamu ambao katika sala zao huwa ni wanyenyekevu.”

Al Muuminun : 1-2

Na alipoulizwa Mtume kuhusu kuweka vizuri mchanga wakati mtu anapokuwa kwenye sujudi, akajibu kwa kusema:

"لا تمسح وانت تصلي فإن كنت لابد فاعلاً فواحدة
تسوية الحصى"

"Usiufute na hali ya kuwa wewe umo ndani ya sala, kama huna budi kufanya hivyo basi ni kusawazisha kijiwe mara moja." Abou Daud 1/571.

Na wanazuoni wengi wanasema kwamba harakati nyingi zenyenye kufuatana kwa mfululizo bila ya kuwa na sababu au haja ya maana hupelekea kubatilika kwa sala, vipi watu hawa wenye kufanya mchezo kwenye sala zao, hali ya kuwa wamesimama mbele ya Mwenyezi Mungu?! Utaona huyu akiangalia kwenye saa yake, au kurekebisha nguo yake au kukata kucha za vidole vyake kwa meno, au kuzuia pua yake kwa mkono na kutupa macho yake huku na huko au kuangalia mbinguni wala haogopi kukwapuliwa macho yake, au na kuibiwa sala yake na shetani!!

MAAMUMA KUMTANGULIA IMAMU WAKE KWENYE SALA KWA KUSUDI.

Tabia ya binaadamu siku zote ni kuwa na pupa na haraka. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَكَانَ الْإِنْسَانُ عَجُولاً﴾

“Kwani mwanaadamu ni mwenye pupa (kutaka jambo).” Bani Israail : 11.

Na amesema Mtume:

« التَّائِي مِنَ اللَّهِ وَالْعَجْلَةُ مِنَ الشَّيْطَانِ »

“Kufanya mambo kwa utulivu kunatokana na Mwenyezi Mungu, na kufanya mambo kwa haraka haraka kunatokana na shetani.” Al Baihakiy 10/104.

Mara nyingi huona mtu akiwa kwenye sala ya jamaa idadi ya wenyewe kusali wakiwa pembeni yake, kuliani kwake na kushotoni, bali wakati mwingine mtu anaweza kujiona ndani ya nafsi yake jinsi anavyoshindana na Imamu kwenye rukuu au sujudi au kwenye takbira za kuhama kwenye vikao mbali mbali vya sala, na hata

wakati mwingine utaona jinsi wanavyompita Imamu. Japo kama kitendo hiki kinaonekana kutokuwa na umuhimu mkubwa mbele ya watu wengi. Lakini Mtume amekikemea vikali sana kwa kusema:

"أَمَا يَخْشِيُ الَّذِي يَرْفَعُ رَأْسَهُ قَبْلَ الْإِمَامِ أَنْ يَحُولَ اللَّهُ رَأْسَهُ رَأْسَ حَمَارٍ".

"Hivi haogopi yule mwenye kuinua kichwa chake kabla ya Imamu kwamba (huenda) Mwenyezi Mungu akakibadilisha kichwa chake na kuwa kichwa cha punda?"
Muslim 1/320-321.

Kama ikiwa mwenye kusali anatakiwa kuijia sala kwa unyenyekevu na utulivu mkubwa, vipi basi itakuwa hali kwenye sala yenyewe? Haitokuwa huko ndiko kwenye kutakiwa utulivu na unyenyekevu wa hali ya juu?

Inaweza kuwachanganya baadhi ya watu kwa kule kuogopa kumtangulia imamu wakaamua kujichelewesha nae, na wajue kwamba wanazuoni wengi

Mwenyezi Mungu awarehemu wameweka kipimo kizuri kwenye suala hili, nacho ni kwamba, inapaswa maamuma kuanza harakati zake mara tu inapokatika takbira ya imamu, pindi inapoisha (ra) ya ALLAHU AKBAR. Hapo maamuma huanza mara moja harakati zake za kumfuata Imamu. Hatangulii zaidi ya hapo wala kuchelewa, na kwa hali hiyo hupangika mambo.

Na walikuwa maswahaba wa Mtume, **Mwenyezi Mungu awe radhi nao wakijihadhari sana na kumtangulia Mtume kwenye sala hapa anahadithia mmoja wao nae ni Al Baraau bin Aazib Mwenyezi Mungu awe radhi nae, anasema kwamba: "walikuwa wakisali nyuma ya Mtume na anapoinua kichwa chake kutoka kwenye rukuu, sijapata kumuona mtu yoyote akiupinda mgongo wake kwa kusujudu mpaka pale atakapoweza Mtume paji lake la uso kwenye ardhi kusujudu, ndipo**

huanguka (hufuatia) walioko nyuma yake kwa kusujudu."Muslim no. 474.

Na muda alipokuwa Mtume mtu mzima (kuanza kuzeeka) ikawa kuna aina fulani ya uzito kwenye mwili wake na kwenye harakati zake, baadhi ya wenyewe kusali nyuma yake wakawa wanamzindua kama katika njia ya kumfanyia haraka kwenye harakati zake, akawageukia Mtume na kuwaambia:

"يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي بَدَنْتُ فَلَا تَسْبِقُونِي بِالرَّكْوَعِ
وَالسُّجُودِ"

"Enyi watu mimi nimekuwa mzito, basi msinitangulie kwenye rukuu na sujudi." Bayhakii 2/93.

Ni juu ya Imamu kufuata sunna kwenye takbira anapokuwa kwenye sala nayo ni kama ilivyokuja kwenye hadithi ya Abi Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi nae; kuwa

عن أبي هريرة رضي الله عنه: "كان رسول الله صلى الله عليه وسلم، إذا قام إلى الصلاة يكبر حين يقوم ثم يكبر حين يهوي ثم يكبر حين يرفع

رأسه ثم يكبر حين يسجد ثم يكبر حين يرفع رأسه، ثم يفعل ذلك في الصلاة كلها حتى يقضيها، ويكبر حين يقوم من الثنين بعد الجلوس"

‘Alikuwa Mtume akileta takbira wakati anaposimama kusali, kisha huleta takbira wakati anaporukuu, kisha husema “Samiallahu Liman hamidah” wakati anapoinua mgongo wake kutoka kwenye rukuu, kisha husema hali ya kuwa amesimama “rabbanaa walakal hamdu.

Kisha huleta takbira wakati anapoanguka chini kusujudu, kisha huleta takbiira wakati anapoinua kichwa chake kutoka kwenye sijida, kisha huleta takbira wakati anaposujudu tena mara ya pili, na kisha huleta takbira wakati anapoinua kichwa chake, kisha hufanya hivi kwenye sala yote mpaka atakapomaliza, Na huleta takbira wakati anaposimama baada ya kumaliza rakaa mbili za mwanzo.

Anapozifanya Imamu takbira zake kwa utulivu na zenyе kufuatana na kuambatana

na harakati zake humfanya maamuma
kuwa na pupa ya kufuata na kushikamana
na namna iliyotajwa hapo nyuma, hivyo
hutengemaa mambo ya maamuma kwenye
sala yao.

KUIENDEA MISIKITI KWA YULE
ALIYEKULA KITUNGUU MAJI AU
THAUMU AU KITU CHENYE HARUFU
MBAYA.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ يَابْنَيَ آدَمَ حَذِّرُوا زِيَّنَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ ﴾

“Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila sala.” Al Aaraaf : 31.¹

Amesema Mtume:

“قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: من أكل ثوماً أو بصلأً فليعتزل مسجداً وليقعد في بيته”

“Mwenye kula kitunguu thaumu au kitunguu maji basi ajitenge nasi, au akasema na ajitenge na msikiti wetu na akae nyumbani kwake.” Bukhariy 2/339.

Na kwenye mapokezi mengine ya muslim;

“من أكل البصل والثوم والكراث فلا يقرب مسجداً
 فإن الملائكة تتاذى مما يتاذى منه بنو آدم”

¹Yaani nendeni msikitini na nguo nzuri..

“Mwenye kula kitunguu maji na kitunguu thaumu na karaathi (namna ya kitunguu kidogo) basi na asiukaribie msikiti wetu, kwa sababu malaika wanaudhika na yale anayoudhika nayo binadamu.” Muslim 1/395.

Siku moja Omar bin Khataab alikuwa akiwahutubia watu siku ya Ijumaa akasema kwenye khutuba yake: ‘Kisha enyi watu mnakula miti hii miwili, nami sioni isipokuwa ni yenyе kuchukiza, hivi vitunguu maji na thaumu hakika nimemuona Mtume wa Mwenyezi Mungu anapoipata (his) harufu yake kutoka kwa mtu ye yote msikitini huamrisha mtu yule akatolewa kwenye bakii (yaani hutolewa nje ya msikiti), basi mwenye kuila na aive (harufu yake) kwa kuipika.’ Muslim 1/396. (Pia rejea kitabu sifa ya sala ya Mtume cha AlBaaniy 131).

Na inaingia kwenye hukumu hii vile vile wale wenye kuingia msikitini moja kwa moja baada ya kutoka kazini na huku harufu mbaya zikitoka kwenye

makwapa yao na soksi zao. Mbaya kuliko hili ni wale wavutaji wa sigara ambao huvuta sigara hali ya kuwa ni haramu kisha wakaingia misikitini na kuwaudhi waja wa Mwenyezi Mungu mionganini mwa malaika na wenye kusali.

UZINIFU.

Kwa vile makusudio na malengo ya sheria ya kiislamu ni kulinda heshima na kuhifadhi kizazi, kwa sababu hiyo basi imeharimisha zinaa. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَا تَقْرَبُوا الَّذِي كَانَ فَاحِشَةً وَسَاءَ سَيِّلًا﴾

“Wala msikaribie zinaa , hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa)” Israa : 32.

Si hivyo tu, bali sheria ya kiislamu imefunga njia zote zenyet kupelekea kwenye mambo ya zinaa kwa kuamrisha kuvala hijabu na kufumba macho na kuharamisha kukaa faragha baina ya mwanamke na mwanamume wa kando na mambo mengineyo. Mzinifu aliyeoa au kuolewa huadhibiwa kwa adhabu kali, ambayo ni kupigwa kwa mawe mpaka kifo, ili apate kuonja ubaya wa uovu wake, na ipate uchungu kila sehemu ya mwili wake kama vile ulivyostarehe kwenye haramu. Ama

yule mzinifu ambae hajaolewa (haja pata kuingiliwa kwa ndoa ya kisheria iliyo sahihi) yeye atapigwa bakora kwa idadi kubwa iliyopokewa kwenye sheria ambapo ni kupigwa bakora mia moja pamoja na kufedheheshwa kwa kuhudhuria adhabu yake kundi la waislamu ili iwe ni adhabu kwake na hizaya, na kisha atatolewa nje ya mji na kupelekwa mji mwingine nje ya ule aliofanyia uovu wake kwa muda wa mwaka mmoja kamili.

Na adhabu ya mume na mke mzinifu kwenye barazakhi ni kwamba watakuwa kwenye tanuri ambapo juu yake tanuri hilo kutakuwa ni kwembamba na chini yake kutakuwa ni kupana. Kisha watakokewa moto chini ya tanuri hilo nao wakiwa humo hali ya kuwa wako uchi, pindi watakapokokewa moto huo watapiga kelele na kuja juu mpaka wakaribie kutoka nje. Na unapozimwa moto huo hurejea tena ndani, na wataendelea kuishi kwenye adhabu hii mpaka kitakaposimama kiama.

Na mambo huwa mabaya zaidi kwa yule mtu mwenye kudumu kwenye zinaa pamoja na kuwa na umri mkubwa wa uzee na kukaribia kuingia kaburini na Mwenyezi Mungu humuachia muda tu aendelee kwenye uchafu wake. Imepokewa kutoka kwa Abi Huraira kwenye hadithi marfuu;

"ثُلَاثَةٌ لَا يَكْلُمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يَزْكِيْهُمْ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ: شَيْخٌ زَانٌ وَمَلَكٌ كَذَابٌ وَعَانِلٌ مُسْتَكْبِرٌ".

'Watu watatu Mwenyezi Mungu hatozungumza nao siku ya kiama na wala hatowatakasa na wala hatowaangalia na watakuwa na adhabu kali kabisa iumizayo (mzee mwenye kuzini, na mfalme muongo na fakiri mwenye kiburi).' Muslim 1/102-103.

Na machumo ya shari zaīdi ni mahari ya malaya nayo ni ujira anaolipwa malaya baada ya zinaa, na mzinifu mwenye kuishi kwa kutegemea utupu wake ni haramu kwake kujibiwa dua wakati inapofunguliwa milango ya mbingu kwenye nusu ya usiku."

(Rejea Sahihul Jaamiy Hadithi no. 2971).

Kwa hiyo basi ni lazima ieleweke kuwa matatizo ya ufakiri na umasikini sio udhuru unaokubaliwa kisheria kiasi cha kumfanya mtu kuchupa mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na kwenye zama zetu za leo milango yote ya mambo machafu ya zinaa imefunguliwa, na shetani amezirahisisha njia za vitimbi vyake na vitimbi vya marafiki zake, na akafuatwa na waasi na watu waovu. Kutembea uchi kwa wanawake bila kuvala mavazi ya sitara na kujipamba, kumeenea kila sehemu. Kumeenea uhuru wa macho kuangalia mambo ya haramu, kuchanganyika wanawake na wanaume wa kando imekuwa ni jambo la kawaida. Magazeti ya matusi na filamu za mambo machafu zimeenea kila pande. zimeongezeka safari za kwenda kwenye miji ya uovu, madanguro, biashara ya umalaya imeshamiri na kuenea kila pande, vitendo vya ubakaji vimekuwa vingi na hatimae kuongezeka idadi ya watoto wa haramu na kutoa mimba

Mola wetu! Tunakuomba rehema zako na upole wako na sitara yako na ulinzi kutoka kwako, wenyе kutulinda na mambo machafu. Tunakuomba ututakase nyoyo zetu na uzilinde tupu zetu na ujaalie baina yetu na haramu ukuta na kizuizi chenye kuzuia.

LIWATI (UFIRAJI).

Madhambi ya watu wa Luti yalikuwa ni kuingiliana wanaume kwa wanaume (kufirana), Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ولوطا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ إِنْكُمْ لَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِّنَ الْعَالَمِينَ أَنْكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ وَتَقْطَعُونَ السَّبِيلَ وَتَأْتُونَ فِي نَادِيكُمُ الْمُنْكَر﴾

“Na (wakumbushe Nabii) luti alipowaambia watu wake; ‘Bila shaka nyinyi mnafanya uovu (ambao) hakuna yoyote aliyekutangulieni, kwa (uovu) huo katika walimwengu. Je mnawaenda wanaume, na mnawakatia njia (watu kwa kuwaua na kuwanyang’anya njiani) na mnafanya maovu katika mikusanyiko yenu?’” Al Ankabuut : 28-29.

Na kutokana na uovu na ubaya uliopita kiasi wa dhambi hii na uhatari wake, Mwenyezi Mungu aliwaadhibu wale wenye kuifanya kwa adhabu za aina nne kwa mara

moja ambapo hajawahi kuwaadhibu kwa pamoja adhabu hizo watu wa aina yoyote kabla yao. Kwanza Mwenyezi Mungu aliyapofua macho yao na akaigeuza ardhi na kuwa chini juu, juu chini, akawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu wa motoni uliokamatana na akawapelekea ukelele mkali wa kutisha.

Kwa hiyo hukumu ya kitendo hiki kiovu kwenye sheria yetu ya kiislamu kulingana na kauli yenyenye nguvu ya wanazuoni wetu ni kuuawa kwa upanga ili iwe ni adhabu kwa mfanyaji na mfanywaji (yaani mfiraji na yule mwenye kufirwa). Pindi itakapokuwa kitendo hiki kimefanyika kwa ridhaa na uchaguzi wa mtu bila kulazimishwa au kutumia nguvu.

Imepokewa kutoka kwa Ibin Abbas kwenye hadithi marfuu;

"من وجدتهم يهـ عمل قـوم لـوط فـاقتـلوا الفـاعـلـ
وـالـمـفـعـولـ بـهـ"

‘Mtakaemkuta akifanya kitendo cha watu wa Luti, basi muueni mfanyakaji na mfanywaji.’ Imam Ahmad 1/300.

Na mambo yanayotokea kwenye miaka hii miongoni mwa tauni na aina mbali mbali za magonjwa ambayo hayajawahi kutokea kwa mababu zetu waliopita kama vile ugonjwa wa ukimwi wenyе kuangamiza mamilioni ya watu ni kwa sababu ya kuenea mambo machafu. Na hii inaonyesha hekima fulani kutoka kwenye hekima za Mwenyezi Mungu kwa kule kuichagua kwake adhabu hii yenye kuumiza na kuangamiza.

MWANAMKE KUMNYIMA UNYUMBA
MUMEWE BILA YA KUWA NA
UDHURU WA KISHERIA.

Imepokewa kutoka kwa Abii Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi nae kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwamba amesema:

"إذا دعا الرجل امرأته إلى فراشه فأبى فبات غضبان
عليها لعنتها الملائكة حتى تصبح"

"Pindi mwanamume anapomwita mkewe kitandani kisha akakataa mwanamke (kujibu wito huo) na akalala mumewe usiku huo hali ya kuwa amemkasirikia, basi malaika humlaani mwanamke huyo mpaka kutakapopambazuka." Bukhariy (Angalia Fathul Baariy. 6/314.

Kunapotokea kutokuelewana na ugomvi baina ya mke na mume, wengi katika wanawake huwaadhibu waume zao kwa kuwanyima haki zao za unyumba. Kitendo hiki husababisha kutokea ujisadi mkubwa kwa waume, kama vile mume kuingia kwenye vitendo vya haramu kwa kuzini nje

ya ndoa, na wakati mwingine mambo huwa mabaya kwa mwanamke huyo hasa pale anapofikia mume kuchukua uamuzi wa kuoa mke mwingine zaidi juu yake.

Kwa hiyo ni wajibu kwa mke kufanya haraka kuujibu mwito wa mumewe pindi anapotakiwa. Kwa ajili ya kufuata na kunyenyeka kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, isemayo:

”إذا دعا الرجل امرأته إلى فراشه فلتجب وإن كانت على ظهر قتب“

“Pindi mwanamume anapomwita mkewe kwenda kitandani ni wajibu kuujibu mwito huo hata kama (Mwanamke huyo) atakuwa juu ya mgongo wa ngamia.” Zawaidul Bazaar 2/181.

Na juu ya mume kuchunga na kuangalia hali ya mkewe kama vile anapokuwa mkewe mgonjwa, au mja mzito au mwenye matatizo ili yapate kudumu kati yao maafikiano na mapenzi na kutoingia kwenye magomvi.

MWANAMKE KUTAKA TALAKA KWA MUMEWE BILA YA KUWA NA SABABU ZA KISHERIA.

Wanawake wengi huwa na pupa na haraka ya kuomba talaka kutoka kwa waume zao pindi zinapotokea tofauti ndogo ndogo kati yao. Au kuomba talaka ikiwa mume hakumpa kitu fulani anachotaka kutoka kwenye mali. Wakati mwingine hushawishiwa kufanya hivyo na baadhi ya jamaa zao wa karibu au majirani zao waovu au mashoga zao. Na hatimae huamua mwanamke huyo kumkabili mumewe kwa kumtolea maneno machafu yenye kuchukiza na kuchochea ghadhabu kama vile kumwambia mumewe; ‘Kama wewe ni mwanamume kweli hebu nipe talaka yangu tuone!’

Kama inavyojulikana kitendo cha kutoa talaka husababisha kutokea ujisadi mkubwa nyuma yake, kama vile kutengana familia na kupotea watoto.

Hali hii humpelekea mwanamke kuja kujuta baadae wakati ambapo majuto huwa hayafai tena. Na kwa sababu hii basi na nyinginezo, ndipo unapoonekana na kudhihirika utukufu na hekima za sheria za kiislamu pale ilipokuja na sheria yenyekumkataza mwanamke kuomba talaka kutoka kwa mumewe bila ya kuwa na sababu ya msingi yenyekukubalika kisheria na yenyemana.

Imepokewa kutoka kwa Thaubani Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwenye hadithi marfuu kwamba;

"أيما امرأة سألت زوجها الطلاق من غير ما بأس
فحرام عليها رانحة الجنة"

'Mwanamke yoyote aliyemuomba talaka mumewe bila ya kuwa na tatizo basi ni haramu kwake (kuipata) harufu ya pepo.'

Ahmad 5/277.

Na kutoka kwa Uqba bin Aamir Mwenyezi Mungu awe radhi nae amesema;

"إن المختلعتات والمنتزعات هن المنافقات"

‘Hakika wale wanawake wenyewe kujiachisha na kujitoa (kwa waume zao) hao ndio wanafiki.’ Tabrani 17/339.

Lau kama ataomba talaka kutoka kwa mumewe kutokana na sababu za kisheria, kama vile mume kuwa hasali, au mlevi au kuwa anatumia madawa ya kulevyia, au kuwa anamlazimisha kwa nguvu kufanya mambo yaliyoharamishwa kisheria au kuwa anamdhulumu kwa kumuadhibu au kuwa anamnyima haki zake kisheria, na mfano wa hayo; na wakati huo ikawa nasaha hazifai tena, na mapatanisho hayakuleta faida yoyote, kwa hali hii basi kama mwanamke ataomba talaka yake kwa ajili ya kutaka kuinusuru na kuilinda dini yake huwa hana makosa mbele ya Mola wake na wakati huo tena huwa inajuzu kwake kisheria kuomba talaka.

DHIHARI -(KUMWITA MKEO MAMA YAKO)

Miongoni mwa matamshi ya kijahilia (kipagani) yalioenea kwenye umma huu ni kuingia kwenye dhihari nako ni kama vile mume kumwambia mkewe; 'Wewe kwangu mimi ni kama mgongo wa mama yangu au dada yangu.' Na mfano wa matamshi kama hayo ambayo sheria ya kiislamu umeyachukia kutokana na kuwapo ndani yake dhuluma kwa mwanamke, na Mwenyezi Mungu ameyaeleza kwa kusema: ﴿الذين يظاهرون منكم من تساندهم ما هن أمهاتهم إن أمهاتهم إلا الالئي ولدتهم وإنهم ليقولون متكرأ من القول وزورا وإن الله لغفور غفور﴾

“Wale miongoni mwenu wawaitao wake zao mama zao (kwa hivyo wakajiepusha nao wasiwaingilie wala wasiwape ruhusa kuolewa na waume wengine) hao si mama zao, hawakuwa mama zao ila wale waliowazaa, wanasema neno baya na la

uongo na Mwenyezi Mungu ni mwenye msamaha na mwenye maghufira.”

Al Mujaadala : 2

Na sheria ya kiislamu kwa kuona uzito wa jambo hili ukaweka kafara nzito sawa sawa na kafara ya mtu mwenye kumuingilia mkewe kwenye mchana wa Ramadhani. Na haifai kwa mwenye kumwambia mkewe wewe ni kama mama yangu kumuingilia mkewe isipokuwa baada ya kuleta kafara. Akasema Mwenyezi Mungu:

﴿وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَاتَلُوا
فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مَّنْ قَبْلُ أَنْ يَتَمَّاسَ دَلِكُمْ شُوَعْظُونَ بِهِ وَاللَّهُ
يَعْلَمُ مَا تَعْمَلُونَ خَيْرٌ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصَيَّامُ شَهْرَيْنِ مُتَّسِعَيْنِ
مِنْ قَبْلُ أَنْ يَتَمَّاسَ فَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَإِطْعَامُ سِتِّينَ مِسْكِينًا
دَلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتَلَكَ حُدُودُ اللَّهِ وَلِلْكَافِرِينَ
عَذَابُ الْيَمِّ﴾

“Na wale wawaitao wake zao mama zao, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema (wakataka kuwarejea wake zao kama kidesturi ya mke na mume) basi wampe

mtumwa uhuru kabla ya kugusana, mnapewa maonyo kwa haya, na Mwenyezi Mungu anajua (yote) mnayoyatenda. Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu ya miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana, na asiyeweza basi awalishe maskini sitini (kila maskini kibaba kimoja cha chakula kinacholiwa mahala hapo) (mumeambiwa) haya ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi mungu (msipindukie); na kwa makafiri iko adhabu iumizayo.”

Al Mujadala :3-4

KUMUINGILIA MKE AKIWA KWENYE HEDHI.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْمَحِيطِ فَلَنْ هُوَ أَدْيٌ فَاعْتَزِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيطِ وَلَا تَقْرِبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهَرْنَ ﴾ ...

“Na wanakuuliza juu ya hedhi, waambie huo ni uchafu, basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi (zao) wala msiwakaribie mpaka watwaharike.” Al Baqarat : 222.

Wala haifai kumuingilia mwanamke kipindi hiki mpaka

atakapooga baada ya kutwaharika; kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu :

﴿ فَإِذَا ظَهَرْنَ فَأُثْوَهْنَ ﴾ ...

“Wakisha kutahirika basi waendeeni katika pale alipokuamrisheni Mwenyezi Mungu.”

Al Baqarat : 222.

Na vile vile Mtume amezungumzia ubaya wa maasi haya pale aliposema:

” من أتى حانضاً أو امرأة في دبرها أو كاهناً فقد كفر بما أنزل على محمد ”

“Mwenye kumuendea (kumuingilia) mwanamke akiwa kwenye hedhi, au akamuendea (akamuingilia) kwenye tupu yake ya nyuma au akamuendea kuhani (mtabiri, mpiga ramli) basi atakuwa ameyakufuru yale yote aliyoteremshiwa Muhammad.” Tirmidhiy 1/243.

Mwenye kufanya kitendo hiki kwa bahati mbaya, kwa ujinga bila kukusudia na hali ya kuwa hajui hukumu yake basi huyo hana makosa. Ama yule mwenye kufanya kitendo hiki kwa kusudi hali ya kuwa anajua hukumu yake, basi atapaswa kutoa kafara kama walivyokwenda baadhi ya wanazuoni , na kafara yake huwa ni dinari moja au nusu dinari.

Wanazuoni wameenda kwa kusema ana uhuru wa kuchagua kati ya kutoa dinari moja au nusu dinari. Na wengine wakasema kwamba kama atamuingilia mkewe mwanzo wa hedhi kwenye mbubujiko wa damu, hapo atapaswa kutoa dinari, na kama atamuingilia mwisho wa damu pindi

**unapopungua mbubujiko wake au kabla
hajaoga na kutwaharika na hedhi atapaswa
kutoa nusu dinari.**

**Na dinari moja kwa makadirio ya kawaida
ni sawa na gramu 2.25 za dhahabu. Atatoa
sadaka hizo dhahabu au atatoa fedha zeny
thamani ya kiwango hicho cha dhahabu¹.**

¹ Na sahihi ni kuwa mwenye kufanya kitendo hiki ana
uhuru wa kuchagua, aidha kutoa dinari au nusu dinari,
sawa iwe amefanya kitendo hiki mwanzo wa hedhi au
mwisho wa hedhi. Ibin Bazi.

KUMUINGILIA MKE KWA NYUMA ‘KWENYE TUPU YA NYUMA.’

Baadhi ya watu wasiokuwa na tabia ya kawaida, dhaifu wa imani huwa hawajizui na matamanio ya nafsi zao, hatimae huwa^{ingilia} wake zao kwenye tupu zao za nyuma (kwenye sehemu ya kutolea haja kubwa). Kitendo hiki ni katika madhambi makubwa, na Mtume amemlaani kila yule mwenye kufanya kitendo hiki. Imepokewa kutoka kwa Abi Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwamba:

"ملعون من أتى امرأة في دبرها"

"Amelaaniwa yule mwenye kumuingilia mkewe kwenye tupu yake ya nyuma."

Imam Ahmad 2/479.

Si haya tu bali pia Mtume amesem

"من أتى حائضاً أو امرأة في دبرها أو كاهناً فقد كفر بما أنزل على محمد"

"Mwenye kumuendea (kumuingilia) mwanamke akiwa kwenye hedhi , au kumuendea (kumuingilia) kwenye

tupu yake ya nyuma au akamuendea kuhani (mtabiri, mpiga ramli) huwa ameyakufuru yale yote aliyoteremshiwa Muhammad.” Tirmidhiy : 1/243.

Pamoja na kwamba wake wengi wenyе tabia nzuri, wenyе maumbile ya salama huwa hawakipendi kitendo hiki na kukataa pindi wanapotakiwa kufanya hivi, lakini baadhi ya waume huwatisha kwa talaka kama hawakutii, na baadhi ya waume huwahadaa wake zao ambao huona haya kuwauliza wanazuoni na kuwafanya waone kwamba kitendo hiki ni halali. Na huleta dalili kwa kutumia kauli ya Mwenyezi mungu isemayo:

﴿نِسَاؤُكُمْ حَرَثُ لَكُمْ فَاثُوا حَرَثُكُمْ أَنِّي شَيْئُمْ﴾ ...

“Wake zenu ni kama konde zenu (mashamba yenu) basi ziendeeni konde zenu mpendavyo.” Al Baqarat : 223.

Na ilivyo kawaida, sunna huitaffsiri Qur’ani na kuiweka wazi, kwa maana hiyo basi imepokewa kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake akieleza kwamba

inajuzu kumuingilia mwanamke kwa staili yoyote aipendayo mtu. Iwe kwa kutokea nyuma au kutokea mbele maadamu lengo la staili hizo litakuwa ni kupata tupu ya mbele kwenye sehemu ile ya kutokea mtoto. Na wala sijambo la kuficha kwamba tupu ya nyuma na sehemu ya kutolea haja kubwa sio sehemu ya kutokea mtoto. Na mionganini mwa sababu za kutokea kitendo hiki kiovu ni kule kuingia kwenye maisha safi ya ndoa wakati mtu bado ana mabaki ya urithi wa kijahilia wa kufanya mambo machafu yasiokuwa ya kawaida, ambayo yameharamishwa katika dini, au akiwa bado amejawa na mkusanyiko wa kumbukumbu za filamu za uchafu (sex film) na kuamua kuingia kwenye maisha ya ndoa kabla ya kutubia kwa **Mwenyezi Mungu**. Na ieleweke wazi kwamba kitendo hiki kimeharamishwa vikali kwenye dini hata kama yatapatikana maafikiano na makubaliano na ridhaa kutoka pande zote mbili zinazohusika, yaani mke na mume,

kwani kukubaliana kwenye jambo la haramu hakulibadilishi jambo hilo na kuwa halali kisheria.

KUTOFANYA UADILIFU BAINA YA WAKE.

Miongoni mwa mambo muhimu aliyo tuusia
Mwenyezi Mungu kutoka kwenye kitabu
chake kitukufu ni kufanya uadilifu na
usawa kati ya wake bila upendeleo kati ya
mke na mke.

Akasema Mwenyezi Mungu:

﴿وَلَنْ يَسْتَطِعُوا أَنْ تَعْذِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَنْ حَرَصُوكُمْ فَلَا
 تَمْبَلُوا كُلَّ الْمَيْلِ فَتَذَرُّوهَا كَالْمُعْلَقَةِ وَإِنْ تَصْلِحُوا وَتَنْقُوا
 فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُورًا رَّحِيمًا﴾

“Nanyi hamuwezi kufanya uadilifu (kweli kweli) baina ya wake, ijapokuwa mtataka kufanya hivyo, kwa hiyo msielekee (upande mmoja) kabisa, msije kumwacha (huyo mwengine msiyempenda) kama aliyeangikwa (aliyetundikwa anasukumika huku na huku; hajijui kuwa ana mume au mjane). Na mkisulu hiana (sasa) na mka mcha Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi

Mungu ni mwingi wa msamaha (na) mwingi wa rehema.” An-nisaa : 129.

Uadilifu unaokusudiwa hapa ni ule uadilifu kwenye kulala. Ni kwamba kila mke lazima awe na siku sawa na mwenzie, na kumpa kila mmoja haki yake kwenye matumizi na mavazi sawa na mwenzie bila kubagua kati yao, na wala haukusudiwi hapa uadilifu wa mapenzi ya moyo, kwa sababu hakuna mja mwenye kuweza kuyamiliki mapenzi ya moyo.

Baadhi ya watu wanapokuwa na mke zaidi ya mmoja humili kwa mmoja wao na kumtelekeza yule mwengine aliyebaki na kulala kwake masiku mengi zaidi ya mwingine, au kumkatia matumizi makubwa na kumpunja yule mwengine. Kitendo hiki ni haramu, na mwenye kukifanya atakuja siku ya kiama akiwa kwenye hali ile aliyoielezea Mtume kutoka kwenye Hadithi ya Abi Huraira kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa amesema:

"من كانت له امرأتان فمال إلى إحداهما جاء يوم
القيمة وشقه مائل"

"Mwenye kuwa na wake wawili kisha
akamili kwa mmoja wapo atakuja siku ya
kiama hali ya kuwa bega lake moja limemili
upande mmoja." Abu Daud 2/601.

**KUKAA FARAGHA BAINA YA
MWANAMUME NA MWANAMKE WA
KANDO.**

Shetani anapupa ya kuwafitinisha watu na kuwaingiza kwenye haramu, kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu ametutahadharisha nae kwa kusema:

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَبَعُوا أَخْطَوَاتِ الشَّيْطَانِ وَمَنْ
يَتَّبِعُ أَخْطَوَاتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ﴾ ...

“Enyi mlioamini msifuate nyayo za shetani, na atakaefuata nyayo za shetani (atapotea), kwani yeye huamrisha mambo machafu na mabaya.” An-Nuur : 21.

Na shetani hupita kwenye mwili wa binaadamu kwa kutumia mishipa ya damu. Na mionganini mwa njia za shetani anazotumia katika kumuingiza mtu kwenye mambo machafu ni kule kukaa faragha baina ya mwanamume na mwanamke wa kando. Kwa sababu hiyo basi, sheria ya kiislamu ikaamua kuifunga kabisa njia

hiyo, kama ilivyokuja kwenye kauli ya Mtume:

" لا يخلون رجل بامرأة إلا كان ثالثهما الشيطان " "Hakai faragha mwanamume na mwanamke isipokuwa shetani huwa ni wata tu wao." Tirmidhiy 3/474.

Haijuzu kabisa kwa mwanamume kukaa faragha na mwanamke wa kando iwe nyumbani au chumbani au kwenye gari, kama vile kukaa faragha na mke wa ndugu yako, au msichana wa kazi kama vile mtumishi au kukaa muuguzi wa kike na daktari wa kiume kwenye chumba kimoja, na kadhalika. Watu wengi huipuuzia hali hii ima kwa kujiamini kwenye nafsi zao au vingine, lakini matokeo yake huingia kwenye mambo machafu bila wao kujitambua au kukaribia kuingia kwenye mambo haya na kusababisha ongezeko la watoto wa haramu na mchanganyiko wa nasaba.

KUPEANA MIKONO NA WANAWAKE WA KANDO.

Hiki ni kitendo kilichoenea katika jamii nyingi za watu, na kudhulumu sheria za Mwenyezi Mungu. Hasa katika zile jamii zilizotawaliwa na mazoea, au tamaduni na ada za kijahilia na kufanya mila za watu kuwa juu ya hukumu za Mwenyezi Mungu. Hata kama utajaribu kumfahamisha mmoja wao kuhusu hukumu ya sheria za Mwenyezi Mungu, na ukamsimamishia hoja za wazi na kumbainishia dalili atakutuhumu kuwa una mambo ya kizamani yaliopitwa na wakati, na mwenye matatizo, na kuwa unataka kukata undugu na kuwatilia mashaka watu wenye nia nzuri. n.k.

Kwa hiyo imekuwa kupeana mikono na mabinti wa mababa wadogo, mabinti wa wajomba, mabinti wa shangazi, mabinti wa mama wadogo na mke wa ndugu yako n.k ni kitu chepesi sana kwenye jamii zetu kuliko hata kunywa maji, lau kama

wataliangalia suala hili kwa mtizamo wa ndani kabisa kuhusu hatari iliyoko ndani yake kisheria basi wasingethubutu hata siku moja kufanya jambo hili.

Amesema Mtume:

” لأن يطعن في رأس أحدكم بمحيط من حديد خير له
من أن يمس امرأة لا تحل له ”

”Kuchomwa na sindano ya chuma kwenye kichwa cha mmoja wenu ni bora kwake kuliko kumgusa mwanamke asiyekuwa halali kwake.” Tabrani 20/212.

Bila shaka kitendo hiki ni katika zinaa ya mikono kama anavyosema Mtume:
” العينان تزنيان واليدان تزنيان والرجلان تزنيان
والفرج يزني ”

”Macho mawili huzini, na mikono miwili huzini, na miguu miwili huzini na tupu huzini.” Imam Ahamad 1/412.

Je kuna mtu yejote ambae moyo wake utakuwa umetakasika kuliko Mtume Muhammad rehema na amani ziwe juu yake, na pamoja na hayo yeye anasema:
»إني لا أصافح النساء«

“Mimi sipeani mikono na wanawake.”
Ahmad 6/357.

Na akasema tena:

«إني لا أمسك أيدي النساء»

“Mimi siigusi mikono ya wanawake.”
Tabraaniy 24/342. (Angalia Al-Iswaabat 4/354. Chapa ya Daarul Kitaabil Arabiy).

Na imepokewa kutoka kwa Bi Aisha mwenyezi Mungu awe radhi nae; ``, Naapa kwa Mwenyezi Mungu katu haujawahi mkono wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuugusa mkono wa mwanamke yoyote isipokua alikuwa akichukua kiapo chao cha uaminifu (baia) kwa maneno.``

Muslim 3/1489

Na wamuogope Mwenyezi Mungu wale watu wanaotishia kuwapa talaka wake zao walio wema wacha Mungu pindi wakataapo kuwapa mikono ndugu zao. Na inafaa ifahamike kwamba kuweka kizuizi au

**kupeana mikono nyuma ya kitambaa
hakusaidii chochote, bali hali zote mbili ni
haramu.**

**MWANAMKE KUJITIA MANUKATO
WAKATI WA KUTOKA NA
KUJIPITISHA MBELE YA WANAUME.**

**Jambo hili limeenea mno kwenye zama zetu
pamoja na kuwapo onyo kali kutoka kwa
Mtume rehema na amani ziwe juu yake:
"أيما امرأة استعترت ثم مرت على القوم ليجدوا
ريحها فهي زانية"**

“Mwanamke yoyote aliyejitia uturi (manukato) kisha akajipitisha mbele ya watu ili waipate harufu yake, basi mwanamke huyo ni mzinifu.” Imamu Ahmad 4/418.

Mghafala, dharau na hali ya kutojali waliokuwa nayo baadhi ya wanawake huwafanya kulipuza jambo hili na kutolitilia maanani ipasavyo. Lakini sheria ya kiislamu imesisitiza vikali kwamba mwanamke yoyote mwenye kujitia manukato kisha akatoka nje japo kama atakuwa amekwenda msikitini ni lazima

aoge josho la janaba. Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

”أيما امرأة تطيبت ثم خرجت إلى المسجد ليوجد
ريحها لم يقبل منها صلاة حتى تغسل اغتسالها من
الجناية“

“Mwanamke yoyote aliyejitia manukato kisha akatoka kwenda msikitini ili (wanaume) waipate harufu yake hatokubaliwa sala yake mpaka atakapooga josho lake la janaba.” Imam Ahmad 2/444.

Mwenyezi Mungu ndie mwenye kushitakiwa na kupelekewa malalamiko yetu juu ya unyonge wetu kutokana na hali iliyopo hivi sasa ya kuwapo mabuhuri na maudi kwenye maharusi na sherehe za wanawake wa kiislamu. Utawaona wanawake wa zama zetu wakishindana kwa manukato ya aina mbali mbali wakati wa kwenda kwenye sherehe hizo, na wakati mwingine hutumia manukato yenyé harufu kali wakiwa masokoni, au kwenye usafiri, au kwenye jamii zenyé kuchanganyika wanawake na wanaume pamoja,

na hata misikitini kwenye masiku ya ramadhani. Inafaa ieleweke kuwa sheria imeweke wazi kwamba, manukato ya mwanamke yanatakiwa yawe yale yenyé kudhihirisha rangi na kupotea au kujificha harufu yake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu asitughadhhibikie na asiwaadhibu watu wema wanawake kwa wanaume kutokana na vitendo vya wapumbavu wa kike na kiume na awaongoze wote kwenye njia yake iliyonyooka.

**MWANAMKE KUSAFIRI AKIWA PEKE
YAKE BILA YA KUWA NA MAHARIMU
WAKE.**

Imepokewa kutoka kwa Bukhariy na Muslim kutoka kwa Ibin Abbas Mwenyezi Mungu awe radhi nae yeye na baba yake akisema;

" لا تُسافر المرأة إلا مع ذي حرم "

'Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba hasafiri mwanamke (peke yake) ila (kwa kufuatana) pamoja na maharimu wake.' Muslim 2/977.

Hukumu hii ni kwa safari za aina zote. Hata safari ya Hija haruhusiwi pia mwanamke kusafiri peke yake. Na kusafiri kwake peke yake huwahadaa baadhi ya mafasiki na kuwapa fursa ya kumsumbuu au kumuudhi na hali ya kuwa yeye ni dhaifu na huenda akachukuliwa, na uchache wa hayo yote ni kule kuudhiwa na kuvunjiwa heshima na utu wake.

Na hata kumpandisha ndege japo kama atakuwapo ndugu yake wa karibu (maharimu wake) wa kumsindikiza na kumuaga na kuwapo maharimu wake wa kumpokea anapofika kama wanavyodai baadhi ya watu, lakini nani atakaepanda nae na kukaa nae kwenye kiti cha jirani yake ndani ya ndege? Na lau kama itatokea hitilafu na kulazimika ndege kutua kwa dharura kwenye uwanja mwengine usiotarajiwa au ikatokea kuchelewa kutoka kwenye muda uliopangwa. Mambo yatakuwaje kwenye hali kama hii? Visa na matukio ni mengi hayataki kuhadithiwa. Kwa hiyo basi inashurutishwa kwa maharimu shuruti nne nazo ni awe muislamu, baleghe, mwenye akili, na awe mwanamume kama alivyosema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

"...أبوها أو ابنتها أو زوجها أو أخوها أو ذو محرم منها"

**“Baba yake, au mwanawe wa kiume, au
mumewe au kaka yake au maharimu
wake.” Muslim 2/977.**

**KUMUANGALIA KWA KUSUDI
MWANAMKE WA KANDO.**

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿فَلِلْمُؤْمِنِينَ يَغْضُبُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ
ذَلِكَ أَزْكَى لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَيْرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ﴾

“Waambie waislamu wanaume wainamishe macho yao, (wasitizame yaliokatazwa) na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; bila shaka Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) wanayoyafanya.” Surat Nuur : 30.

Anasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

”فَزَنَا الْعَيْنُ النَّظَرُ... ”

“Na zinaa ya jicho ni kuangalia.” -yaani kuangalia maharamisho ya Mwenyezi Mungu. Bukhariy -Fathul Baariy 11/26.

Inajuzu kwa daktari kumuangalia mwanamke wa kando kwa dharura za kisheria kama vile kwenye matibabu, na mwenye kuposa pia anaruhusiwa kumuangalia mchumba wake.

Ni haramu vile vile kwa mwanamke kumuangalia mwanamume wa kando kwa jicho la pozi na tabasamu. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ ﴾ ...

“Na waambie waislamu wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao.” Surat Nuur : 31.

Ni haramu kwa mwanamume kuiangalia tupu ya mwanamume mwenzie, kama ilivyo haramu pia kwa mwanamke kuiangalia tupu ya mwanamke mwenzie. Kila tupu iliyokuwa haramu kwako kuiangalia basi ni haramu pia kuigusa japo kama utafanya hivyo ukiwa nyuma ya pazia au sitara.

Na mionganini mwa michezo ya shetani anayowachezea baadhi ya watu ili kuwavuta kwenye mambo machafu ni kule kuangalia picha zilizomo kwenye magazeti na kuangalia filamu kwa hoja kwamba sio vitu vya ukweli, lakini ufisadi na uchocheaji

**wa matamanio ya nafsi unaopatikana
kwenye uangaliaji wa picha hizo na filamu
hizo uko wazi kwa kila mtu.**

DIYAATHA: KUTOKUWA NA WIVU.

Imepokewa kutoka kwa Ibn Omar, Mwenyezi Mungu awe radhi nae yeye na baba yake kwenye hadithi marfuu; "ثلاثة قد حرم الله عليهم الجنة: مدمن الخمر، والعاق، والديوث الذي يقر في أهله الخبث"

"Watu watatu Mwenyezi Mungu amewaharamishia pepo. Mwenye kunywa pombe, mwenye kuasi wazazi wake, na duyuthi (yule asiyekuwa na wivu) ambae huruhusu uovu (mambo machafu) kwa watu wa nyumbani kwake." Imamu Ahmad 2/69.

Miongoni mwa uovu mkubwa unaofanywa majumbani mwetu kwenye zama zetu za leo ni kuwaruhusu mabinti wetu au wanawake wetu majumbani mwetu kuwasiliana na wanaume wa kando na kuzungumza nao mazungumzo ya mapenzi au kuruhusu mmoja wa wanawake wa nyumbani kwako kukaa faragha na mwanamume wa kando, na vile vile

kumuacha mmoja wa wanawake wa nyumbani kwako kupanda gari peke akiwa na mwamume wa kando kama vile dereva wa taxi n.k. Kuwaruhusu wanawake kutoka bila kucaa hijabu ya kisheria na kuwafanya wanaume wanaokwenda huku na huko kustarehe nao. Vile vile kuleta filamu na magazeti yenyeye kueneza ufisadi, ufasiki na uasherati na kuyaingiza nyumbani.

**KUDANGANYA NASABA YA MTOTO
NA KUMNASIBISHA NA MTU
ASIYEKUWA BABA YAKE, NA MTU
KUMKANA MWANAE.**

Haijuzu kisheria kwa muislamu kujinasibisha na mtu asiyekuwa baba yake au kujinasibisha na watu ambao hahusiani nao hata kidogo kiukoo, na baadhi ya watu hufanya kitendo hiki kwa tamaa ya pesa , na kuthibitisha nasaba ya uongo kwenye fomu, na wengine hufanya kitendo hiki kwa kumchukia baba yake ambae labda alimtelekeza au kumuacha wakati alipokuwa mdogo. Mambo haya yote ni haramu katika sheria, na husababisha kupatikana ujisadi mkubwa kwenye mambo mbali mbali , kama vile kwenye maharimu, ndoa, mirathi n.k. Na imepokewa kutoka kwenye Sahihul Bukhariy kutoka kwa Saad na Abii Bakra Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote kwenye hadithi marfuu;

" من ادعى الى غير أبيه وهو يعلم فالجنة عليه حرام "

‘Mwenye kujiita (kujinasibisha) kwa mta
asiyekuwa baba yake na hali ya kuwa
anajua (kuwa huyo anaejinasibisha kwake
sio baba yake) basi pepo ni haramu
kwake).’’ Bukhariy Fat-hul Baariy 8/45.

Ni haramu katika sheria kufanya
kitu ambacho ndani yake kuna kuchezea au
kutukana nasaba au kudanganya

Baadhi ya watu wanapogombana na
wake zao huwatuhumu kuwa wamezini nje
ya ndoa na kujivua na mtoto wake bila ya
kuwa na ushahidi wowote, hali ya kuwa
huyo mtoto ametoka kwenye kitanda chake.
Na baadhi ya wanawake huzisaliti amana
zao na kuzini nje ya ndoa na kupata mimba
na kuingiza kwenye nasaba ya mumewe
mtoto ambae hatokani nae. Na Mtume
ameonya vikali kuhusiana na hali hii kama
ilivyopokewa kutoka kwenye hadithi ya Abi
Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi nae
kwamba amemsikia Mtume wa Mwenyezi
Mungu akisema wakati ilipoteremshwa aya
ya Mulaana: .

"أيما امرأة أدخلت على قوم من ليس منهم فليست من الله في شيء ولن يدخلها الله جنته، وأيما رجل جد ولده وهو ينظر إليه احتجب الله منه وفضحه على رؤوس الأولين والآخرين"

"Mwanamke yoyote aliyemuingiza kwa watu mtoto ambae si katika wao, mwanamke huyo hatokuwa na chochote mbele ya mwenyezi Mungu na hatomuingiza kwenye pepo yake. Na mwanamume yoyote aliyemkana mwanaehali ya kuwa anamuangalia, Mwenyezi Mungu atajizuia nae na atamfedhehesha mbele ya watu wa mwanzo na wa mwisho (siku ya kiama)." Abou Daud 2/695 - Mishkaatil Masaabih uk. 3316.

KULA RIBA.

Mwenyezi Mungu hajatangaza kuwa na vita na mtu yoyote kwenye kitabu chake isipokuwa kwa watu wenyewe kula riba.
Anasema Mwenyezi Mungu:

﴿يَا يَهُودَ الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ الْرِّبَا إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ فَإِنَّمَا لَمْ تَفْعُلُوا فَأَذْنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ﴾ ...

“Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na acheni yaliyobakia katika riba, ikiwa mmeamini. Na kama hamtafanya (hivyo) basi fahamuni mtakuwa na vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake.” Al Baqara : 278-279.

Hii inatosha kabisa kuonyesha uovu na ubaya wa kitendo hiki mbele ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kuangalia usawa wa maisha kati ya mtu mmoja mmoja na mataifa, bila shaka ataona upeo wa uharibifu na uangamivu ulioachwa nyuma kutokana na kufanya biashara kwa njia ya

riba, kuanzia kafilisika, kukosa masoko, kuharibika kwa bidhaa, kushindwa kulipa madeni, kuanguka kwa uchumi, ongezeko la idadi ya watu wasiokuwa na kazi na kuanguka kwa mashirika na viwanda mbali mbali. Haikuwa hii isipokuwa ni matokeo ya riba, na hivyo kufanya mashirika mengi na viwanda kufanya juhudi ya pato la kila siku na jasho la kazi za kila siku litumike kwa kulipa madeni ya riba yasiokwisha kwa mla riba. Na matokeo ya hali hii ni kupatikana matabaka ya watu kwenye jamii, na kufanya mali nyingi ikusanyike kwenye mikono ya watu walio wachache.

Huenda ikawa hali hii ni sehemu tu ya picha ya vita ambavyo Mwenyezi Mungu amewaaahidi wale wenye kufanya biashara kwa njia ya riba. Na kila mwenye kula riba, kuanzia pande zote muhimu zinazo husika mawakala wake na wasaidizi wake hao wote wamelaaniwa kwenye ulimi wa Mtume Muhammad rehema na amani

ziwe juu yake. Imepokewa kutoka kwa Jaabir Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwamba;

عن جابر رضي الله عنه قال: لعن رسول الله صلى الله عليه وسلم : " أكل الربا ومؤكله وكاتبه وشاهديه .
وقال: هم سواء "

‘Amemlaani Mtume wa Mwenyezi Mungu mwenye kula riba, mwenye kuilisha, mwandishi wake na mashahidi wake wawili.’

Kisha akasema: “Hao wote ni sawa.”
(Yaani hao wote hukumu yao ni moja).
Muslim 3/219.

Kutokana na haya, basi haifai kufanya kazi ya kuandikisha riba, wala kujiandikisha, wala haifai pia kuipokea riba au kuitoa au kuidhamini na kuilinda.

Kwa ujumla ni haramu kushiriki au kusaidia chochote kinachohusiana na riba kwa vyovyyote vile itakavyokuwa.

Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake alijitahidi sana kuiweka wazi na kuibainisha dhambi hii ya aina yake kama

ilivyopokewa kutoka kwa Abdillah bin Masoud Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwenye hadithi marfuu:

"الربا ثلاثة وسبعون باباً أيسراً مثل أن ينكح الرجل أمه، وإن أرباً الربا عرض الرجل المسلم"

"Riba ni milango sabini na tatu mwelesi zaidi kuliko yote ni kama vile mtu kumuoa (kumuingilia) mama yake mzazi, na riba kubwa zaidi ni (mtu kuurefusha ulimi wake kwa) kuishambulia heshima ya ndugu yake muislamu." Al Haakim 2/37.

Na kwenye hadithi nyingine kutoka kwa Abdillahi bin Handhala Mwenyezi Mungu awe radhi nae kutoka kwenye hadithi marfuu vile vile;

"درهم ربا يأكله الرجل وهو يعلم أشد من ست وثلاثين زانية"

"Dirham moja ya riba anayokula mtu na hali ya kuwa anajua (kuwa inatokana na riba) adhabu yake ni kali mno kuliko (adhabu ya) wazinifu thalathini na sita." Imam Ahmad.

Riba ni haramu kwa kila mtu na wala sio tu kwa watu fulani kinyume na watu wengine, kama wanavyofikiria hivyo baadhi ya watu. Baadhi ya watu wanadhani kwamba riba iliyoharamishwa hapa ni ile tu anayofanya mtu tajiri kumfanyia mtu masikini. Hii sio kweli, bali uharamu wa riba unawahu watu wote bila kubagua baina ya huyuna huyu, iwe tajiri kwa tajiri au masikini kwa maskini, yote ni riba. Ni matajiri wangapi na wafanyi biashara wakubwa kupindukia waliofilisika kwa sababu ya riba?! Na uchache wa hayo yote ni kufutwa baraka ya mali japo kama itakuwa nyingi kupindukia, kama anavyosema Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa:

”الرِّبَا وَإِنْ كَثُرَ فَإِنْ عَاقِبَتْهُ تَصِيرٌ إِلَى قُلْ“

“(Mali ya) riba japo kama itakuwa nyingi kupindukia kwa hakika mwisho wake huwa ni kwenye upungufu wa mali.” Al Haakim 2/225.
Na ieleweke wazi kuwa riba sio tu maalum kwenye kiwango chake kiasi mtu akadai

kuwa riba inayokatazwa kisheria ni ile inayokuwa ya kiwango kikubwa, lakini kama itakuwa ya kiwango kidogo hapo huwa si haramu. Hii si kweli, bali yote ni haramu, iwe ya kiwango kikubwa au kidogo yote ni sawa. Na mwenye kuila atafufuliwa siku ya kiama kutoka kaburini mwake na kusimama kama yule aliyezugwa na shetani kwa kumsawaa na kuwa mbioni tu bila ya kuwa na kituo.

Lakini pamoja na uovu wa dhambi hii na ukubwa wake, lakini bado Mwenyezi Mungu amesema kuwa yeye hukubali toba ya kila yule mwenye kutubia kwake na kuacha kula riba, kisha akawafahamisha namna ya kufanya wale wenyewe kula riba. Kwa kusema:

... ﴿ وَإِنْ ثَبَثْمَ فَلَكُمْ رُؤُسُ أَمْوَالِكُمْ لَا ظَلَمُونَ وَلَا ظَلَمُونَ ﴾

“Na ikiwa mmetubu basi mtapata rasilmali zenu msidhulumu wala msidhulumiwe.”

Al Baqarah : 279.

Na huu ndio uadilifu hasa!

Ni wajibu kwa nafsi ya muislamu kujiweka mbali na kuikimbia dhambi hii kubwa, na auhisi ubaya na uovu wake, na hata wale wanaohifadhi mali zao kwenye mabenki ya riba kwa kulazimika kufanya hivyo baada ya kukosa njia nyingine ya kuhifadhi mali zao na kuchelea wizi na kupotea, wao pia wanapaswa kuhisi hisia za mtu mwenye kulazimishwa kufanya jambo kwa nguvu pamoja na kwamba nafsi yake haiko radhi. Na kuchukia kama yule mwenye kula maiti au chuki zake ziwe zaidi ya hapo, pamoja na kumtaka msamaha Mwenyezi Mungu na kujitahidi kutafuta ufumbuzi wa suala hili ili ajiepushe nalo haraka iwezekanavyo.

Na wala haifai kwao kuzidai benki faida za riba kutoka kwenye hesabu zao, bali kama itatokea kuwekewa faida za riba kwenye hesabu zao basi ni lazima waepukane nazo kwa njia yoyote ile ifaayo lakini sio kwa kuzitolea sadaka. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mzuri hakubali isipokuwa kitu

kilichokuwa kizuri. Wala haifai pia kufaidika na faida hizo za riba kwa namna yoyote ile, si kwa kula, au kunywa, au kuvaan au kujengea au kutoa kwenye matumizi ya mke na watoto, baba au mama.

Na wala haifai pia kuitolea zaka au kulipia kodi, isipokuwa atajiepusha nayo kwa ajili ya kuchelea adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

KUFICHA AIBU YA BIDHAA NA KUTOMFAHAMISHA MNUNUZI.

مرّ رسول الله ﷺ على صبرة طعام فأدخل يده فيها فنالت أصابعه بلا فقل: "ما هذا يا صاحب الطعام؟" قال أصابعه السماء يا رسول الله. قال: أفلأ جعلته فوق الطعام كي يراه الناس؟ من غشنا فليس منا"

Siku moja mtume rehema na amani ziwe juu yake alipita kwenye fungu la chakula (sokoni) akaingiza mkono wake ndani ya lile fungu la chakula na mikono yake ikapata unyevunyevu; Akasema Mtume kumwambia muuzaji: "Kitu gani hiki ewe mwenye chakula (muuzaji)?" Akajibu yule mwenye chakula kwa kusema; 'Kilinyeshewa na mvua ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Akasema Mtume: "Kwa nini basi hiki kilichonyeshewa na mvua usikiweke juu ya chakula ili watu wakapata kukiona? Mwenye kutufanyia ghishi (udanganyifu) huyo si katika sisi." Muslim 1/99.Na wauzaji wengi leo hii mionganoni mwa wale wasio kuwa na khofu kwa Mwenyezi Mungu hujaribu kuficha

aibu au ubovu wa bidhaa kwa kuweka mfuniko juu yake, au kubandika gundi, au kuweka bidhaa mbovu chini ya sanduku au chini ya gunia, au kwa kutumia baadhi ya kemikali na kadhalika ili zionekane mbele ya mnunuzi zikiwa kwenye sura nzuri na mandhari ya kuvutia, au wakati mwingine huficha sauti ya aibu ambayo ipo kwenye mashine, na mnunuzi anapoondoka na chombo huwa hakai nacho muda mrefu kabla ya kile chombo kumharibikia. Na baadhi yao hubadilisha tarehe yenyε kuonyesha uzima wa bidhaa, au humzuia mnunuzi kuikagua bidhaa kwa uangalifu au kuichunguza na kuijaribu. Na watu wenye kufanya biashara kama vile ya kuuza magari au mashine huwa hawaonyeshi kwa mnunuzi aibu au ubovu wa mashine au magari. Kitendo hiki ni haramu katika uislamu. Mtume anasema:

”المسلم أخو المسلم ولا يحل لمسلم باع من أخيه بيعا فيه عيب إلا بيته له“

Muislamu ni ndugu wa muislamu, wala si halali kwa muislamu kumuuzia ndugu yake (muislamu) kitu (bidhaa) ambacho kina aibu ndani yake, kabla ya kumbainishia aibu yake." Ibn Majah 2/754.

Baadhi ya watu hudhani yeye huondokana na kuwajibika na masuulia kama atamwambia mnunuzi kwenye minada ya hadhara kwamba ninauza vyuma kwa mafungu! Nauza vyuma kwa mafungu! Ifahamike kwamba biashara kama hii huwa imeondoshwa baraka kama anavyosema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

"البیعن بالخیار ما لم یتفرق فیان صدق و بینا بورک

لهمَا فِي بَيْعَهُمَا وَإِنْ كَذَبَا وَكُلَّمَا مَحْقَتْ بَرَكَةَ بَيْعَهُمَا"

"Wawili wenyе kuuziana huwa kwenye khiari kabla ya kuachana, na kama watakuwa wakweli na kuwekeana wazi hubarikiwa kwenye biashara yao na ikiwa wataongopeana na kufichana ukweli huondoshewa baraka ya biashara yao." Bukhariy Al-fathul Baariy 4/328.

BIASHARA YA KUPANDISHIANA BEI.

Ni kama vile mtu kuongeza bei ya bidhaa na hali hataki kuinunua ili aweze kumhadaa mnunuizi mwengine mwenye nia ya kutaka kununua bidhaa ile au aweze kuhadaika na kuvutika na kujipandishia bei ya bidhaa yeye mwenyewe. Mtume amesema:

« لا تاجشووا »

“Msipandishiane bei.” Bukhariy Fat’hul Baariy. 10/484.

Hii bila shaka ni aina ya hadaa na udanganyifu, na Mtume amesema :

« المكر والخدعه في النار »

“(Mwenye kufanya) hila (udanganyifu) na hadaa atakuwa motoni.” (Angalia silsilatil Ahaadiithi Sahihat. Hadithi no. 1057).

Na madalali wengi kwenye minada ya hadhara na maonyesho ya biashara ya magari machumo yao ni machafu kwa sababu ya mambo mengi ya haramu wanayofanya, kwa kule kutangaza kwao

biashara ya kuzidishiana bei, na kumlaghai na kumrubuni mnunuzi au muuzaji mwenye kuja na bidhaa yake na kumhadaa kwa kutangaza kushusha bei ya bidhaa yake. Lau kama bidhaa ile ingekuwa ya kwao au ya mmoja wao basi ingekuwa kinyume cha hapo. Na huwakanganya wanunuzi na kuwapandishia bei kwenye minada na kuwa hadaa waja wa Mwenyezi Mungu na kuwadhuru.

KUENDELEA KUFANYA BIASHARA
BAADA YA ADHANA YA PILI SIKU YA
IJUMAA.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا ثُوِّدَتِ الصَّلَاةُ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ
 فَاسْتَعِوْدُوا إِلَى ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ
 تَعْلَمُونَ ﴾

“Enyi mliaoamini, kukiadhiniwa kwa ajili ya siku ya Ijumaa, nendeni upesi kumtaja Mwenyezi Mungu na acheni biashara, kufanya hivi ni bora kwenu ikiwa mnajua.”

Al Jumua : 9

Baadhi ya wauzaji huendelea kufanya biashara zao kwenye maduka yao au mbele ya misikiti hata baada ya kuadhiniwa adhana ya pili, na watu hawa hushirikiana dhambi na wale wenye kununua kutoka kwao japo kama kinachonunuliwa kitakuwa ni mswaki, kwa sababu biashara kipindi hiki huwa ni haramu. Na baadhi ya watu wenye

mahoteli, mabekari ya kuokea mikate na viwanda huwalazimisha kwa nguvu wafanyikazi wao kuendelea kufanya kazi wakati wa sala ya Ijumaa. Watu hawa hata kama kwa nje wataonekana kupata faida kubwa kibiashara lakini kwa hakika faida yao huwa haiwazidishii lolote isipokuwa ni hasara, ama mfanyakazi, yeye hanabudi isipokuwa kufuata kauli ya Mtume isemayo:

”لا طاعة لبشر في معصية الخالق“

“Hakuna twaa kwa kiumbe katika kumuasi muumbaji.” Ahmad 1/129.

KAMARI.

Amesema Mwenyezi Mungu:

» إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَنِيرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَرْلَامُ رِجْسٌ مَّنْ
عَمِلَ الشَّيْطَانَ فَاجْتَبَوْهُ لَعَلَّكُمْ تَقْلِبُونَ «

“Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kutazamia kwa mishare ya kupigia ramli ni uchafu (ni) katika kazi za shetani, basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu.” Al-Maida : 90.

■ Watu wa zama za jaahiliya walikuwa wakicheza kamari, na kamari iliyokuwa mashuhuri wakati huo, ni kuwa walikuwa watu kumi wakishirikiana kwenye ngamia mmoja, kwa kugawana mafungu sawa sawa, kisha hupigwa mshale (aina fulani ya kura) kisha watu saba huchukua fungu maalum lenye kutofautiana kulingana na mazoea yao, na watu watatu waliobaki hawachuku kitu. chochote. Ama kamari kwenye zama zetu za leo ina sura tofauti -

kama vile bahati nasibu- nayo ina sura
 nyingi tofauti; na iliy
 maarufu zaidi ni;

- 1) kununua namba kwa pesa, kisha wakati wa kuichezesha huvutwa namba moja, yule ambaye namba yake ndio itakayotoka mwanzo ndie hutangazwa kuwa mshindi wa kwanza na kupata zawadi ya mshindi wa kwanza na mshindi wa pili na kadhalika zawadi nyingine tofauti. Na mchezo huu ni haramu kabisa japo kama watauita kwa majina ya kheri.
- 2) kununua bidhaa bila kufahamu kilichomo ndani yake au kupewa namba wakati wa kununua bidhaa fulani kisha ikachezesewa bahati nasibu na kupata washindi wa zawadi.
- 3) miongoni mwa kamari za zama zetu pia mikataba ya bima ya biashara, bima ya maisha, bima ya usafiri, bima ya bidhaa dhidi ya moto, na aina nyingine za bima na kitu cha kushangaza zaidi utaona mpaka

waimbaji wa muziki nao wana bima ya sauti zao!

Hii pamoja na sura nyingine za kamari ambazo zote kwa pamoja huingia kwenye hukumu ya kamari.

Leo hii utaona kuna vilabu maalumu vyatia kuchezeshea kamari na ndani kuna meza zinazoitwa “meza za kijani” ambazo ni maalum kwa kufanyia maasi haya yaliyo makubwa.

Na vile vile kuwekeana dau kwenye mashindano kama vile mashindano ya mpira wa miguu na yenyewe kufanana na hayo. Hii vile vile ni katika aina ya kamari nayo pia ni haramu.

Ama mashindano yapo kwenye aina tatu tofauti:-

1. **Mashindano ambayo ndani yake kuna malengo ya kisheria na makusudio ya dini, mashindano kama haya yanaruhusiwa kuwekewa zawadi kwa washindi, au kutowekewa zawadi. Kama vile mashindano ya mbio za farasi, na ngamia kutupa**

mishale na kulenga shabaha, pia yanaingia kwenye hukumu ya mashindano haya mashindano ya kuhifadhishe Qurani kwa kauli yenyе kutegemewa na wanazuoni wengi.

2. mashindano ambayo kwenye nafsi yake ni halali. Kama vile mashindano ya mpira wa miguu, na mashindano ya mbio (riadha) yanapokuwa yanafanyika bila ya kuambatana na mambo ya haramu ndani yake, kama vile kupoteza sala, na kutembea uchi, mashindano kama haya yanajuzu bila kuwapo zawadi kwa washindi.
3. Mashindano ambayo ni haramu kwenye nafsi yake au yanapelekea kwenye mambo ya haramu kama vile mashindano ya ufisadi yanayoitwa mashindano ya kumtafuta malkia wa urembo ulimwenguni, au mashindano ya ngumi yenyе kuambatana na makonde ya uso, mashindano kama haya ni haramu. Au mashindano ya kupiganisha

kondoo au majogoo na mfano wa haya pia yanaingia kwenye hukumu ya haramu.

WIZI.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقةُ فَاقْطِعُوهُمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبُوا
نَكَالًا مَنْ أَنْهَى اللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾

“Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke ikateni mikono yao, malipo ya yale waliyochuma, ndiyo adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na mwenye hikima.” Al Maida : 38

Na wizi wenyewe uovu mkubwa kabisa ni kuwaibia mahujaji na watu wenyewe kuzuru nyumba ya Mwenyezi Mungu. Aina hii ya wizi haina mfano wake kwenye mipaka ya Mwenyezi Mungu hasa inapokuwa uovu huu unafanywa kwenye viwanja bora kabisa ulimwenguni, na mbele ya nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na Mtume  anasema kwenye kisa cha sala ya kupatwa kwa jua:

”لَقَدْ جَاءَ بِالنَّارِ وَذَلِكَ حِينَ رَأَيْتُمُونِي تَأْخِرُتْ مَخَافَةً
أَنْ يُصِيبَنِي مِنْ لَفْحَهَا، وَهَذِهِ رَأْيَتْ فِيهَا صَاحِبَ
الْمَحْجُنِ يَجْرِيْ قَصْبَهُ [أَمْعَاءَهُ] فِي النَّارِ، كَانَ يَسْرِقُ
الْحَاجَ بِمَحْجُنِهِ، فَبَلَى فَطَنَ لَهُ قَالَ: إِنَّمَا تَعْلَقُ بِمَحْجُنِي،
وَإِنْ غَفَلَ عَنِهِ ذَهَبَ بِهِ“

“Uliletwa moto mbele yangu na hii ni pale
mliponiona nikirudi nyuma kwa kuchelea
nisije nikaunguzwa, ndipo nilipomuona mtu
mwenye mihjani¹ akiwa ndani ya moto huo
akiyaburuza matumbo yake kwenye moto,
(mtu huyu) alikuwa akiwaibia mahujaji
kwa kutumia hiyo mihjani yake.
Wanapomgundua husema ilinasa (kwa
bahati mbaya) kwenya mihjani yangu na
anapopuuzwa huondoka nazo (mali za
watu).”Muslim na. 904.

Na katika wizi mkubwa vile vile
kuiba mali za umma. Baadhi ya watu wenye

¹ Fimbo ndefu iliyopindika mwishoni. (crooked)

kufanya kitendo hiki husema tunaiba kama wanavyoiba wenzetu, wala hawajui kuwa wizi huu ni sawa na kuwaibia waislamu wote, kwa sababu mali ya umma ni mali ya waislamu wote, na kitendo cha wale wasiomuogopa Mola wao sio hoja ya kukufanya wewe uwaige na kuiba mali ya umma.

Baadhi ya watu huiba mali ya makafiri kwa hoja kwamba hawa ni makafiri. Kitendo hiki sio sahihi, kwa sababu makafiri walioruhusiwa kuchukuliwa mali zao ni wale wenyewe kuwapiga vita waislamu peke yake, na hii haihusu mashirika yao na mtu mmoja mmoja binafsi.

Na katika njia ya wizi vile vile kuiba mali za watu kwa siri. Baadhi ya watu huingia kwenye nyumba za watu wengine kama wageni na kuiba. Na wengine huiba kwenye mifuko ya wageni wao, na wengine huingia kwenye sehemu za biashara kama vile (supermarket)na kuficha bidhaa

kwenye mifuko yao au kwenye nguo zao. Au kama vile wanavyofanya baadhi ya wanawake ya kuficha vitu chini ya nguo zao. Na baadhi ya watu hupuuzia na kuiba vitu vidogo vidogo au vitu rahisi, na hali ya kuwa Mtume amesema:

”لَعْنَ اللَّهِ السَّارِقِ يُسْرِقُ بِيَضْنَةٍ فَتَقْطَعُ يَدَهُ وَيُسْرِقُ
الْحَبْلَ فَتَقْطَعُ يَدَهُ“

”Mwenyezi Mungu amemlaani yule mwenye kuiba yai na akakatwa mkono wake na mwenye kuiba kamba akakatwa mkono wake.” Bukhariy Fat'hul Baariy 12/18.

Ni wajibu wa kila mwenye kuiba chochote kukirejesha kwa mwenyewe baada ya kutubia kwa Mola wake. Sawa akirejeshe kwa wazi au kwa siri, au kwa kwenda yeye mwenyewe binafsi au kwa kumtumia mtu mwengine. Ikiwa atashindwa kufika kwa mwenye mali au kwa warithi wake baada ya kufa mwenye mali pamoja na kujitahidi kutafuta basi

**atatoa sadaka na kunuia thawabu zimfikie
mwenye mali.**

KUPOKEA NA KUTOA RUSHWA .

Kutoa rushwa kwa hakimu au kadhi kwa lengo la kubatilisha haki, au kuuficha ukweli na kuunyamazia, ni uovu mkubwa kwa sababu hupelekea kupatikana udhalimu kwenye hukumu na kumdhulamu mwenye haki na hatimae kuenea ufisadi kwenye jamii. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْتَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتَدْلُوا بِهَا إِلَى الْحُكَمِ لِتَأْكُلُوا فِرِيقًا مَّنْ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴾

“Wala msiliane mali zenu kwa batili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpare kula sehemu ya mali za watu kwa dhambi na hali mnajua.” Al Baqara : 188.

Imepokewa kwa Abi Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwenye hadithi marfuu:

«لعن الله الراشي والمرتشي في الحكم»

“Amemlaani Mwenyezi Mungu mwenye kula rushwa na mwenye kutoa rushwa

kwenye hukumu.” Ahmad 2/387 Sahihi Jamii Hadith No. 5069.

Ama rushwa inayotolewa kwa lengo la kutafuta haki au kuzuia dhuluma, ambapo haiwezekani kupata haki au kuzuia dhuluma isipokuwa kwa kutoa rushwa; rushwa hii haiingii kwenye hukumu ya adhabu.

Hivi leo rushwa imeenea kwenye jamii yetu kwa kiwango cha kutisha kiasi kwamba imefikia rushwa kuwa ndio njia ya kupatia mali kwa wafanyakazi wa vyeo mbali mbali. Sio hivyo tu, bali imefikia kuwa ni kifungu kimojawapo cha bajeti ya mashirika mengi. Imekuwa shughuli nyingi haziwezi zikaanza kufanyika au kwisha isipokuwa kwa kutoa rushwa, na matokeo yake wale mafakiri wanyoge ndio wenyewe kuathirika vikali na madhara yake. Na kuharibu uaminifu wa watu wengi kwa sababu yake, na pia kuwa ni sababu ya kuharibika wafanyakazi wengi kwa waajiri wao. Imekuwa huduma bora hazitolewi isipokuwa kwa yule mwenye

kutoa rushwa, na yule asietoa rushwa hupewa huduma hafifu na mbaya, au hucheleweshwa na kupuuzwa kabisa, na watu wenye rushwa waliokuja nyuma yake hushughulikiwa na kuondoka mapema na kubakishwa yeye hali ya kuwa ndie aliyekuja mwanzo kabla yao.

Na kutokana na rushwa imesababisha mali nyingi wanazostahiki waajiri na mashirika ya umma kuingia kwenye mifuko ya mawakala wa mauzo na ununuzi wa mashirika haya kwa dhuluma. Na kwa sababu hizi na nyinginezo si jambo la ajabu kwa Mtume kuwaombea laana na kufukuzwa kwenye rehema za Mwenyezi Mungu wale wote wanaoshiriki kwenye uovu huu. Imepokewa kutoka kwa Abdillah bin Amruu Mwenyezi Mungu awe radhi nae yeye na baba yake akisema, amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa:

«لغة الله على الراشي والمرتشي»

**“Laana ya Mwenyezi Mungu iwe kwa mla
rushwa na mtoa rushwa.” Ibin Maajah No.
2313 - Sahihul Jamii : 5114.**

KUPORA ARDHI;

Khofu inapokosekana kwa mtu, na ucha Mungu, hila na nguvu huwa ni balaa kwa mwenye nazo, hutumia hila na nguvu hizo kwa dhuluma na kupora mali za watu wengine. Na mionganini mwa dhuluma hizo ni kupora ardhi za watu. Na adhabu za uovu huu ni kali kupita kiasi.

Imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Omar kwenye hadithi marfuu akisema ;

"من أخذ من الأرض شيئاً بغير حقه خسف به يوم القيمة إلى سبع أرضين"

"Mwenye kuchukua chochote kwenye ardhi bila ya kuwa na haki nayo atadidimizwa nayo siku ya kiama mpaka kwenye ardhi ya saba." Bukhariy - Fat'hul Baariy 1/103.

Na imepokewa kutoka kwa Yaala bin Murrat Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwenye hadithi marfuu vile vile akisema:

"أيما رجل ظلم شبراً من الأرض كلفه الله أن يحفره (في الطبراني: يحضره) حتى آخر سبع أرضين ثم يطوقه يوم القيمة حتى يقضى بين الناس"

“Mtu yoyote aliyedhulumu shibri moja ya ardhi Mwenyezi Mungu atamlazimisha aichimbe (kwenye mapokezi ya tabraaniy imekuja ‘Mwenyezi Mungu atamlazimisha ailete’) mpaka mwisho wa ardhi ya saba. Kisha amvishe nayo shingoni siku ya kiama (akae nayo hivyo) mpaka atakapomaliza Mwenyezi Mungu kuhukumu baina ya watu.” Tabraniy 22/270 Sahihil Jaamiy 2719.

Na inaingia kwenye hukumu ya hadithi hizi pia kubadilisha alama na mipaka ya ardhi , ikawa mtu anabadilisha ardhi yake na kumdhulumu jirani yake. Na hali hii ndio aliyoashiria Mtume kwa kusema:

”لَعْنَ اللَّهِ مَنْ غَيَّرَ مِنَارَ الْأَرْضِ“

“Mwenyezi Mungu amemlaani mwenye kubadilisha mipaka ya ardhi.” Muslim Sharh Nnawawiy 13/141.

KUKUBALI ZAWADI KWA SABABU YA KUWATETEA WATU.

Kuwa na cheo kitukufu na kuheshimiwa na kukubalika mbele za watu ni mionganini mwa neema kubwa za Mwenyezi Mungu anazompa mja wake pindi anaposhukuru kwa kuruzukiwa neema hiyo. Na mionganini mwa njia za kushukuru neema hii ni kuitumia kwa kuwanufaisha waislamu, na hii inaingia kwa jumla kwenye kauli ya Mtume ﷺ:

”من استطاع منكم أن ينفع أخيه فليفعل“
 “Mwenye kuweza mionganini mwenu kumnufaisha (kumsaidia) ndugu yake basi na afanye hivyo.” Muslim 4/1726.

Na mwenye kutumia cheo chake kwa kumsaidia ndugu yake muislamu kwa kuzuia dhuluma dhidi yake, au kumsaidia kwenye jambo la kheri bila ya kufanya mambo yaliyoharamishwa au kufanya uadui kwenye haki basi ajue kuwa atalipwa ujira wake mbele ya Mwenyezi Mungu

Mtukufu pindi atakapofanya kitendo hiki kwa nia safi ya kutaka ujira na thawabu kwa Mwenyezi Mungu, kama alivyosema **Mtume** ﷺ:

«أشفوا تؤجروا»

“Wasaidieni (wanufaisheni wenzenu) mtalipwa (na Mwenyezi Mungu).” Abu Daud No. 5132 - Fat’hul Baariy 10/450.

Wakati wa kumsaidia mtu kwa kumtetea, kumuombea au kuwa mtu wa kati kati baina yake na mtu mwingine haifai kuchukua kitu chochote kama malipo kwa kazi yako. Na dalili ya hayo ni hadithi ya Abi Umama Mwenyezi Mungu awe radhi nae:

” من شفع لأحد شفاعة، فأهدي له هدية (عليها) فقبلها (منه) فقد أتى بباباً عظيماً من أبواب الربا ”

“Mwenye kumsaidia yejote kwenye utetezi akapewa zawadi juu ya kitendo hiki nae akaikubali (zawadi hiyo) basi atakuwa ameuingia mlango mkubwa kabisa katika

milango ya riba.” Ahmad 5/261 - Sahihil Jaamiy 6291.

Kuna mionganini mwa watu hujitolea kutumia cheo chake na uwezo wake kwa kumtaka yule mwenye kumsaidia atoe kitu chochote ili aweze kumpandisha cheo, au kumhamisha kutoka idara fulani kwenda idara nyingine, au kumhamisha kutoka mkoa fulani kwenda mkoa mwingine, au kumtibu mgonjwa na mfano wa haya.

Na ukweli hasa ujira huu anaotaka ni haramu kwa ushahidi wa hadithi ya Abi Umama iliyopita hivi punde. Si hayo tu bali dhahiri ya hadithi inaharamisha kuchukua zawadi japo kama bila hata kutanguliza sharti. Mwenye kufanya wema na kheri yanamtosha malipo ya Mwenyezi Mungu atakayoyakuta siku ya kiama.

Siku moja alikuja mtu mmoja kwa Al Hassan bin Sahli akimuomba amsaidie kwenye matatizo aliyokuwa nayo, na Al Hassan bin Sahli akafanya hivyo, baada ya kusaidiwa akageuka yule mtu kumshukuru

Al-Hassan kwa wema na msaada wake aliomfanyia. Al-Hassan bin Sahli akamwambia yule mtu, unatushukuru kwa jambo gani kubwa tulilolifanya? sisi tunaona kuwa cheo kitukufu kinastahili kutolewa zaka kama vile mali inavyostahili kutolewa zaka.” Adabu sharia Ibin Muflih 2/176.

Hapa inafaa ifahamike kuwa kuna tofauti baina ya kumuajiri mtu kutekeleza jambo fulani na kumpa ujira wake baada ya kutekeleza umuhimu wake na baina ya mtu kutumia cheo chake na uwezo wake wa kuwa mtu wa kati kati na kumsaidia mtu kwa malipo fulani, hii imeharamishwa kisheria.

KUMUAJIRI MTU KWA KAZI FULANI
KISHA UKAKATAA KUMLIPA UJIRA WA
KAZI.

Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akipenda sana kumlipa muajiriwa ujira wake kwa haraka iwezekanavyo. Amesema rehema na amani ziwe juu yake:

"اعطوا الأجير حقه قبل أن يجف عرقه"

"Mpeni muajiriwa haki yake kabla halijakauka jasho lake. " Ibin Maajah 2/817. Sahihil Jaamii Hadithi No. 1493.

Miongoni mwa aina za dhuluma zinazopatikana kwenye jamii za kiislamu ni kutowapa waajiriwa na vibaruwa na wafanyakazi wa maofisini malipo yao wanayostahiki kwa wakati unaostahiki, na dhuluma hii ipo kwenye sura tofauti:-

■/kukana muajiri kuwa mfanyakazi wake hana haki zozote na mfanyakazi kukosa ushahidi wa kuthibitisha haki yake kwa muajiri. Hii hata kama itapotea haki yake

hana duniani, lakini katu haki yake haitaweza kupotea mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya kiama. Siku hiyo dhalimu atakuja akiwa amekula mali ya mdhulumiwa hapo mdhulumiwa atapewa mema ya dhalimu, baada ya Mwenyezi Mungu kumnyang'anya mema yake. Kama mema yake yatakwisha na ikawa bado anadaiwa, basi yatachukuliwa madhambi ya mwenye kudhulumiwa na kutupiwa dhalimu kisha atupwe motoni.

■ **Kuwapunja wafanyakazi mishahara yao na kutowapa kwa ukamilifu au kuipunguza bila ya kuwa na haki yoyote, na Mwenyezi Mungu anasema:**

﴿ وَيَلِلِّلَّمَطْقَفِينَ ﴾

“Maangamizo yatawathubutikia wapunjao (wenzi wao).” Al Mutaffifin : 1. Na mionganini mwa mifano ya dhuluma hii ni kama vile kitendo cha baadhi ya waajiri wanapokuwa wanachukua wafanyakazi kutoka nje,

huwekeana nao mikataba ya kuwalipa
 kiwango fulani cha mshahara kwa mwezi,
 wanapofunga mkataba na kuanza kazi,
 waajiri hawa hubadilisha mikataba hiyo na
 kuwapa mishahara ya kiwango cha chini
 tofauti na ile walioandikiana na
 kukubaliana kwenye mkataba uliopita, na
 kusababisha hawa wafanya kazi kufanya
 kazi kwa kinyongo, chuki na ghadhabu, na
 wakati mwingine wafanyakazi hushindwa
 kuthibitisha haki zao kwa kutokuwa na
 ushahidi wa kutosha, na kumshitakia
 Mwenyezi Mungu dhuluma hii. Hata kama
 itakuwa muajiri dhalimu ni muislamu na
 anaedhulumiwa ni mfanyakazi kafiri bado
 itakuwa kupunja huku ni kuzuia kwenye
 njia ya Mwenyezi Mungu na atastahili
 madhambi yake.

Kuwaongeza muda wa ziada wa kufanya
 kazi (overtime) au kurefusha muda wa
 zamu na kumpa mshahara wake wa
 kawaida na kumnyima mshahara wa kazi
 ya ziada (overtime).

■ Kukawiza mishahara yao, hawalipi isipokuwa baada ya kutoa juhudi kubwa na kushitakiana na kupelekana mahakamani. Wakati mwingine huwa lengo la muajiri kumcheleweshea mfanyakazi mshahara wake ni kumfanya achoke na kukata tamaa na kuacha haki na kuamua kutoifuutilia. Au wakati mwingine hukusudia kufaidika na mishahara ya wafanyakazi kwa kuifanyia kazi nyingine, au kuingiza kwenye riba, na kumuacha mfanyakazi akiwa masikini kiasi cha kushindwa hata kupata chakula cha siku moja, au kushindwa kupata chochote cha kutuma kwa familia yake, mke wake na watoto wake, wenye matatizo ambao amesafiri na kujitenga nao mbali kwa ajili yao.

Ole wao waajiri hawa madhalimu na adhabu ya Mwenyezi Mungu siku ya kiama!

**Imepokewa kutoka kwa Abi Huraira
Mwenyezi Mungu awe radhi nae kutoka
kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake
akisema, amesema Mwenyezi Mungu :**

قال تعالى: "ثلاثة أنا خصمهم يوم القيمة رجل أعطى
ببي ثم غدر، ورجل باع حررا وأكل ثمنه، ورجل استأجر
أجيرًا فاستوفى منه ولم يعطه أجره"

**"Watu watatu mimi nitakuwa mgomvi wao
siku ya kiama; mtu aliyetoa kiapo chake
kwa jina langu kisha akakhini¹, na mtu
aliyemuuza muungwana kisha akala
thamani yake, na mtu aliyemuajiri
mfanyakazi akamfanyia kazi yake kisha
asimpe ujira wake.²" Bukhariy - Fat'hul
Baariy 4/447.**

¹ Yaani mtu aliyechukua ahadi na akaapa kwa jina la
Mwenyezi Mungu, kisha akavunja ahadi yake
asiitekeleze.

² Yaani akakataa kumpa malipo ya kazi yake
anayostahili.

MZAZI KUTOFANYA UADILIFU WA MATUMIZI KWA WATOTO WAKE.

Baadhi ya watu kwa kusudi kabisa huamua kuwabagua watoto wao na kuwapenda zaidi watoto fulani na kuwapa zawadi na misaada mbali mbali kinyume na watoto wengine. Kitendo hiki kwa ukweli hasa ni kitendo cha haramu katika uislamu ikiwa mtu atakifanya bila ya kuwa na matatizo na ruhusa ya kisheria, kama vile mmoja wa watoto kuwa na matatizo kama vile ya ugonjwa au deni n.k. ambayo watoto wengine hawanayo au kumpa zawadi kwa kuhifadhi Qur'ani kwa mfano, au hawezikufanya kazi, au kuwa ana familia kubwa kuliko wengine au mwanafunzi mwenye kutumia wakati wake wote kwenye elimu, na mfano wa hayo.

Kwa hiyo ni wajibu kwa mzazi kunuia ndani ya nafsi yake wakati anapokuwa anatoa chochote kumpa mmoja wa watoto wake kwa sababu ya kisheria

kwamba, lau kama mtoto mwingine atakuwa na matatizo kama hayo aliyokuwa nayo huyo aliyempa, basi atampa zawadi kama anavyompa huyu wa kwanza.

Na dalili kwa ujumla ni kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

«اعدلو هو أقرب للتفوى واتقوا الله» ...

“Fanyeni uadilifu; huko ndiko kunakomkurubisha mtu na ucha mungu, na mcheni Mwengezi Mungu.” Al Maidah: 8.

Ama dalili khasa ni ile iliyokuja kutoka kwa An-numan bin Bashir Mwenyezi Mungu awe radhi nae kuwa baba yake alikwenda kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kumuambia;

عن النعمان بن بشير رضي الله عنهمما أن أباه أتى به إلى رسول الله صلى الله عليه وسلم فقال: «إني نحلت ابني هذا غلاماً، فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم: «أكل ولدك نحلته مثله؟» فقال: لا، فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم فأرجعه، وفي رواية فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم: فاتقوا الله واعدلو بين

أولادكم » قال: فرجع فرد عطيته، وفي رواية: « فلا تشهدني إذن فانني لا أشهد على حور »

“Mimi nimempa huyu mwanangu zawadi ya mtumwa, akasema Mtume ﷺ: “Je na watoto wako wote umewapa zawadi kama hii?” Akajibu: la. Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: basi mrudishe. Na kwenye mapokezi mengine akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: “Muogopeni Mwenyezi Mungu na fanyeni uadilifu kati ya watoto wenu.” Fat’hul Baariy. Akasema, akarejea kisha akarudisha zawadi yake. Fat-Hul Baariy 5/211. Na kwenye mapokezi mengine, akasema Mtume: “kwa hiyo basi usinishuhudishe mimi, kwa sababu mimi sishuhudii udhalimu.” Sahihi Muslim 3/1243.

Na mtoto wa kiume hupewa mafungu ya wanawake wawili kama kwenye mirathi na hii ni kauli ya Imam Ahmad. (Rejea Masailil Imam Ahmad Liabii Daud uk. 204).

Leo hii ukiangalia kwenye hali ya baadhi ya familia utaona baadhi ya wazazi

wasiomuogopa Mwenyezi Mungu jinsi wanavyofanya ubaguzi wa wazi wazi kwa watoto wao, na kuwapenda baadhi na kuwapa zawadi kemkem na kuwabagua wengine na kuwanyima zawadi. Hali hii husababisha watoto wa familia moja kuchukiana wao kwa wao na hatimae kupandikiza chuki, husuda na bughudha kubwa na kukosekana mapenzi na huruma kati yao. Utaona mzazi akimpa mmoja wa watoto wake zawadi eti kwa sababu amefanana na baba zake wadogo, (ma Ami zake) au utaona akiwapa watoto wa mmoja wa wake zake vitu tofauti na vile anavyotoa kuwapa watoto wa mke mwingine. Wakati mwingine utaona akiwaingiza watoto wa mmoja wa wake zake kwenye shule khasa tofauti na wengine. Hii husababisha mtoto kuja kumuasi mzazi wake baadae, kwa sababu yule mwenye kunyimwa mara nyingi hutokea kutomfanyia wema baba yake hapo baadae. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema kwa yule

mwenye kufanya ubaguzi kati ya watoto wake kuwa:

"أَلَيْسَ يَسِّرُكُ أَنْ يَكُونُوا إِلَيْكُ فِي الْبَرِّ سَوَاءً"

"Je haikufurahishi itakapokuwa wote wakikufanyia wema kwa sawa sawa?"
Imam Ahmad 4/269 - Sahihi Muslim.
Hadithi No. 1623.

KUWAOMBA WATU BILA YA KUWA NA MATATIZO.

Imepokewa kutoka kwa Sahli bin Handhalat Mwenyezi Mungu awe radhi nae akisema, amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwamba:

” من سأّل الناس وعندّه ما يقّيه فإنّما يسْتَكثِرُ من جرْ جهنّم، قالوا وما الغُى الذِّي لَا تَنْبَغِي مَعَهُ الْمَسَأَةُ؟ قَالَ قَدْرٌ مَا يَغْدِيهُ وَيَعْشِيهُ ”

“Mwenye kuomba na hali ya kuwa nae ana kitu cha kumtosheleza bila shaka mtu huyo atakuwa anajiongeza mkaa wa moto wa jahanam.” Wakasema (maswahaba) kiasi gani cha utajiri ambacho hakifai kwa mtu kuomba? Akasema Mtume: (awe na utajiri wa) “Kiasi cha kumtosheleza kula yake ya mchana na usiku.” Abu Daud 2/281. Sahihil Jaamiy 6280.

Na imepokewa kutoka kwa Ibin Masoud Mwenyezi Mungu awe radhi nae, amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

"من سأله ما يغطيه جاءت يوم القيمة خوشا أو
كدوشا في وجهه"

"Mwenye kuomba na hali ya kuwa nae ana kitu cha kumtosheleza atakuja siku ya kiama hali ya kuwa amechanjwa chanjwa usoni." Imamu Ahmad. 1/388. Sahihi Jaamiy 6255.

Baadhi ya omba omba (wenye kuomba) utawaona wakisimama misikitini mbele ya waja wa Mwenyezi Mungu na kuwakatisha tasbihi zao kwa maombi yao, na baadhi yao hutumia uongo na uzushi wa visa vy aina mbali mbali vy uongo. Na omba omba (wenye kuomba) wengine huwasambaza watoto wao kwenye misikiti mbali mbali wakisha kukusanya kwenye misikiti hiyo huhamia kwenye misikiti mingine. Na hali ya kuwa wao wako kwenye hali ya utajiri na hakuna anaejua hali ya utajiri wao isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na wanapokufa ndipo unapodhahirika utajiri wao kutokana na mali wanazoziacha.

Na wengine huwa na matatizo ya kweli lakini yule asiyewajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri wakubwa kwa sababu ya kujizuia kwao na kuomba. Utawafahamu kuwa ni wahitaji kwa alama zao zinazoonyesha ufakiri lakini hawaombi watu. Na wala hakuna anaewajua na kuwapa sadaka.

MWENYE KUKOPA KISHA AKAKATAA KULIPA DENI.

Haki za waja mbele ya Mwenyezi Mungu zina madhara makubwa. Mtu anaweza akajikwamua na haki za Mwenyezi Mungu kwa kuleta toba, lakini haki za waja hazina budi kulipwa kabla ya kuja ile siku ambayo mtu hatokuwa tena na uwezo wa kulipa deni la mtu kwa dinari au dirham au shilingi, lakini atalilipa kwa mema au maovu yake. Na Mwenyezi Mungu anasema:

﴿إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤْدُوا الْأَمَانَاتَ إِلَى أَهْلِهَا﴾ ...

“Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe.”

Annisaa : 58.

Na mionganini mwa mambo yalioenea kwenye jamii yetu hivi sasa ni kulichukulia kwa upole suala la kukopa, baadhi ya watu huamua kukopa bila ya kuwa na matatizo makubwa isipokuwa tu huamua kukopa

kwa ajili ya kupenda starehe za kidunia na kushindana na watu wengine kwenye mapambo ya majumbani na mfano wa starehe kama hizi za kilimwengu ambazo ni zenye kupita kwa haraka.

Na mara nyingi huingia kwenye matatizo ya kunadisha mali zao ili kufidia madeni, ambapo mara nyingi huwa na shub-ha au uharamu ndani yake.

Kufanya dharau na madeni ya watu mara nyingi humuongoza mtu kwenye kusitasita kulipa madeni haya, na hatimae kupelekea kupotea mali za watu au kuharibika. Amesema Mtume akihadharisha mwisho mbaya wa kitendo hiki kuwa:

**"من أخذ أموال الناس يريد أداءها أدى الله عنه،
ومن أخذ يريد إتلافها أتلفه الله"**

"Mwenye kukopa (kuchukua) mali za watu (kwa lengo la) kutaka kuzilipa (baada ya kumaliza haja yake) Mwenyezi Mungu humlipia (humsaidia kuzilipa) na mwenye kukopa (kuchukua) mali za watu kwa ajili ya kutaka kuziangamiza Mwenyezi Mungu

humuangamiza yeye" Bukhariy Fat-hul Baariy 5/54.

Na watu wengi huyachukua masuala ya deni kijuu juu na kuyadharau kwa kudhani kwamba ni masuala mepesi hali ya kuwa masuala haya mbele ya Mwenyezi Mungu ni masuala mazito. Bali hata yule shahidi (aliyekufa kwenye njia ya Mwenyezi Mungu) pamoja na kuwa na daraja kubwa, cheo kikubwa na malipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu hatosalimika kama atakuwa na mabaki ya deni. Na dalili ya hayo ni kauli ya Mtume isemayo:

"سبحان الله ماذا أنزل الله من التشديد في الدين
والذي نفسي بيده لو أن رجلا قتل في سبيل الله، ثم
أحيي ثم قتل، ثم أحيي ثم قتل وعليه دين ما دخل الجنة
حتى يقضى عنه دينه"

"Ametakasika Mwenyezi Mungu! Kitu gani hiki kigumu alichokiteremsha Mwenyezi Mungu kwenye dini! Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake, lau kama mtu atauawa kwenye njia ya Mwenyezi Mungu, kisha akahuishwa kisha

akauawa tena, kisha akahuishwa kisha akauawa tena nae akawa ana deni (la mtu), basi asingeingia peponi mtu yule mpaka alipiwe deni lake." Annasaai 7/314.

Je baada ya maonyo makali kama haya basi hawazingatii watu hawa wenye kudharau madeni na kuyachukulia kwa wepesi na hali ya kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu ni masuala mazito?

KULA HARAMU.

Asiyemuogopa Mwenyezi Mungu huwa hajali wapi alikochuma mali yake, na ameitoa kwenye kitu gani au njia gani, isipokuwa hima yake kubwa huwa ni kuongeza pato lake japo kama litakuwa kwa njia ya haramu. Iwe ni kwa njia ya wizi, rushwa kupora au kughushi au kufanya biashara ya haramu au riba au mali ya yatima au malipo ya kazi ya haramu, kama vile kupiga bao, zinaa, kuiba au kuifanyia uadui nyumba ya mali ya waislamu (bait-ul maal), au mali za umma au kuchukua mali za watu wengine kwa kuomba ombo, au kuomba bila ya kuwa na matatizo makubwa. Na mfano wa haya; kisha hula kwa kutumia mali hizi za haramu na kuvaan na kupanda vipando viliviyotokana na mali hizi au kujenga au kuajiri, au kupamba nyumba yake kwa

mali hizi na kula haramu. Na mtume rehema na amani ziwe juu yake anasema:

"كل لحم نبت من سحت فالنار أولى به"

"Kila kipande cha nyama kilichomea kutoka kwenye haramu basi moto ni bora kwake." Tabraaniy 19/136; Sahihil Jaamiy 4495.

Na atakuja kuulizwa siku ya kiama kuhusu mali yake wapi alikoichuma au aliitoa kwenye njia zipi, na hapo ndipo kutakapokuwa na maangamizi na khasara na majuto. Basi yule aliyesaliwa na mabaki ya mali ya haramu na afanye haraka haraka kuepukana nayo sasa hivi. Ikiwa ni mali iliyokuwa haki ya binaadamu mwenzie basi afanye haraka kuirejesha kwa mwenyewe pamoja na kuomba msamaha kabla haijamfikia siku ambayo hatoweza kulipa kwa dinari au dirham au shilingi isipokuwa kwa mema au maovu.

KUNYWA POMBE JAPO KAMA TONE MOJA.

Mwenyezi Mungu amesema:

﴿ إنما الخمر والميسر والأنصاب والأزلام رجس من عمل الشيطان فاجتنبوه لعلكم تفلحون ﴾ ..

“Enyi mlolioamini! Bila shaka ulevi na kamari, na kuabudiwa (na kuombwa) asiye kuwa Mwenyezi Mungu na kutazamia kwa mishale ya kupiga ramli (na kwa vinginevyo) yote haya ni uchafu (ni) katika kazi ya shetani, basi jiepusheni navyo ili mpate kufaulu.” Al Maidah : 90.

Na amri ya kujiepusha ni dalili yenye nguvu zaidi kuliko kuharamisha, na Mwenyezi Mungu amefananisha pombe na “answabu” ambayo ni Miungu ya makafiri na masanamu yao, kwa hiyo hakuna hoja tena kwa yule mwenye kusema kuwa Mwenyezi Mungu hakusema pombe ni haramu isipokuwa amesema jiepusheni nayo!!

Na yamekuja maonyo makali kutoka kwenye hadithi sahihi ya Mtume kwa yule mwenye kunywa pombe. Imepokewa kutoka kwa Jaabir kwenye hadithi marfuu kwamba;

"إِنَّ عَلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ عَهْدَ الْمَنِ يَشْرُبُ الْمَسْكُرَ أَنْ يَسْقِيَهُ مِنْ طَيْنَةِ الْخَيْلِ" قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ وَمَا طَيْنَةُ الْخَيْلِ؟ قَالَ: «عَرْقُ أَهْلِ النَّارِ أَوْ عَصَارَةُ أَهْلِ النَّارِ»

"Hakika mwenyezi Mungu mtukufu ana ahadi na wale wenyewe kunywa pombe kwamba atawanywesha "tiinatilkhabaal" wakasema maswahaba 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni nini hii "tiinatilkhabaal?' Akasema Mtume: "Ni majasho ya watu wa motoni au maji ya watu wa motoni." Muslim 3/587.

Na imepokewa kutoka kwa Ibin Abbas Mwenyezi Mungu awe radhi nae yeye na baba yake kwenye hadithi marfuu;

"مَنْ مَاتَ وَهُوَ مَدْمُنٌ خَمْرًا لَقِيَ اللَّهَ وَهُوَ كَعَابِدٌ وَثَنٌ"

"Mwenye kufa hali ya kuwa mlevi mzoefu atakutana na Mwenyezi Mungu hali ya kuwa ni kama mtu aliyekuwa anaabudu

masanamu.” Tabraniy 12/45. Sahihil Jaamiy No. 6525.

Na kwenye zama zetu za leo kuna pombe na aina mbali mbali za vimeo zikiwa zimetapaka kila sehemu na zikiwa kwenye sampuli mbali mbali na kupewa majina ya aina tofauti tofauti, kama vile beer, alcohol, vodka, champagne, wiski, konyagi, gongo, chang’aa, mbege, wine n.k na kujitokeza kwenye umma huu kundi la watu aliowaelezea Mtume kwenye hadithi tukufu:

”ليشربن ناس من أمتي الخمر يسمونها بغير اسمها“
 ”Miongoni mwa watu wa umma wangu watakunywa pombe na kuiita majina yasiokuwa yake.“ Imam Ahmad 5/342.
 Utawaona watu wakiita vinywaji vya kircho, vinywaji vikali, vinywaji vya kukonga roho badala ya pombe hii ni kwa ajili tu ya kutaka kufanya hadaa na kuharibu maana yake.

﴿يَخَادِعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَمَا يَخْدِعُونَ إِلَّا أَنفُسُهُمْ﴾
 ﴿وَمَا يَشْعُرُونَ﴾

“Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao, nao hawatambui.” Al Baqara : 9.

Na sheria ya kiislamu imekuja na kanuni tukufu kabisa ambayo imekata kabisa mizizi yote ya fitina na vitimbi vyatowe wale wenye kucheza na sheria, pale aliposema Mtume:

”كل مسكر حمر وكل مسكر حرام“

“Kila chenye kulevyaa ni pombe na kila pombe ni haramu.” Muslim 3/1587.

Kwa hiyo basi kila chenye kuichanganya akili na kuilevyaa huwa ni haramu kutumia, iwe kidogo au kwa wingi kama ilivyokuja kwenye hadithi;

”فكل ما خالط العقل وأسكنه فهو حرام قليلاً وكثيراً“

“Kila chenye kuichanganya akili na kuilevyaa ni haramu (kunywa) kidogo au kwa wingi.” Abou Daud No. 3681, na kwenye Sahihi Abou Daud 3128.

Kwa hiyo ni lazima ieleweke kuwa pamoja na pombe kuwa na majina mengi mengi tofauti, lakini kinachokusudiwa ni kitu kimoja na hukumu yake iko wazi iwe gongo (chang`aa) au beer zote ni pombe.

Na mwisho, haya hapa tena ni mawaidha kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwa wale wenyewe kunywa pombe. Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa:

”من شرب الخمر وسكر لم تقبل له صلاة أربعين صباحاً، وإن مات دخل النار، فإن تاب تاب الله عليه، وإن عاد فشرب فسكر لم تقبل له صلاة أربعين صباحاً، فإن مات دخل النار، فإن تاب تاب الله عليه، وإن عاد فشرب فسكر لم تقبل له صلاة أربعين صباحاً، فإن مات دخل النار، فإن تاب تاب الله عليه، وإن عاد كان حقا على الله أن يسقيه من ردغة الخبال يوم القيمة. قالوا: يا رسول الله وما ردغة الخبال؟ قال: عصارة أهل النار“

“Mwenye kunywa pombe na kulewa hatokubaliwa sala yake kwa muda wa siku arobaini na akifa kwenye siku hizo atainingia

motoni. Ikiwa atatubu, basi Mwenyezi Mungu atamkubalia toba yake; ikiwa atarejea tena na kunywa na kulewa hatokubaliwa sala yake kwa muda wa siku arobaini, na ikiwa atakufa ataingia motoni, na ikiwa atatubu basi Mwenyezi Mungu atamkubalia toba yake. Na ikiwa atarejea tena na kunywa na kulewa hatokubaliwa sala yake kwa muda wa siku arobaini na akifa ataingia motoni, na akitubia Mwenyezi Mungu humkubalia toba yake, na ikiwa atarejea tena basi itakuwa ni haki kwa Mwenyezi Mungu kumnywesha radgatul khabaal siku ya kiama, wakasema (maswahaba) Ni nini hii “radghatul khabaal” Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema ni maji yanayowatoka watu wa motoni.” Ibin Maajah No. 3377 na katika Sahihil Jaamiy 6313.

Ikiwa hii ni hali halisi ya wale wenye kutumia pombe, basi fikiria vipi itakuwa hali ya wale wenye kutumia ulevi ambaou una madhara makubwa zaidi na kudumu

**kwenye hali hiyo Kama wale wanaotumia
madawa ya kulevya na Mwenyezi Mungu
atuepushe nayo.**

KUTUMIA VYOMBO VYA FEDHA NA DHAHABU KWA KULIA NA KUNYWA.

Hutokuta sehemu yoyote ya kuuzia vyombo na vifaa vya nyumbani leo hii ila utakuta mara nyingi kuna vyombo vya dhahabu na fedha, au vikiwa vimepakwa au kuchovyekwa kwenye maji ya dhahabu na fedha. Na vile vile kwenye nyumba za matajiri na mahoteli mbali mbali. Si hivyo tu bali aina ya vyombo hivi imekuwa leo hii ndio mionganini mwa zawadi mashuhuri wanazopeana watu kwenye sherehe za aina mbali mbali.

Baadhi ya watu huenda ikawa wasiweke vyombo hivi majumbani mwao, lakini huvitumia kwenye majumba ya watu wengine na kwenye karamu zao za harusi. Mambo haya yote ni katika mambo yaliyoharamishwa katika sheria ya kiislamu, na Mtume ameonya vikali kuhusu kutumia vyombo hivi. Imepokewa kutoka

kwa Umm Salama kutoka kwenye hadithi marfuu:

"إِنَّ الَّذِي يَأْكُلُ أَوْ يَشْرَبُ فِي آنِيَةِ الْفَضْلَةِ وَالْذَّهَبِ
إِنَّمَا يَجْرِي فِي بَطْنِهِ نَارُ جَهَنَّمَ"

"Hakika yule anaekula au kunywa kwenye vyombo vya fedha au dhahabu bila shaka atakuwa anajivutia moto wa Jahanam kwenye tumbo lake." 3/1634.

Na hukumu hii inahusu vifaa na vyombo vyote vya chakula kama vile sahani za chakula, vijiko, uma, visu na vyombo vya kuwakaribishia wageni, na sahani za keki zinazotumika kwenye harusi na kadhalika.

Na baadhi ya watu husema sisi hatuvitumii vyombo hivi kwa chakula, lakini tunaweka kwenye rafu za kioo kwa ajili ya mapambo tu. Hili vile vile halifai kwa kule kuchelea labda unaweza kutumia baada ya kushawishiwa na shetani kwa sababu ni bora kuzuia kuliko kutibu.

KUSHUHUDIA UONGO.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿فَاجتَبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجتَبُوا قَوْلَ الزُّورِ
خَنَافِعَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ﴾ ...

“Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa uongo, mkhalisike kwa Mwenyezi Mungu bila kumshirikisha.” Suratil Hajj 30-31.

Na imepokewa kutoka kwa Abdul Rahman bin Bakra Mwenyezi Mungu awe radhi nae yeye na baba yake , nae akipokea kutoka kwa baba yake akisema:

‘(Siku moja) tulikuwa mbele ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema:

”أَلَا أَنْبَكُمْ بِأَكْبَرِ الْكَبَّانِرِ (ثَلَاثَةً) : الإِشْرَاكُ بِاللَّهِ وَعَقْوَقُ الْوَالَّدِينَ وَجُلُسُوكُانَ مُتَكَبِّرًا - فَقَالَ : أَلَا وَقُولُ
الزُّورَ قَالَ فَمَا زَالَ يَكْرِرُهَا حَتَّى قَلَّنَا : لَيْتَهُ سَكَتَ“

“Je nikupeni khabari ya madhambi makubwa? Je nikupeni khabari ya madhambi makubwa? Je nikupeni khabari ya madhambi makubwa?”(akasema)

“**kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kuwaasi wazee wawili,**” alikuwa ameegemea akakaa sawa kisha akasema “**Juweni na kusema uongo.**” Akasema (baba yake Abdul Rahman bin Bakrat) Ikawa anarejea rejea kauli hii (na kusema uongo) mara nyingi mpaka tukasema; ‘**laiti angenyamaza.**’ Bukhari Fat’hul Baariy 5/261.

Na huku kuirejelea mara nyingi kauli ya kusema uongo ni maonyo na mazingatio kutoka kwa Mtume kutokana na kuchukuliwa kwa wepesi suala hili la kuapa na kushuhudia uongo na kudharauliwa na watu wengi na hivyo kuongezeka madai ya uongo kutokana na husuda na uadui, hatimae kuleta ufisadi mkubwa kwenye jamii. Haki ngapi zimepotea kutokana na ushahidi wa uongo, watu wangapi waliowadhulumu watu wema kutokana na uongo au kupata mambo wasiostahiki kwa sababu ya kutumia uongo au kupewa nasaba zisizokuwa zao kutokana na uongo?

Na miongoni mwa dharau inayofanywa na watu kwenye suala hili, ni haya mambo yanayofanywa na baadhi ya watu mahakamani kwa kumwambia mtu; “twende ukanitolee ushahidi nami nitakutolea ushahidi!” Watu hawa huwa wamekutana tu mahakamani au njiani na wala wakikuwa hawajuani, kabla ya hapo na hivyo kuthubutu kutoa ushahidi wa uongo kwenye jambo ambalo huhitaji ujuzi na ukweli wa hali yenyewe. Kama vile kumtolea ushahidi juu ya haki ya kumiliki ardhi au nyumba au kusifia tabia njema. Huu ni uongo na uzushi kwa sababu ushahidi unatakiwa uwe kama ulivyopokewa kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu;

﴿وَمَا شَهَدْنَا إِلَّا بِمَا عَلِمْنَا﴾

“Na sisi hatukutoa shahada ile isipokuwa kwa yale tuliyoyajua.” Yusuf : 81.

KUSIKILIZA MUZIKI.

Ibin Masoud alikuwa akiapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa muradi wa kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

﴿وَمَنَ النَّاسُ مَنْ يَشْتَرِي لَهُوَ الْحَدِيثُ لَيُضْلِلَ عَنْ سَبِيلِ
اللَّهِ﴾ ...

“Na katika watu wako wanaokhitari maneno ya upuuzi ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu pasipo wao kujua lolote.” Luqman : 6 ni nyimbo, angalia tafsiri ya Ibin Kathiir 6/333.

Imepokewa kutoka kwa Abii Aamir na Abu Malik Al Ash-aariy Mwenyezi Mungu awe radhi nao wakipokea kutoka kwa Mtume kuwa amesema:

”ليكونن من أمتى أقوام يستحلون الحر والحرير
والخمر والمعازف...”

“Watakuja watu kwenye umati wangu watakaokuwa wakihalalisha zinaa na hariri

(kwa wanaume) na pombe na muziki.”
Bukhari Fat hul Baariy 10/51.

Na imepokewa kutoka kwa Anas Mwenyezi
Mungu awe radhi nae kwenye hadithi
marfuu:

”ليكونن فى الامة خسف و قذف و مسخ وذلك اذا
شربوا الخمر و اتذدوا القينات و ضربوا بالمعازف”

”Kutakuja kutokea kwenye umma huu,
kudidimizwa, na kutupwa kutoka juu hadi
chini na kugeuzwa sura ,na hiyo ni pindi
(watu wa umma huu) watakapokunywa
pombe na kuwachukua waimbaji wa kike,
na watakapopiga muziki.” Angalia Silsilati
Sahiihat No. 2203; Tirmidhiy No. 2212.

Na Mtume amekataza kupiga
ngoma, na akaisifu zumari na zeze kuwa ni
sauti ya mpumbavu alie muovu. Na
wanazuoni waliopita kama Imam Ahmad
Mwenyezi Mungu awe radhi nae
wameweka wazi kuhusu uharamu wa ala za
pumbao na muziki kama vile udi, gambusi,
kinubi, filimbi, zumari na toazi. Bila shaka
ala za Muziki wa kileo kwa jumla zinaingia

kwenye hadithi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kukataza muziki. Na ala hizo kama vile violin, fiddle, vinanda, piano, gitaa na zana nyingine, bali ulevi na furaha isiyo na upeo na taathiri inayopatikana kwenye ala za muziki wa kileo ni kubwa zaidi kuliko ala za muziki wa kale ambazo zimeharamishwa Kwenye baadhi ya hadithi si hayo tu bali ulevi wa muziki na urushaji wake wa akili ni mkubwa zaidi kuliko hata ulevi wa pombe. Kama walivyotaja baadhi ya wanazuoni kama Ibin Al Qayyim na wengineo. Bila shaka madhambi huongezeka maradufu na uharamu kuwa mkubwa pindi muziki unapoambatana na nyimbo na sauti tamu kama vile sauti za waimbaji wa kike. Na msiba huwa mkubwa zaidi inapokuwa beti za mashairi ya nyimbo hizo zinapokuwa zinazungumzia mambo yenye kuhusu mapenzi, kusifia ufuska au ujisadi kama vile mashairi ya mipasho au kusifia maungo ya siri ya mwanamke, na kwa sababu hiyo basi ndio maana

wanazuoni wakasema kuwa nyimbo ni posta ya zinaa, na huotesha unaafiki kwenye moyo. Na kwa ujumla imekuwa masuala ya nyimbo na muziki ni katika masuala yenyе kuleta fitina kubwa kwenye zama zetu za leo.

Na mionganini mwa mambo yaliyoongeza balaa kwenye zama hizi ni kuingizwa muziki kwenye vitu vingi kama vile saa, kengele, michezo ya watoto, "kompyuta" na baadhi ya simu, kiasi kwamba imekuwa kujiepusha na muziki ni suala linalohitaji azma kubwa na Mwenyezi Mungu ndie wa kutakiwa msaada.

KUSENGENYA.

Yamekuwa mazungumzo mengi siku hizi kwenye vikao ni kuwasengenya waislamu na kuramba heshima zao, na hali ya kuwa hili ni jambo alilolikataza Mwenyezi Mungu na kuwakimbiza waja wake, na akalitolea mfano wa sura mbaya na yenyekuchukiza kabisa ambapo nafsi ya mtu huona kinyaa pindi anapotajiwa. Akasema Mwenyezi Mungu:

﴿وَلَا يَغْتَبْ بَعْضُكُمْ بَعْضًا أَيْحَبُ أَحَدُكُمْ أَنْ يَأْكُلْ لَحْمَ أَخِيهِ مِنْتَافَرْ هَتْمُوه﴾ ...

“Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine, Je mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliekufa? La hampendi, (basi na haya msiyapende).” Al Hujuraat : 12.

Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake ameweeka wazi maana yake kwa kusema:

"أَتَدْرُونَ مَا الْغَيْبَةِ؟ قَالُوا: اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَعْلَمُ. قَالَ: ذَكْرُكُ أَخَاكَ بِمَا يَكْرِهُ قَلْيلٌ: أَفَرَأَيْتَ إِنْ كَانَ فِي أَخِي مَا أَقُولُ؟ قَالَ: إِنْ كَانَ فِيهِ مَا تَقُولُ فَقَدْ أَغْتَبَهُ وَإِنْ لَمْ يَكُنْ فِيهِ فَقَدْ بَهَتْهُ".

"Je mnajua nini maana ya kusengenya? Wakasema Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wenyewe kujua zaidi akasema ni kumtaja ndugu yako kwa jambo analolichukia. Ika semwa, unaonaje kama ndugu yangu atakuwa nalo jambo hilo ninalolisema. Akasema kama atakuwa nalo jambo hilo unalolisema utakuwa umemsengenya na kama atakuwa hana jambo hilo unalolisema utakuwa umemzulia uongo." Muslim 4/2001.

Usengenyi ni kule kumtaja ndugu yako muislamu kwa mambo anayoyachukia sawa iwe mambo hayo yapo kwenye mwili wake au kwenye dini yake au dunia yake au nafsi yake au tabia zake au umbile lake, na usengenyi una sura nyingi tofauti, kama vile kutaja aibu zake, au kuhadithia kwa kumuiga kwa njia ya dhara.

Na watu wengi hulichukulia suala la usengenyi kwa juu juu pamoja na kuwa maovu yake ni makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na ushahidi wa hayo ni kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake isemayo:

”الربا اثنان وسبعون باباً أدناها مثل إتيان الرجل أمه وإن أرباً الرجل في عرض أخيه“.

“Riba ni milango sabini na mbili wa chini kuliko yote ni kama vile mtu kumuingilia mama yake mzazi na riba kubwa zaidi ni mtu kurefusha ulimi wake kwa kuishambulia heshima ya ndugu yake.”
Silsilati Ssahiihat No. 1871.

Kwa hiyo ni wajibu kwa mwenye kuhudhuria kikao kuukataza uovu huu na kumlinda ndugu yake mwenye kusengenywa na Mtume amelipendezesha suala hili kwa kusema:

”من رد عن عرض أخيه رد الله عن وجهه النار يوم القيمة“

“Mwenye kuihifadhi heshima ya ndugu yake Mwenyezi Mungu atauhifadhi

**uso wake na moto siku ya kiama.” Ahmad
6/450 ; Sahihil Jaamiy no. 6238.**

USAKUBIMBI - UDUKIZI.

Kupeleka maneno ya watu huku na huku kwa lengo la kutaka kuwachonganisha na kuwafanyia ufisadi kati yao ni miongoni mwa sababu kubwa zinazopelekea kukata mafungamano na kuwasha moto wa chuki na uadui kati ya watu. Na Mwenyezi Mungu amekiumbua kitendo hiki kwa kusema:

﴿وَلَا تُطِعْ كُلَّ حَلَافٍ مَّهِينٍ ﴾ هَمَّازَ مَشَاءَ بِنْمِيمٍ ﴾

“Wala usimtii kila muapaji sana aliye dhalili, msengenyaji (msemaji watu) aendae akitia fitina.” Al Qalam : 10-11.

Imepokewa kutoka kwa Hudhaifa kutoka kwenye hadithi marfuu:

« لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ فَتَاتٌ »

“Hatoingia peponi sakubimbi (mchonganishi).” Bukhari 10/472 Fat hul Baariy.

Na imepokewa kutoka kwa Ibin Abbaas akisema ;

عن ابن عباس قال مر النبي صلى الله عليه وسلم بحاط من حيطان المدينة فسمع صوت انسانين يذبيان في قبورهما فقال النبي صلى الله عليه وسلم: " يذبيان، وما يذبيان في كبير - ثم قال - بلى [وفي رواية وإنه ل الكبير] كان أحدهما لا يستتر من بوله وكان الآخر يمشي بالنسمة"

‘(Siku moja) Mtume alikuwa akipita kwenye bustani moja mionganini mwa bustani za madina akasikia sauti za watu wawili wakiadhibiwa kwenye makaburi yao akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

“Watu hawa wanaadhibiwa na hawaadhibiwi kwa kosa kubwa.” Kisha akasema ‘ndio’. Na kwenye mapokezi mengine akasema hakika ni kosa kubwa ; alikuwa mmoja wao hajizui na chachizo za mkojo wake, na mwingine alikuwa akienda (huku na huku) kwa usakubimbi (uchonganishi).” Bukhari Fat’hul Baaariy 1/317.

Na katika sura mbaya kabisa za usakubimbi ni kumchonganisha mtu na mkewe au mke na mumewe, nayo ni kujitahidi kupekeka maneno huku na huku kwa kutaka kuharibu uhusiano uliopo kati yao. Vile vile kitendo cha baadhi ya wafanyakazi maofisini ya kuchukua maneno ya wengine na kuyapeleka kwa meneja au mkurugenzi kwa namna ya uchonganishi ili kuwaletea madhara wafanyakazi wengine. Haya yote ni katika mambo ya haramu kubwa ambayo ni wajibu kabisa kwa kila Muislamu kujiепusha nayo na kujiweka nayo mbali kabisa.

KUINGIA KWENYE NYUMBA ZA WATU BILA RUHUSA.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بَيْوَاتًا غَيْرَ بَيْوَاتِكُمْ حَتَّىٰ
تَسْتَأْسِفُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أهْلِهَا ﴾.....

“Enyi mliaoamini! Msiiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa (mpige hodi) na muwatolee salamu waliomo humo.” An Nuur : 27.

Na akasema Mtume kwa kuweka wazi suala hili kuwa; ila iliyopelekea kuwekwa sheria ya kuomba idhini ni kwa sababu ya kuchelea mtu kuchungulia aibu za wenye nyumba ikiwa kama ataingia kwenye nyumba za watu bila ya kuomba idhini.”

Akasema Mtume:

“إِنَّمَا جَعَلَ الْإِسْتِدَانَ مِنْ أَجْلِ الْبَصَرِ”

“Kuomba idhini kumewekwa kwa ajili ya macho.” Bukhariy Fat’hul Baariy 11/24.

Na leo hii pamoja na kukaribiana majengo na kugusana magorofa na kukabiliana madirisha na milango , imekuwa uwezekano wa kufichuka siri za majirani wao kwa wao ni mkubwa, na wengi wao huwa hawainamishi macho yao chini.Bali watu wengi wenyewe kukaa nyumba za juu kwa kupitia kwenye madirisha na mapaa ya nyumba zao huchungulia kwa kusudi nyumba za chini zilizopakana na nyumba zao. Hii ni khiana na kukiuka heshima ya jirani na ni njia mojawapo yenyewe kupelekea kwenye mambo ya haramu, na pia kitendo hiki husababisha maafa na fitina kubwa baina ya majirani. Na inatosha dalili ya kuonyesha hatari na uovu mkubwa wa jambo hili pale tunapokuta kuwa sheria ya kiiislamu imeruhusu kupofua jicho la yule mwenye kufanya ujasusi kwa kuchunguza au kuchungulia mambo yasiyomhusu.

Amesema Mtume:

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: "من اطلع في بيته
فَوْمَ بَغْرِيْرِ اذْنَهُمْ فَقَدْ حَلَّ لَهُمْ أَنْ يَفْقَوْا عَيْنَهُمْ".

“Mwenye kuchungulia kwenye nyumba ya watu bila ya idhini yao ni halali kwao kulipofua jicho lake.” Muslim 3/1699.

Na kwenye mapokezi mengine:

وفي رواية: ”ففقووا عينه فلا دية له ولا فقصاص.“

“Pofueni jicho lake na wala hana dia wala kisasi.”¹ Ahmad 2/385 Sahihil Jaamiy No. 6022.

¹ Yaani hastahiki mtu huyu kupewa dia wala kulipiza kisasi.

KUNONG'ONA WATU WAWILI MBELE
YA MTU WA TATU.

Haya ni katika maafa ya vikao na ni miongoni mwa hatua anazotumia shetani katika kuwatenganisha waislamu na kupandikiza mbegu ya chuki kwenye vifua vyao. Na katika kuweka wazi hukumu na ila ya kitendo hiki, amesema Mtume:

"إِذَا كُنْتُمْ ثُلَاثَةَ فَلَا يَتَاجِي رَجُلٌ دُونَ الْآخَرِ حَتَّىٰ
 تَخْتَلِطُوا بِالنَّاسِ أَجْلَ أَنْ ذَلِكَ يَخْزُنَهُ".

"Mnapokuwa watatu, basi wasinong'one watu wawili na kumuacha mwengine mpaka mtakapochanganyika na watu wengi kwa sababu kitendo kile kitamhuzunisha (yule wa tatu)." Bukhariy (Angalia Fat'hul Baariy 11/83).

Na inaingia kwenye hukumu ya kitendo hiki pia kunong'ona watu watatu na kumuacha mtu wa nne au kuzungumza watu wawili kwa lugha asiyoifahamu mtu

**wa tatu. Bila shaka kunong'ona ndani yake
kuna aina
ya kumdharau mtu wa tatu au kumfanya
afikiri kwamba hawa watu wawili wana
njama za shari dhidi yake.**

KUREFUSHA NGUO.

Isbaali - ni katika mambo wanayodhania watu wengi kuwa ni mepesi na hali ya kuwa madhambi yake ni makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Isbaali maana yake ni kurefusha nguo mpaka ikaruka au kupita vifundo viwili vya miguu, na baadhi ya watu hurefusha nguo mpaka ikawa anaiburuza kwa nyuma yake , au kugusa chini.

Imepokewa kutoka kwa Abi Dhari Mwenyezi Mungu awe radhi nae :

عن أبي ذر رضي الله عنه مرفوعاً: ثلث لا يكلمهم
الله يوم القيمة ولا ينظر إليهم ولا يزكيهم ولهم عذاب
اليم: المسيل [وفي رواية: إزاره] والمنان [وفي
الرواية: الذي لا يعطي شيئاً إلا منه] والمنفق سلطته
بالحلف الكاذب".

“Watu watatu Mwenyezi Mungu hatozungumza nao siku ya kiama, na wala hatowaangalia na wala hatowatakasa,

na watakuwa na adhabu kali iumizayo;
 (watu hao ni) yule mweye kurefusha (nguo yake)

(na kwenye mapokezi mengine mwenye kurefusha shuka yake)¹, na mwenye kusimanga, (na kwenye mapokezi mengine, na yule ambae hatoi kitu chochote isipokuwa husimbulia (husimanga), na yule mwenye kutoa bidhaa yake kwa kiapo cha uongo.” Muslim 1/102.

Yule mwenye kusema kuwa; “urefushaji wangu wa nguo sio wa kibri,” huyu atakuwa anajaribu kuitakasa nafsi yake kwa utakaso ambao haukuliki, kwa sababu onyo lililokuja kwa mwenye kurefusha nguo yake ni kwa jumla sawa mtu awe amekusudia kufanya kibri au hakukusudia kufanya hivyo.

¹ Mpaka ikawa imevuka na kufunika vifundo viwili vyatayi.

Lakini wote wanaingia kwenye hukumu moja, kama ilivyokuja kwenye:

"ما تحت الكعبين من الإزار ففي النار"

"nguo itakayovuka chini ya vifundo viwili vya miguu, basi vifundo hivyo vitakuwa motoni." Ahmad 6/254 Sahihil Jaamiy No.5571.

Na atakapoirefusha nguo yake kwa kibri hapo adhabu yake huwa ni kali na kubwa kupita kiasi kama ilivyokuja kwenye hadithi:

"من جر ثوبه خلاء لم ينظر الله إليه يوم القيمة."

"Mwenye kuburuta nguo yake kwa kibri, Mwenyezi Mungu hatomuangalia siku ya kiama." Bukhariy 3465.

Hii ni kwa sababu atakua amekusanya makosa ya aina mbili ambayo yote ni haramu. Na kurefusha nguo kupita vifundo viwili ni haramu kwa kila vazi kama ilivyokuja kwenye hadithi ya Ibin Omar Mwenyezi Mungu awe radhi nae:

عن ابن عمر رضي الله عنهم مرفوعاً" الإسبال في الإزار والقميص والعمامة، من جر منها شيئاً خيلاً لم ينظر الله إليه يوم القيمة".

"Kurefusha nguo (Isbali) kupo kwenye shuka (kikoi) kanzu na kiremba, mwenye kuburuta kitu chochote katika hiso kwa kibri basi Mwenyezi Mungu hatomuangalia siku ya kiama." Abou Daud Sahihii Jaamiy 2770.

Na mwanamke yeye huruhusiwa kurefusha nguo yake kupita vifundo viwili vya miguu kiasi cha shibri moja au dhiraa moja ili iweze kusitiri miguu yake kwa akiba, kwa kule kuchelea kuwa isije ikafunuka kwa sababu ya upemo na mfano wa huo. Lakini haifai kuvuka kiwango kilichowekwa kama ilivyo kwenye baadhi ya nguo za mabibi harusi ambazo hupita shubiri moja na hata kufikia wakati mwingine kubebwa na mtu kwa nyuma yake.

WANAUME KUJIPAMBA KWA
DHAHABU KWA NAMNA YOYOTE ILE.

Imepokewa kutoka kwa Abii Mussa Al Ash-
 ariy kwenye hadithi marfuu kuwa:

”عن أبي موسى الأشعري مرفوعاً: أحل لِإثاث
 أمتى الحرير والذهب وحرم على ذكرها“.

“Wameruhusiwa wanawake wa umati
 wangu (kuvaa) hariri na dhahabu na
 kuharamishwa kwa wanaume wake.” Imam
 Ahmad.

Leo hii utakuta kwenye maduka
 idadi kubwa ya vitu vilivyotengenezwa kwa
 ajili ya wanaume kuanzia saa, miwani,
 vifungo, kalamu, mikufu na medali vikiwa
 vimetengenezwa kwa dhahabu au vikiwa
 vimechovwa kwenye maji ya dhahabu
 halisi. Na katika uovu vile vile matangazo
 ya zawadi yanayotangazwa kwa washindi
 wa mashindano mbali mbali utakuta
 wakisema mshindi wa kwanza atapata saa

ya kiume iliyotengenezwa kwa dhahabu n.k.!!

عن ابن عباس رضي الله عنه أن رسول الله صلى الله عليه وسلم رأى خاتماً من ذهب في يد رجل فنزعه فطرحه، فقال: ((يعد أحدهم إلى جمرة من نار فيجعلها في يده؟)) فقيل للرجل بعد ما ذهب رسول الله صلى الله عليه وسلم: خذ خاتمك وانتفع به. قال: لا والله لا أخذه أبداً وقد طرحته رسول الله صلى الله عليه وسلم.

Imepokewa kutoka kwa Ibin Abbas Mwenyezi Mungu awe radhi nae pamoja na baba yake kwamba, Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliiona pete ya dhahabu kwenye mkono wa mtu mmoja akaivua ile pete kisha akaitupilia mbali, kisha akasema; (vipi) anafanya kusudi mmoja wenu (na kuthubutu) kuchukua kaa la moto na kuliweka mkononi mwake? kisha akaambiwa yule mtu baada ya kuondoka Mtume; “Chukua pete yako ufaidike nayo (utumie kwa njia nyingine) akasema ‘hapana, naapa kwa Mwenyezi Mungu sintoichukua pete hiyo milele,

hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ameitupa.' (Nitaichukua vipi wakati Mtume wa Mwenyezi mungu ameitupa)?! Muslim 3/1655.

KUVAA NGUO FUPI NA ZA KUBANA NA
ZENYE KUONYESHA KWA
WANAWAKE.

Miongoni mwa vita tunavyopigwa na maadui wetu kwenye zama hizi ni hii mitindo ya mavazi (fashion) ya kileo ambapo wao ndio walioweka na kubuni mitindo na style zake nakuenea miongoni mwa waislamu. Mavazi haya huwa hayasitiri utupu kwa ufupi wake na kuonyesha viungo vya ndani kutokana na jinsi yanavyobana. Na mavazi mengi katika haya huwa hayajuzu kuvaliwa hata mbele ya wanawake wao kwa wao au mbele ya maharimu. Na Mtume alishatubashiria hali hii ya mavazi ya wanawake wa zama za

mwisho kwenye hadithi ya Abii Huraira, marfuu kuwa:

عن أبي هريرة رضي الله عنه مرفوعاً: صنفان من أهل النار لم أرهما: قوم معهم سياط كاذناب البقر يضربون بها الناس، ونساء كاسبيات عاريات ممبلات مائلات رفسهن كأسنمة البخت المائلة لا يدخلن الجنة ولا يجدون ريحها وإن ريخها ليوجد من مسيرة كذا وكذا".

"Makundi mawili ya watu wa motoni sijawahi kuyaona, watu watakaokuwa na mijeledi kama mikia ya ng'ombe wakiwapiga watu (kwa kutumia mijeledi hiyo) na wanawake wenyewe kuonekana wamevaa hali ya kuwa wako uchi, wenyewe kutembea kwa maringo kwa kujitupa tupa, vichwa vyao ni kama nundu za ngamia zilizoinama hao hawataingia peponi na wala hawataipata harufu yake, kwa sababu harufu yake inapatikana kwenye mwendo wa masafa kadhaa wa kadhaa." Hadithi ameipokea Muslim 3/1680

Na yanaingia kwenye hukumu ya mavazi haya, vile vile mavazi wanayovaa baadhi ya wanawake ambayo huwa na mkato mrefu

kwa chini, au kuchanwa kwa nyuma au mbele, au kuwa yamekatwa katwa kwa chini, kiasi kwamba anapokaa mwanamke hufikia kuonyesha sehemu zake za siri. na huku ni kujifananisha na makafiri na kuwafuata kwenye mitindo na staili zao walizozusha za mavazi yenyenye fedheha. Mwenyezi Mungu ndie tunaemuomba salama.

Na katika mambo ya hatari vile vile kuwapo picha chafu chafu mbali mbali kwenye baadhi ya mavazi kama vile picha za wanamuziki, au kikundi cha muziki au chupa za pombe au picha za vitu vyenye roho ambazo zimeharamishwa kisheria, au alama za vilabu na jumuia za kikhabithi au maneno machafu yaliyokosa heshima na adabu.

**KUUNGANISHA NYWELE KWA
NYWELE ZA BANDIA KWA
MWANAMUME NA MWANAMKE.**

Imepokewa kutoka kwa Asmaa bint Abubakar akisema:

عن أسماء بنت أبي بكر قالت جاءت امرأة إلى النبي صلى الله عليه وسلم فقالت: يا رسول الله إن لي ابنة عريساً أصابها حصبة فت薨ق (تساقط) شعرها أفالله؟ فقال: "لعن الله الوالدة والمستوصلة".

Alikuja mwanamke mmoja kwa Mtume akasema; 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mimi nina binti yangu bi harusi amepatwa

na surua na nywele zake zinaanguka. Je niziunganishe (kwa nywele bandia) akasema Mtume:

"Amemlaani Mwenyezi Mungu mwenye kuunganisha nywele na mwenye kutaka kuunganishiwa." Muslim 3/1676.

Na imepokewa kutoka kwa Jaabir bin Abdillah akisema kuwa:

”عن جابر قال: زجر النبي صلى الله عليه وسلم أن تصل المرأة برأسها شيئاً“

Mtume amekataza kwa mwanamke kuunganisha chochote kwenye kichwa chake.” Muslim 1679.

Na mfano wa hii ni hizi nywele za bandia zinazojulikana kwenye zama zetu kwa jina la wigi (wig) au baroka. Na mwenye kuunganisha nywele wa zama zetu ni hawa watu wenye saloon.

Na mfano wa haramu hii vile vile kuвая nywele za kuazima kama wanavyofanya baadhi ya waigizaji wa kike na kiume wasiokuwa na tabia nzuri kwenye tamthilia na michezo ya kuigiza.

WANAWAKE KUJIFANANISHA NA
WANAUME, NA WANAUME
KUJIFANANISHA NA WANAWAKE
KWENYE MAVAZI, MANENO AU
MAUMBILE.

Miongoni mwa maumbile ambayo Mwenyezi Mungu ameyawekea sheria kwa waja wake ni kwa mwanamume kujaribu kuhifadhi umbile lake la asili la kiume aliloumbwa na Mwenyezi Mungu na kwa mwanamke kuhifadhi umbile lake la kike aliloumbwa na Mwenyezi Mungu. Na na kuhifadhi sheria hii ni moja ya sababu ambazo hupelekea kunyooka maisha ya binadamu na kupatikana utulivu, kinyume cha hapo huwa hakuna utulivu. Na Mwanamke kujifanlisha na mwanamume au mwanamume kujifanlisha na mwanamke ni kwenda kinyume na maumbile halisi ya Mwenyezi Mungu na pia ni sababu ya kufungua milango ya

maasi na kueneza ujisadi kwenye jamii. Na hukumu ya kitendo hiki kisheria ni haramu. Na inapokuja laana kwenye aya au hadithi kwa mtu mwenye kufanya kitendo fulani maana yake huwa ni kuhamishwa kwa kitendo hicho na kwamba kitu hicho huingia kwenye madhambi makubwa. Imepokewa kutoka kwa Ibin Abaas Mwenyezi Mungu awe radhi nae na baba yake kuwa:

وَعَنْ أَبْنَ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا مَرْفُوعًا: لَعْنَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "الْمُتَشَبِّهِينَ مِنَ الرِّجَالِ بِالنِّسَاءِ وَالْمُتَشَبِّهَاتِ مِنَ النِّسَاءِ بِالرِّجَالِ".

‘Mtume wa Mwenyezi Mungu amewalaani wanaume wenyewe kujifananisha na wanawake na wanawake wenyewe kujifananisha na wanaume.’ Bukhariy Fat’hul Baariy 10/332.

Na imepokewa tena kutoka kwa Ibin Abbas kwenye hadithi marfuu:

وَعَنْ أَبْنَ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا مَرْفُوعًا: "لَعْنَ رَسُولِ اللَّهِ الْمُخْتَنِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالْمُتَرْجَلَاتِ مِنَ النِّسَاءِ".

“ Amewalaani Mtume wa Mwenyezi Mungu wale wanaume wenyе kujifanya wanawake na wanawake wenyе kujifanya wanaume.” Bukhariy Fat’hul Baariy 10/333.

Na kujifananisha huku kunaweza kukawa kwa njia ya harakati, utulivu au mwendo kama vile kujilegezalegeza kwenye mwili au kuzungumza au kutembea kama mwanamke.

Pia kujifananisha kupo kwenye mavazi. Haifai kwa mwanamume kuваа mikufu (chain), bangili, vikuku vya mguuni au hereni n,k. kama ilivyoenea kwa watu wengi na hasa vijana wa kileo wasiojali sheria za Mwenyezi Mungu.

Vile vile haifai kwa mwanamke kuваа mavazi ambayo ni hasa kwa mwanamume kama vile kuваа kanzu ya kiume au shati, si hivyo tu bali ni wajibu pia kutofautiana na mwanamume kwenye umbo na staili pia.

Na dalili yakuwa ni wajibu kwa kila mmoja katika jinsia mbili hizi kujitofautisha

na mwingine kwenye mavazi. Ni hadithi iliyopokewa na Abii Huraira marfuu kuwa: عن أبي هريرة رضي الله عنه مرفوعاً: "لعن الله الرجل يلبس لبسة المرأة، والمرأة تلبس لبسة الرجل". "Mwenyezi Mungu amemlaani mwanamume anaevaa vazi la kike na mwanamke anaevaa vazi la kiume." Abu Daud 4/355 Sahihil Jaamiy No. 5071.

KUPAKA RANGI NYEUSI KWENYE NYWELE.

Kwa hakika kitendo hiki ni haramu kutokana na onyo kali lilotajwa kwenye kauli ya Mtume kuwa:

قال النبي صلى الله عليه وسلم: "يكون قوم يخضبون في آخر الزمان بالسود حواصل الحمام لا يريحون رائحة الجنة".

"Watakuwa watu kwenye zama za mwisho wakipaka rangi nyeusi (kwenye vichwa vyao) kama vile uchafu wa njiwa (kinyesi). (Watu hawa) hawataipata harufu ya pepo" Abou Daud 4/319 sahihil Jaamiy No. 8153.

Kitendo hiki kimeenea kwa watu wengi hasa walioanza kutokewa na mvi. Huamua kubadilisha rangi yamvi hizo kwa kupaka rangi nyeusi. Kitendo hiki kimepelekea kupatikana ufisadi kama vile kufanya hadaa na udanganyifu kwa waja wa Mwenyezi Mungu na kujifananisha na hali isiyokuwa ya kwao.

Na bila shaka kitendo hiki kina athari mbaya kwa tabia ya mtu, na huenda kikapelekea kwenye hatari. Imethibiti kwenye hadithi sahihi kuwa Mtume alikuwa akibadilisha mvi kwa kupaka hina na mfano wake, na kupelekea nywele zake kuwa rangi ya njano njano au wekundu au kumili kwenye rangi ya buni.

Na alipoletewa Abii Kuhaafa siku ya kukombolewa mji wa Maka huku kichwa chake na ndevu zake zikiwa kama mti wenyewe matunda mengi kwa shida ya weupe wake akasema Mtume:

”غِرِّوْهُذَا بَشِّيْءَ وَاجْتَبِوا السَّوَادَ“

”Zibadilisheni mvi hizi kwa kitu kingine na jiepusheni na rangi nyeusi.“ Muslim 3/1663. Na sahihi kwa mwanamke ni sawa na mwanamume haifai kwake kupaka rangi nyeusi isiyokuwa weusi wa nywele zake.

KUCHORA VITU VYENYE ROHO KWENYE NGUO KUTANI NA KWENYE KARATASI.

Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Masoud Mwenyezi Mungu awe radhi nae kwenye hadithi marfuu, kuwa:

عن عبد الله بن مسعود رضي الله عنه مرفوعاً: "إن
أشد الناس عذاباً عند الله يوم القيمة المصوروں".

“Watu watakaokuwa na adhabu kali zaidi siku ya kiama ni wale wachoraji.” Bukhariy Fat’hul Baariy 10/382.

Na imepokewa kutoka kwa Abii Huraira kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

عن أبي هريرة رضي الله عنه مرفوعاً: قال الله تعالى: "وَمَنْ أَظْلَمَ مَنْ يَخْلُقُ كُلْفَةً فَلِيَخْلُقْهَا حَبَّةً وَلِيَخْلُقْهَا ذَرَّةً".

“Ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anaeumba kama umbile langu, na waumbe japo kama punje moja na waumbe japo kama mdudu chungu.”

Na imepokewa kutoka kwa Ibin Abbas kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa: عن ابن عباس رضي الله عنهما مرفوعاً: كل مصور في النار يجعل له بكل صورة صورها نفس فتعذب في جهنم." قال ابن عباس: إن كنت لا بد فاعلا فاصنع الشجر وما لا روح فيه.

"Kila mchoraji atakuwa motoni, atawekewa nafsi kwa kila picha aliyoichora kisha aadhibiwe Jahanam." Akasema Ibn Abbas: Kama huna budi kufanya basi tengeneza za miti au vitu visivyokuwa na roho ndani yake. " Muslim 3/1671.

Hadithi hizi zinajulisha kuwa ni haramu kuchora picha za vitu vyenye roho kuanzia binaadamu na baadhi ya wanyama wenyе vivuli au wasiokuwa na vivuli. Sawa iwe imechapishwa, au imechorwa au imenakishiwa au imechongwa na mfano wa hizo. Na hadithi zenye kuharamisha zinajumlisha hali hizo zote.

Na muislamu wa kweli ni yule mwenye kusalimu amri mbele ya aya za Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume wake bila

kuleta ubishi au kuhoji kwa kusema; 'mimi siabudu hizi picha wala kuzisujudia.' Lau kama mtu mwenye akili timamu atatizama kwa undani na kutafakari ufisadi mmoja tu wa kuenea picha kwenye zama zetu, basi atajua hikma ya sheria hii, kwa nini imekuja na kuhamramisha picha, na ufisadi mkubwa ulioenea kwenye zama zetu wa kuchochea matamanio ya kijinsia bali wakati mwingine kumuingiza mtu kwenye kufanya mambo machafu yanatokana na mapicha haya yalioenea kila kona. Haifai kwa muislamu kuhifadhi picha ya vitu vyenye roho nyumbani kwake ili isije kuwa ni sababu ya kuwafanya malaika wakatae kuingia nyumbani kwake; kwa sababu Mtume anasema:

قال النبي صلى الله عليه وسلم: " لا تدخل الملائكة
بيتاً فيها كلب ولا تصاوير "

"Malaika hawaingii kwenye nyumba yenyeye mbwa au picha." Bukhariy -fat'hul Baariy 10/380.

Kwenye baadhi ya majumba ya Waislamu utakuta ndani yake kuna masanamu, na baadhi ya masanamu haya yakiwa ni vitu vinavyoabudiwa na makafiri lakini huekwa kwenye majumba hayo kwa kudai kuwa ni ukumbusho au ni mapambo. Masanamu kama haya uharam wake ni mkubwa kuliko mengine.

Na vile vile picha zilizotundikwa uharamu wake huwa ni mkubwa kuliko nyingine zisizotundikwa, mara ngapi masanamu au picha hizi tumeziona zikipelekea kwenye kuabudiwa , na mara ngapi masanamu haya au picha hizi tumezishuhudia zikiwa ni sababu ya kufufua huzuni zilizosahaulika?, na mara ngapi zimewapelekea watu kwenye kujifakharisha?

Kwa hiyo ni wajibu kuziondosha picha zote au kuzifuta isipokuwa tu zile ambazo kuna uzito wa kufanya hivyo kama vile picha zilizoenea kwenye makopo ya bidhaa mbali mbali, picha za kwenye makamusi

mbali mbali na vitabu vya rejea (reference books) ambavyo huwa na faida kwa watu. Lakini hii ni pamoja na kufanya juhudi ya kutafuta mbinu ya kuondokana nazo kwa kadri itakavyowezekana.

Inaruhusiwa kuhifadhi picha kwa matumizi muhimu ya dharura kama vile picha za vitambulisho mbali mbali, leseni, pasi za kusafiria na matumizi mengine muhimu.

Baadhi ya wanazuoni wameruhusu picha zenye kudharauliwa kama zile zenye kukanyagwa kwa miguu.

Mwenyezi Mungu anasema:

..... ﴿فَإِنْتُمْ أَنْتُمُ الْمُسْتَطْعِمُونَ﴾

“Mcheni Mwenyezi Mungu muwezavyo (mwisho wa jitihada zenu).” Attaghaabun 16.

KUONGOPA KWENYE NDOTO.

Baadhi ya watu kwa kusudi kabisa huzusha ndoto ambazo hawakuziona kwa ajili ya kutafuta utukufu na umashuhuri na sifa kwa watu, au kwa ajili ya kujinufaisha kimali; au kumtisha mtu mwenye kuwa na uadui nae na kadhalika.

Na watu wengi wa kawaida wanaamini Imani hii ya ndoto na kushikamana nazo. Hivyo watu hawa hupata fursa ya kuwahadaa watu wa kawaida kwa uongo wao, lakini wajue kuwa Mtume ameonya vikali kwa yule mwenye kufanya kitendo hiki, kwa kusema:

"إِنَّمَا أَعْظَمُ الْفَرِيَادِيَّ يَدْعُ الرَّجُلَ إِلَىٰ غَيْرِ أَبِيهِ أَوْ يَرِيَ عَيْنَهُ مَا لَمْ تَرُ وَيَقُولُ عَلَىٰ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَا لَمْ يَقُلْ"

"Hakika katika uzushi mkubwa ni mtu kudai asiyekuwa baba yake, au kuona jicho lake jambo ambalo hajalionna na kumzushia Mtume wa Mwenyezi Mungu jambo

ambalo hakulisema.” Bukhariy Fat’hul 6/540.

Amesema Mtume:

”من تحلم بحلم لم يره كلف أن يعقد بين شعيرتين ولن يفعل ”

“Mwenye kujiotesha ndoto ambayo hakuiona atalazimishwa kufunga punje mbili za shayiri na hatoweza.” Bukhariy Al Fat’hu 6/540

Bila shaka kuzifunga punje mbili za shayiri ni jambo lisilowezekana kabisa kwa hiyo malipo yake yatakuwa mfano wa kitendo hiki.

KUKAA JUU YA KABURI NA
KUKANYAGA NA KUJISAIDIA HAJA
KWENYE MAKABURI.

Imepokewa kutoka kwa Abii Huraira akisema; Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

عن أبي هريرة رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: "لأن يجلس أحدكم على جمرة فتحرق ثيابه فتخلص إلى جلده خير له من أن يجلس على قبر".

“ Ni bora kwa mmoja wenu kukaa juu ya kaa la moto ambalo linaweza kuunguza nguo yake na kuja kukutana na ngozi yake kuliko kukaa juu ya kaburi.” Muslim 2/667.

Ama kukanyaga makaburi, baadhi ya watu hufanya hivi bila kujali lolote wakati wa kuzika maiti wao. Tena hukanyaga kwa viatu vyao kwenye makaburi ya jirani bila kuheshimu maiti wengine, na kwa uovu wa kitendo hiki anasema Mtume:

"لأن أمشي على جمرة أو سيف أو أخصف نعلي
برجلي أحب إلى من أن أمشي على قبر مسلم."

"Kutembea juu ya mkaa wa moto au juu ya upanga au kutengeza kiatu changu kwa mguu wangu ni bora kwangu kuliko kutembea juu ya kaburi la muislamu" Ibin Maajah 1/499. Sahihil Jaamiy 5038.

Ikiwa hii ni hali ya mtu mwenye kutembea juu ya kaburi, vipi itakuwa hali ya wale wenye kupora ardhi ya makaburi na kusimamisha majengo ya biashara juu yake, au nyumba za kuishi?

Ama kujisaidia haja kubwa au haja ndogo kwenye makaburi kama wanavyofanya baadhi ya watu wasio kuwa na maadili mema wanaopanda kwenye makaburi na kujisaidia ndani na kuwaudhi maiti kwa harufu na najisi yake, watu hawa Mtume anasema kuwa:

قال النبي صلى الله عليه وسلم: "وما أبالي أوسط القبر قضيت حاجتي أو وسط السوق."

“ Sijali, je ni kati ya kaburi nimekidhi haja yangu au kati kati ya soko.” Ibin Maajah 1/499.

Yaani ubaya na uovu wa mtu kwenda haja kwenye makaburi ni sawa na uovu wa mtu kuvua nguo na kujisaidia haja yake mbele za watu na kati kati ya soko.

Na wale wanaotupa uchafu juu ya makaburi na kuyageuza makaburi hasa yale yalihamwa kuwa ni majaa ya taka hao watakuwa na maovu sawa na hao waliotajwa hapo nyuma.

Na adabu inayotakiwa wakati wa kufanya ziara kwenye makaburi ni kuvua viatu wakati unapotaka kupita kati ya kaburi.

KUTOJIZUIA NA MKOJO.

Miongoni mwa uzuri wa sheria ya kiislamu ni kuwa imekuja kutengeneza kila jambo lenye kupendeza na binaadamu na miongoni mwa mambo hayo ni kuondosha najisi, na kwa ajili hiyo ikaweka sheria ya kustanji kwa maji na kutumia vijiwe wakati wa kwenda haja ndogo au kubwa, na kubainisha namna ya kujinadhifisha na kujisafisha kwa vijiwe hivyo au maji. Baadhi ya watu hudharau kuondosha najisi wakati wa kwenda haja ndogo au kubwa na kusababisha kuchafuka nguo zao,

au kuchafuka miili yao na hatimae kutosihi sala zao.

Na mtume amesema kuwa kitendo hiki cha kutojinadhifisha na kujisafisha na mkojo ni miongoni mwa sababu kubwa zitakazo pelekea mtu kuadhibiwa kaburini kwake.

Imepokewa kutoka Ibin Abbas kuwa alipita Mtume kwenye bustani mionganini mwa bustani za Madina akasikia sauti ya watu wawili wakiadhibiwa kwenye makaburi yao. Akasema Mtume:

عَنْ أَبْنَى عَبَّاسٍ قَالَ مِنَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِحَاطِنَ مِنْ حِيطَانِ الْمَدِينَةِ فَسَمِعَ صَوْتَ إِنْسَانَيْنِ يَعْذَبَانِ فِي قُبُورِهِمَا فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: « يَعْذَبَانِ، وَمَا يَعْذَبَانِ فِي كَبِيرٍ ثُمَّ قَالَ - بَلَى [وَفِي رَوَايَةِ إِنَّهُ لَكَبِيرٍ] كَانَ أَحَدُهُمَا لَا يَسْتَرِّ مِنْ بُولِهِ وَكَانَ الْآخَرُ يَمْشِي بِالنَّمِيمَةِ ».

”(Watu hawa)wanaadhibiwa na hawaadhibiwi kwa kosa kubwa, kisha akasema ndio.“

Na kwenye mapokezi mengine :

”Kwa hakika wanaadhibiwa kwa kosa kubwa, alikuwa mmoja wao hajizui na chachizo za mkojowake na alikuwa mwingine akienda huku na huku kwa usakubimbi (uchonganishi). “ Bukhariy Fat'hul Baariy 1/317.

”أَكْثَرُ عَذَابِ الْقَبْرِ فِي الْبُولِ“

Bali amesema Mtume, na adhabu nyingi (zitakazowapata watu) kaburini (zitatokana na kutojizuia kwao) kwenye mkojo. Imam Ahmad 2/326 Sahihil Jaamiy 1213.

Na kutojizuia na chachizo za mkojo zinamhusu kila mmoja anaekwenda haja, kisha akasimama haraka haraka kabla ya kuisha mkojo, au akawa anakwenda haja kwenye ukuta au kwenye sehemu ambayo husababisha mkojo wake kuruka na kurudia kwenye nguo zake, au akaacha kustanji kwa maji au kutumia vijiwe au kupuuza kabisa.

Hivi leo imefikia hali ya kujifananisha na makafiri katika upeo wa hali ya juu kiasi kwamba imefikia baadhi ya vyoo vimetengenezwa sehemu ya kukidhia haja ndogo ukutani tena sehemu iliyokuwa wazi. Imekuwa mtu anajisaidia haja ndogo mbele ya watu wanaotoka na kuingia bila haya au aibu yoyote, kisha akainua nguo zake na kucaa juu ya najisi. Na hivyo anakuwa amekusanya mambo

mawili ya haramu kwa wakati mmoja. Kwanza kabisa hakujistiri au kuhifadhi tupu yake mbele ya macho ya watu. Na pili hakujisafisha na kujiepusha na chachizo za mkojo wake.

**KUSIKILIZA MAZUNGUMZO YA WATU
HALI YA KUWA WENYEWE
HAWAPENDI.**

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَا تَجْسِدُوا﴾

“Wala msipeleleze habari za watu.”

Al Hujuraat : 11.

Imepokewa kutoka kwa Ibin Abbaas Mwenyezi Mungu awe radhi nae yeye na baba yake , kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa:

عن ابن عباس رضي الله عنه مرفوعاً: "من استمع إلى حديث قوم وهم له كارهون صب في أذنيه الآنك يوم القيامة".

“Mwenye kusikiliza mazungumzo ya watu hali ya kuwa wenyewe hawapendi atapigwa risasi za moto kwenye masikio yake siku ya kiamaa.” Tabraaniy 11/248-249.

Na ikiwa atakuwa anachukua maneno yao bila wao wenyewe kujua kwa nia ya kutaka kuwatia kwenye madhara basi atakuwa

anajiingiza kwenye dhambi nyingine, ya ujasusi na kuingia kwenye kauli ya mtume isemayo:

« لا يدخل الجنّة قاتٍ »

“Hatoingia peponi mchonganishi (sakubimbi).” Bukhari Fat’hul Baariy 10472.

KUWA NA UJIRANI MBAYA.

Kumuudhi jirani ni katika mambo makubwa ya haramu yalioharamishwa kwenye Uislamu kutokana na haki kubwa alizo nazo jirani. Imepokewa kutoka kwa Abii Shureihi Mwenyezi Mungu awe radhi nae kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa;
 عن أبي شريح رضي الله عنه مرفوعاً: " والله لا يؤمن والله لا يؤمن و الله لا يؤمن قيل: من يا رسول الله؟ قال: " الذي لا يؤمن جاره بوانقه".

“Wallahi haamini, wallahi haamini, wallahi haamini! (akaambiwa nani huyo asiyeamini) ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema ; “Yule ambae hasalimiki(hatulii) jirani yake kwa maudhi yake.”

Bukhariy Fat'hul Baariy 10/443.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئاً وَبِالْوَالَّدَيْنِ إِحْسَاناً وَبِذِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَى

وَالْجَارُ الْجَنْبُ وَالصَّاحِبُ بِالْجَنْبِ وَابْنُ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ
أَيْمَانَكُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَلِّاً فَخُورًا ﴿٤﴾

“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote, na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima

na masikini na jirani walio karibu na jirani walio mbali na rafiki walio ubavuni (mwenu) na msafiri aliyeharibikiwa, na wale iliyowamiliki mikono yenu yakulia (kuume). Bila shaka Mwenyezi Mungu hawapendi wenyewe kiburi wajivunao.”

Annisa : 36.

Na Mtume amefanya sifa njema anazokusifia jirani yako au sifa mbaya anazokusifia kuwa ni kipimo cha ihsani au uovu. Imepokewa kutoka kwa Ibin Masoud Mwenyezi Mungu awe radhi nae akisema, alisema mtu mmoja kumuambia Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa:

عَنْ أَبْنَى مُسْعُودَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَجُلٌ لِلنَّبِيِّ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ كَيْفَ لَيْ أَعْلَمَ إِذَا

أَحْسَنْتُ أَوْ إِذَا أَسَأْتُ؟ فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: إِذَا سَمِعْتَ جِيرَانَكَ يَقُولُونَ: "قَدْ أَحْسَنْتَ قَدْ أَحْسَنْتَ إِذَا سَمِعْتُهُمْ يَقُولُونَ: قَدْ أَسَأْتَ قَدْ أَسَأْتَ".

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi mungu, mimi nitajua je kama nimefanya wema au kufanya uovu?” Akasema Mtume; “Utakapowasikia jirani zako wakisema hakika umefanya vizuri, basi (jua) umefanya wema, na utakapowasikia wakisema hakika umekosea basi jua umefanya uovu.” Ahmad: 1/402 Sahihil Jaamiy 6348.

Kumuudhi jirani yako kuna sura nydingi tofauti mionganini mwa hiso kumkataza kuingiza au kupitisha mbao au mti kwanye ukuta mnaoshirikiana pamoja, au kuinua jengo juu yake na kumkinga na jua, au hewa safi bila ya idhini yake, au kufungua madirisha upande wake au kuyarefusha kwa lengo la kutaka kuchungulia siri zake za ndani, au kumuudhi kwa sauti za kusumbua kama vile kugonga vitu,

kupiga kelele na hasa wakati wa kulala na kupumzika au kuwapiga watoto wake au kutupa uchafu kwenye kizingiti cha mlango wake, na dhambi huwa kubwa mara mbili zaidi kama mtu atakiuka heshima ya jirani yake. Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa:

"لأن يزني الرجل بعشر نسوة أيسر عليه من أن يزني بأمرأة جاره، لأن يسرق الرجل من عشرة أبيات أيسر عليه من أن يسرق من بيت جاره." رواه البخاري في الأدب المفرد، رقم: ١٠٣

"Mtu kuzini na wanawake kumi madhambi yake huwa mepesi juu yake kuliko kuzini na mke wa jirani yake; na mtu kuiba kwenye nyumba kumi madhambi yake huwa ni mepesi juu yake kuliko kuiba kwenye nyumba ya jirani yake." Bukhari Adabul Mufrad No. 103.

Baadhi ya watu wasioikuwa waaminifu hutumia fursa ya kutokuwapo jirani yake kama vile kuwapo kwenye zamu ya usiku kazini kwa kuingia nyumbani kwake kwa lengo la kutaka kufanya ufisadi

na uharibifu. Basi ole wao watu hao na adhabu kali ya siku ya kiama.

KUFANYA MADHARA KWENYE USIA.

Katika misingi mikuu ya uislamu ni kuwa hakuna kufanya madhara wala kulipiza kufanya madhara. Na mionganini mwa mifano ya msingi huu ni kuwadhuru warithi wa kisheria au baadhi yao, na mwenye kufanya kitendo hiki basi ole wake na kauli hii ya Mtume:

قال صلى الله عليه وسلم: "من ضار أضر الله به ومن شاق شق الله عليه"

"Mwenye kutaka kudhuru Mwenyezi Mungu humdhuru yeye mwenyewe, na mwenye kutaka kuyafanyisha mambo kuwa magumu basi Mwenyezi Mungu humfanyia ugumu yeye mwenyewe." Ahmad 3/453 ; Sahihil Jaamiy No. 6348.

Na miongoni mwa sura za madhara kwenye usia ni kumnyima mmoja wa warithi haki yake ya kisheria kwenye urithi au kuwausia warithi kinyume na maamrisho ya sheria ya Mwenyezi Mungu, au kuusia zaidi ya thuluthi ya mali.

Kwenye baadhi ya nchi ambazo hazihukumu kwa sheria za Mwenyezi Mungu humwia vigumu mwenye haki kuchukua haki yake aliyopewa na Mwenyezi Mungu kutokana na kanuni za mahakama zisizotumia sheria za Mwenyezi Mungu kuhukumu kinyume na sheria za Mwenyezi Mungu, na kuamuru kwa nguvu kutekeleza usia wa kidhalimu ulioandikishwa mbele ya wakili. Ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao na ole wao kwa yale wanayoyachuma.

KUCHEZA DADU (DICE)

Michezo mingi iliyoenea na kutumiwa na watu wengi huwa imekusanya mambo mengi ya haramu, na miongoni mwa michezo hiyo ni dadu.

Na Mtume ameuhadharisha vikali mchezo huu kwa sababu hufungua milango ya kamari, akasema:

"من لعب بالنردشير فكأنما صبغ يده في لحم خنزير
ودمه" ودمه

"Mwenye kucheza dadu ni kama mtu aliyeuchovya mkono wake kwenye nyama ya nguruwe na damu yake." Muslim 4/1770.
Na imepokewa kutoka kwa Abii Mussa kutoka kwenye hadithi marfuu:

عن أبي موسى رضي الله عنه: "من لعب بالنرد
فقد عصى الله ورسوله"

"Mwenye kucheza dadu atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake."
Ahmad 4/394; Sahihil Jaamiy 6505.

KUMLAANI MUISLAMU NA KUMLAANI ASIYESTAHIKI KULAANIWA.

Watu wengi hushindwa kumiliki ndimi na nafsi zao wakati wanapopatwa na ghadhabu, na haraka haraka hukimbilia kwenye kutoa laana. Huwalaani binaadamu, wanyama, vitu yabisi, masiku na masaa, na wakati mwingine hufikia hata kujilaani ye ye mwenyewe binafsi na watoto wake na wakati mwingine mke kumlaani mumewe au mume kumlaani mkewe. Kitendo hiki ni cha uovu mno, tena kina hatari kubwa ndani yake. Imepokewa kutoka kwa Abii Zaidi Thaabit bin Dhihak Al-Ansaariy Mwenyezi Mungu awe radhi nae, kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa: عن أبي زيد ثابت ابن الصحák الأنصاري رضي الله عنه مرفوعا " ومن لعن مؤمنا فهو كفتله ". "Mwenye kumlaani muislamu ni kama vile aliyemuua." Bukhariy - Fat'hul Baariy 10/465.

Kwa vile laana imekuwa kitu cha kawaida kwa wanawake wengi, kwa sababu hiyo basi ameweka wazi Mtume kuwa kitendo hiki ni mionganini mwa sababu za kuwaingiza watu wengi motoni. Na vile vile wenye kulaaniana hawatokuwa na wakuwaombea siku ya kiama. Na hatari kubwa kupita zote ni kuwa laana huenda ikamrudia mwenye kuitoa ikiwa atakuwa ameitamka kwa dhuluma. Na kwa sababu hiyo basi atakuwa amejiombea yeye mwenyewe binafsi kufukuzwa na kuwekwa mbali na rehma za Mwenyezi Mungu.

KUOMBOLEZA KWENYE KIFO.

Katika uovu mkubwa kabisa ulioenea miongoni mwa baadhi ya wanawake ni kuinua sauti juu na kupiga kelele kumuombolezea maiti, au kupiga mashavu, `au kuchana nguo, au kunyoa nywele au kuzifunga na kuzikata, na mambo haya yote yanaonyesha juu ya kutoridhika kwao na kadari au hukumu iliyopitishwa na Mwenyezi Mungu na kutokuwa na subira juu ya misiba. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake amewalaani vikali wale wote wenye kufanya vitendo hivi.

Imepokewa kutoka kwa Abii Umaamat **Mwenyezi Mungu awe radhi nae kuwa:**
 عن أبي أمامة رضي الله عنه "أن رسول الله صلى الله عليه وسلم لعن الخامسة وجهها وشاقة جيبيها وداعية بالويل والثبور".

“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amemlaani mwanamke mwenye kuparura uso wake na mwenye kuchana nguo zake na mwenye

kujiombea uangamivu na msiba.” Ibin Maajah 1/505; sahihil jaamiy No. 5068.

Na imepokewa kutoka kwa Abdillah bin Masoud Mwenyezi Mungu awe radhi nae, kutoka kwenye hadithi marfuu:

عن أبي مسعود رضي الله عنه مرفوعاً: "ليس منا من لطم الخدود وشق الجيوب ودعى بدعوى الجاهلية" "Si katika sisi (Waislamu) yule mwenye kupiga mashavu yake, na kuchana nguo zake, na kufuata mila za kipagani (mila za zama za kijahilia)." Bukhariy - Fat'hul Baariy 3/163.

Amesema Mtume:

قال النبي صلى الله عليه وسلم: " الناحية إذا لم تتب قبل موتها تقام يوم القيمة وعليها سربال من قطران ودرع من جرب " قاتل

“Mwanamke mwenye kuomboleza kama hakutubia (kwa Mola wake) kabla ya kufa kwake atasimamishwa siku yakiamaka huku akiwa na vazi la lami na deraya za vigaga.”

KUPIGA USONI NA KUJIWEKA ALAMA KWENYE USO.

Adhabu hii hutumiwa na wazazi wengi na walimu pindi wanapowaadhibu watoto kwa kuwapiga makofi usoni na mfano wa hii. Na vile vile baadhi ya watu hutumia kipigo hiki kwa watumishi wao. Kipigo hiki pamoja na kuwa ndani yake kuna kuudharau uso alioutukuza Mwenyezi Mungu kwa binaadamu, pia kipigo hiki kinaweza kusababisha kupoteza baadhi ya viungo vyahisia muhimu vilivyokusanyika kwenye uso na hatimae kupatikana majuto kwa mtu, kwa sababu huenda akalipizwa kisasi pindi atakapoposhitakiwa mahakamani.

Pia ni haramu kuwatia alama wanyama kwenye uso, kwa lengo la kumsaidia mchungaji kuitambua mifugo yake au kurejeshewa pindi inapopotea. Hiki ni kitendo cha haramu kwa sababu ndani yake kuna kuharibu umbile la Mwenyezi Mungu na pia kupatikana mateso kwa mnyama.

Hata kama watu watahoji kwa kudai kuwa hiyo ni ada na mazoea ya kabilia lao, sawa, lakini inaweza kuwekwa alama hiyo kwenye sehemu nyingine yoyote isiyokuwa uso; kwa sababu uso ni sehemu iliyotukuzwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuupiga au kuutia alama kama hizo ni sawa na kuudhalilisha au kuudharau hali ya kuwa Mwenyezi Mungu ameutukuza.

KUMHAMA MUISLAMU ZAIDI YA SIKU
TATU BILA YA KUWA NA SABABU YA
KISHERIA.

Miongoni mwa hatua za shetani ni kuzusha chuki na husuda baina ya waislamu, na kukatana mapande. Na watu wengi wanaofuatisha hatua za shetani huwahama ndugu zao waislamu kwa sababu zisizokuwa za kisheria. Ima kwa kutofautiana kipesa, au kwa msimamo wa kipuuzi, na chuki huendelea muda mrefu na hatimae kuhamana na kupigana mapande. Na anaweza mtu akaapa kutomsemesha ndugu yake, au akatishia kutoingia nyumbani kwake, na anapokutana nae njiani humkimbia na kujitenga nae. Na anapokutana nae kwenye vikao fulani basi atapeana mikono na watu walioko kabla yake na watu walioko baada yake, na kumruka bila kupeana nae mikono.

Kitendo hiki ni miongoni mwa sababu za kupatikana udhaifu kwenye umma wa kiislamu, na kwa sababu hii ndio maana sheria ya kiislamu ikawa iko wazi na kutoa onyo kali kwa yejote yule mwenye kufanya kitendo hiki.

Imepokewa kutoka kwa Abii Huraira Mwenyezi Mungu awe radhi nae kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مَرْفُوعًا: "لَا يَحِلُّ لِمُسْلِمٍ أَنْ يَهْجُرْ أَخَاهُ فَوْقَ ثَلَاثٍ فَمَنْ هَجَرَ فَوْقَ ثَلَاثٍ فَمَاتَ دَخْلَ النَّارِ"

” Haifai kwa muislamu kumhama nduguye (piga pande) zaidi ya siku tatu, na mwenye kumhama nduguye zaidi ya siku tatu kisha akafa basi ataingia motoni. “ Abou Daud 5/215. Sahihil Jaamiy 7635.

Na imepokewa pia kutoka kwa Abii Haraadhi Al-Aslamiy Mwenyezi Mungu awe radhi nae kutoka kwenye hadithi marfuu:

عَنْ أَبِي خَرَاشَ الْأَسْلَمِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مَرْفُوعًا: "مَنْ هَجَرَ أَخَاهُ سَنَةً فَهُوَ بِسَفْكِ دَمِهِ".

” Mwenye kumhama ndugu yake mwaka mzima basi atakuwa) ni kama mtu aliyemwaga damu yake. “ Bukhariy Al Adad Hadithi No.406. Sahihil Jaamiy 6557.

Inatosha kwa kitendo hiki cha kuhamana na kupigana mapande baina ya waislamu kustahiki kunyimwa msamaha wa Mwenyezi Mungu. Imepokewa kutoka kwa Abii Huraira kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa:

عن أبي هريرة مرفوعاً: "تعرض أعمال الناس في كل جمعة مرتين، يوم الإثنين ويوم الخميس فيغفر الله لكل عبد مؤمن إلا عبداً بينه وبين أخيه شحناه فيقال: أترکوا أو أرکوا (يعني أخرموا) هذين حتى يفينا"

” Matendo ya watu huonyeshwa kila wiki mara mbili, siku ya jumatatu na siku ya Alkhamisi,

na husamehewa kila mja muumini isipokuwa mja mwenye kuwa na uhasama baina yake na ndugu yake. Hao huambiwa waacheni,

au wachelewesheni hawa wawili mpaka watakaporejea (kutoka kwenye ugomvi wao). " Muslim 4/1988.

Na mwenye kutubu kwa Mwenyezi Mungu kati ya wagomvi wawili hawa basi ni lazima arejee kwa mwenzake na kumtolea salamu (kumsalimia) na kumuomba msamaha. Ikiwa atafanya hivi na mwenzie akakataa, basi atakuwa ameondokana na dhima mbele ya Mwenyezi Mungu, na kubaki dhambi kwa yule mwenye kukataa.

Imepokewa kutoka kwa Abii Ayoub kutoka kwenye hadithi marfuu kuwa:

عن أبي أويوب مرفوعاً: " لا يحل لرجل أن يهجر أخاه فوق ثلات ليالٍ يلتقيان فيعرض هذا ويعرض هذا وخيرهما الذي يبدأ بالسلام".

"Haifai kwa mtu kumhama nduguye zaidi ya siku tatu. Ikawa wanapokutana huyu humpiga pande huyu na huyu humpiga pande huyu, na mbora wa wawili hawa ni yule mwenye kuanza kutoa salamu. " Bukhariy Fat'hul Baariy 10/492.

Ama kama zitapatikana sababu za kisheria kama vile kwa mtu kuacha kusali, au kung'ang'ania kushikamana na mambo machafu, na ikiwa ataona kumhama ni bora zaidi au kutamsaidia yule mwenye kufanya makosa na kurejea kwenye njia ya haki au kutamfanya ahisi kosa lake na kujirudi, hapo itakuwa kumhama mtu huyo ni wajibu.

Ama kama itakuwa kumhama hakumzidishii mtu huyu mwenye kufanya makosa isipokuwa kupinga zaidi, au hakuleti matokeo mazuri zaidi ya mfarakano, chuki, ukaidi, kiburi, ujeuri na kuongeza zaidi kufanya madhambi, hapa itakuwa haifai kumhama mtu huyu kwa sababu hakuna maslahi mazuri ya kisheria yatakayopatikana isipokuwa ni kuongezeka kwa ufisadi. Hivyo inakuwa njia nzuri zaidi ni kuendelea kumfanyia wema na ihsani, na kumpa nasaha njema na kumkumbusha kila wakati, kama vile Mtume alivyomhama

Kaabu bin Maalik na wenzake wawili muda
 ,
alipoona kwamba kufanya hivi kutaleta maslaha kwao, na akaacha kumhama Abdullah bin Ubayyi bin Saluul na wanaafiki wengine kwa sababu aliona kuwa kutowahama ni suluhi.

Na mwisho, haya ndio mionganini mwa mambo ya haramu yalioenea kwenye jamii nilioweza kuyakusanya kwa uchache. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa majina yake matukufu atupe khofu yenyeye kutuzuia baina yetu na maasi, na atupe twaa yenyeye kutufikisha kwenye pepo yake. Na atusamehe madhambi yetu na upotevu kwenye mambo yetu na atutosheleze na halali yake dhidi ya haramu, na tunamuomba hayo kwa fadhila zake, kwa sababu hakuna fadhila bora zisizokuwa zake. Na tunamuomba azikubali toba zetu, na ayasafishe madhambi yetu, hakika Mwenyezi Mungu yeye ndie mwenye kusikia zaidi na mwenye kujibu.

**Na rehema na amani za Mwenyezi Mungu
ziwe juu ya Nabiyyil umiyyi Muhammad
pamoja na aali zake na maswahaba wake
wote na kila sifa njema ni za Mwenyezi
Mungu, Mola wa walimwengu wote.**

**KITABU HIKI KIMETAFSIRIWA NA
KUREJEWNA KUSAHIHISHWA NA
KUINGIZWA KWENYE KOMPYUTA CHINI YA
USIMAMIZI WA KAMATI YA
WAISLAMU WAGENI.(WALIOREJEA).
MADINA. SAUDI ARABIA.**

*DIBAJI**I*1. KUMSHIRIKISHA MWENYEZI MUNGU 24*D*DIYAATHA: KUTOKUWA NA WIVU 116*K*KAMARI 136KUABUDU MAKABURI 26KUACHA UTULIVU KWENYE SALA 60KUAMINI KUWA NYOTA ZINA MAMLAKAKWENYE MATUKIO NA MAISHA YA
WATU 40KUCHEZA DADU (DICE) 241KUDANGANYA NASABA YA MTOTO NAKUMNASIBISHA NA MTU ASIYEKUWABABA YAKE, NA MTU KUMKANAMWANAE 118KUENDELEA KUFANYA BIASHARA BAADAYA ADHANA YA PILI SIKU YA IJUMAA 134KUFANYA IBADA KWA KUJIONYESHA (RIA)

..... 45

KUFANYA MCHEZO NA HARAKATIZISIZOKUWA NA MAANA KWENYE SALA

64

KUFICHA AIBU YA BIDHAA NA KUTOMFAHAMISHA MNUNUZI	129
KUIENDEA MISIKITI KWA YULE ALIYEKULA KITUNGUU MAJI AU THAUMU AU KITU CHENYE HARUFU MBAYA.....	72
KUINGIA KWENYE NYUMBA ZA WATU BILA RUHUSA.....	197
KUKAA FARAGHA BAINA YA	101
KUKAA JUU YA KABURI NA KUKANYAGA NA KUJISAUDIA HAJA KWENYE MAKABURI.....	226
KUKAA NA WANAAFIKI AU WATU WAOWU NA KUWAFANYA NDIO MARAFIKI WA KUSHIRIKIANA NAO.....	58
KULA HARAMU.....	172
KULA RIBA.....	121
KUMHAMA MUISLAMU ZAIDI YA SIKU TATU BILA YA KUWA NA SABABU YA KISHERIA.....	248
KUMUAJIRI MTU KWA KAZI FULANI KISHA UKAKATAA KUMLIPA UJIRA WA KAZI.....	155
KUMUANGALIA KWA KUSUDI MWANAMKE WA KANDO.....	113
KUMUINGILIA MKE AKIWA KWENYE HEDHI.....	91
KUMUINGILIA MKE KWA NYUMA.....	94
KUNONG'ONA WATU WAWILI MBELE YA MTU WA TATU.....	200

<u>KUOMBOLEZA KWENYE KIFO</u>	244
<u>KUONGOPA KWENYE NDOTO</u>	224
<u>KUPAKA RANGI NYEUSI KWENYE NYWELE</u>	217
<u>KUPOKEA NA KUTOA RUSHWA</u>	145
<u>KUPORA ARDHI;</u>	149
<u>KUREFUSHA NGUO</u>	202
<u>KURUSHA NDEGE</u>	49
<u>KUSENGENYA</u>	190
<u>KUSIKILIZA MAZUNGUMZO YA WATU HALI YA KUWA WENYEWE HA WAPENDI</u>	233
<u>KUSIKILIZA MUZIKI</u>	186
<u>KUTOFANYA UADILIFU BAINA YA WAKE</u> ..	98
<u>KUTOJIZUIA NA MKOJO</u>	229
<u>KUTUMIA VYOMBO VYA FEDHA NA DHAHABU KWA KULIA NA KUNYWA</u>	181
<u>KUUNGANISHA NYWELE KWA NYWELE ZA BANDIA KWA MWANAMUME NA MWANAMKE</u>	211
<u>KUWA NA UJIRANI MBAYA</u>	235
<u>KUWAOMBWA WATU BILA YA KUWA NA MATATIZO</u>	165
<i>L</i>	
<u>LIWATI (UFIRAJI)</u>	80

M

<u>MAAMUMA KUMTANGULIA IMAMU WAKE</u>	
<u>KWENYE SALA KWA KUSUDI</u>	66
<u>MWANAMKE KUMNYIMA UNYUMBA</u>	
<u>MUMEWE BILA YA KUWA NA UDHURU</u>	
<u>WA KISHERIA</u>	83
<u>MWANAMKE KUSAFIRI AKIWA PEKE YAKE</u>	
<u>BILA YA KUWA NA MAHARIMU WAKE</u> . 110	
<u>MWANAMKE KUTAKA TALAKA KWA</u>	
<u>MUMEWE BILA YA KUWA NA SABABU ZA</u>	
<u>KISHERIA</u>	85
<u>MWENYE KUKOPA KISHA AKAKATAA KULIPA</u>	
<u>DENI</u>	168

U

<u>UCHAWI NA UTABIRI NA UPIGAJI RAMLI</u> ..	35
<u>USAKUBIMBI - UDUKIZI</u>	194
<u>UTANGULIZI</u>	2, 4
<u>UZINIFU</u>	75

W

<u>WANAWAKE KUJIFANANISHA NA WANAUME,</u>	
<u>NA WANAUME KUJIFANANISHA NA</u>	
<u>WANAWAKE KWENYE MAVAZI, MANENO</u>	
<u>AU MAUMBILE</u>	213

محرمات استهان بها بعض الناس

تأليف

الشيخ / محمد بن صالح المنجد

اللغة السواحلية

يهدى ولا يباع



ادارة اوقاف

عبدالعزيز الراجحي

محرمات استهان بها بعض الناس

تأليف

الشيخ / محمد بن صالح المنجد

اللغة السواحلية

لجنة الدعوة والتعليم بالمدينة المنورة قسم الترجمة والنشر

طبع على نفقه

ادارة اوقاف صالح عبد العزيز الراجحي

غفر الله له ولوالديه وليذرته ولجميع المسلمين

يهدى ولا يباع